# UBABEDUME KATIKA SHEREHE ZA UPIGANISHAJI FAHALI KATIKA JAMII YA WAIDAKHO MAGHARIBI MWA KENYA

**AUSTINE INDULAGI ASALACHE**

**Tasnifu Iliyowasilishwa Katika Shule ya Mafuzu kwa Madhumuni ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili Katika Chuo Kikuu cha Chuka**

**CHUO KIKUU CHA CHUKA**

**OKTOBA 2024**

## UNGAMO NA IDHINI

**Ungamo**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada au stashahada katika Chuo Kikuu kingine chochote.

Sahihi.................................................. Tarehe...24/10/2024...

Asalache Austine Indulagi
AM12/45714/19

**Idhini**

Tasnifu hii imetahiniwa, ikapitishwa na kuwasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu.

Sahihi.................................................. Tarehe...22/10/2024...

Dkt. Onesmus Ntiba
Chuo Kikuu Cha Chuka

Sahihi.................................................. Tarehe...22/10/2024...

Dkt. Dorcas. M. Musyimi
Chuo Kikuu Cha Chuka

**HATILINZI**

©2024

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuiga, kurudufisha, kuhifadhi kwa njia ya kielektroniki au kutoa vipengele fulani kwa namna yoyote ile bila idhini kutoka kwa mwandishi au chuo kikuu cha Chuka.

# TABARUKU

Ninatabaruku kazi hii kwa mpendwa Asalache Coby Patrick, Dorothy Indulagi, dada yangu Joyce Kagai na mfadhili wangu Astrid Hareide

## SHUKURANI

Shukrani zangu za kwanza zimwendee Mola kwa kunipa uzima. Nikishukuru Chuo Kikuu cha Chuka kwa kunisajili na kunipa nafasi ya kuyaendeleza masomo yangu katika kiwango cha Uzamili. Ninawashukuru wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Chuka hususan wale walio katika Idara ya Fani na sanaa, kwa kunisaidia kuijenga kazi hii. Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Onesmus Gitonga Ntiba na Dkt. Dorcas Musyimi kwa uvumilivu, hekima, unyenyekevu na busara kubwa waliyoonyesha katika kunisaidia kuiboresha tasnifu hii hadi upeo wa ufanisi. Kwao nimejifunza si haba na walinikimu kwa mengi.

Shukrani za dhati ziwaendee wahadhiri wote walionifunza katika kiwango hiki cha Uzamili kama vile wasimamizi wangu wote wawili pamoja na Dkt. Allan Mugambi na Bw. Matundura Enock. Ninawashukuru kwa dhati kwa kuniwekea msingi madhubuti katika taaluma ya utafiti. Hakika, mchango wenu ulikuwa ni wa thamani kubwa kwangu. Mihadhara tuliyokuwa nayo kila mara ilifungua nadhari yangu na kunipa motisha wa kutia bidii. Ziara za kitaaluma kule nyanjani magharibi mwa Kenya hasa katika kumbi za kupiganisha fahali pamoja na kuwatembelea wazee wa kijiji kuwahoji wasailiwa katika jamii ya Waidakho ziliyapanua mawazo yangu na kunipa mwelekeo mpya kitaaluma. Hongereni nyote kwa kunitaalamisha. Kazi hii ni tunu kwangu.

Ninawapa ahsante wazamili wenzangu ambao tulipiga mbizi nao na kutiana shime; Bw. Lemmy Muriuki, Bw. Mutegi Newton, Bw. Karangi Kennedy na Madam Mwende Carolyne. Mungu awabariki sana kwa mchango wenu wa busara kiakademia. Ninawapa pongezi wazazi wangu wapenzi; Bw. Asalache Coby Patrick na Bi. Dorothy Indulagi Asalache kwa kujitolea kwa hali na mali na kuhakikisha kuwa nimepata kisomo. Dada zangu wapenzi Bi. Joyce Kagai na Bi. Joan Betty. Ingawa siwezi kuwataja wote kwa majina, kwa unyenyekevu na taadhima ningependa kuutambua mchango wao na kumwomba Mungu awajalie baraka tele.

## IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza ubabedume katika miviga ya upiganishaji fahali ambapo mtafiti alichunguza sifa za mwanamume zinazodhihirisha ubabedume, maudhui katika nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za upiganishaji fahali na ishara za kiuana zinazodhihirisha ubabedume katika miviga ya upiganishaji fahali. Ili kutimiza malengo haya, utafiti ulichunguza namna ishara maana, sifa za mwanamume na maudhui katika nyimbo hudhihirisha ubabedume. Ishara na nyimbo zinazoimbwa katika miviga ya upiganishaji fahali ni nyenzo kuu ya kumkumbusha mwanamume nafasi yake katika jamii katika kukuza utamaduni wa Waidakho. Mtafiti aliongozwa na nadharia mbili: nadharia ya Ubabedume ambayo iliasisiwa na Raewyn Connel miaka ya 1995. Nadharia hii ilieleza mahusiano ya wanawake na wanaume katika jamii. Kisha, nadharia ya Semiotiki iliyoasisiwa na Ferdinand de Saussure miaka ya 1970.nadharia hii ilichunguza maana, ishara-maana na misingi ya kitamaduni ya jamii. Uteuzi wa sampuli kimaksudi ulitumiwa kumchagua mwenyekiti wa mipango ya miviga ya upiganishaji fahali pamoja na kumbi zilizotumiwa kupiganisha fahali. Data asilia iliyotumiwa ilikusanywa kupitia hojaji, kusaili, utazamaji na uchunzaji-shiriki. Nyimbo na ishara zilizokusanywa zilitafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili kwa kuwa zilikuwa zimeimbwa kwa lahaja ya Ki-idakho. Nyimbo na ishara zilizotafsiriwa zilifanyiwa uchanganuzi kwa misingi ya madhumuni ya utafiti. Mtafiti alichanganua data kwa njia ya maelezo kwa kupanga, kuweka katika kanda za kunasa sauti, kisha kuihakiki na kuchanganua kwa kutazama idadi ya marudio kwa kila jibu. Umuhimu wa utafiti huu ni kuweka nyimbo za upiganishaji wa fahali katika kumbukumbu kwa kuwa matini za nyimbo zilizokusanywa zilihifadhiwa katika maandishi kwa matumizi ya kufundishia na utafiti wa usomi katika utanzu wa nyimbo. Kuwepo kwa kumbukumbu hizi kutarahisisha kupokeza kwa mitazamo na itikadi za ubabedume kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia miviga ya upiganishaji fahali ambapo nyimbo hutumiwa kama nyenzo ya kuwakumbusha wanaume na watoto wa kiume kuhusu misimamo na mitazamo ya jamii ya Waidakho.

## ABSTRACT

This study examined masculinity in bullfighting ceremonies where the researcher examined the characteristics of men that showed masculinity, content in the songs sung in bullfighting ceremonies and signs and symbols that potrayed masculinity in bullfighting ceremonies. In order to achieve these goals, the researcher examined how symbols, meanings, characteristics of men and themes in songs revealed masculinity since the songs sung during bullfighting are very key in potraying the Idakho traditions and their perception about the conduct of men and women in their community. Signs and songs sung during the bullfighting ceremony serves as an avenue to remind men of their role in the society as a way promiting cultural growth. The researcher was guided by two theories: the theory of Masculinity which was founded by Raewyn Connel in 1995 which explained the relationship between women and men in society. Also, the theory of Semiotics founded by Ferdinand de Saussure in the 1970s which examined meaning, sign-meaning and the cultural foundations of society. Purposive sampling was used to select the chairman of bullfighting ceremonies and venues used for bullfighting. The primary data was collected through questionnaire, interview, observation and participant observation. The songs that were collected were translated into Kiswahili since they were sung in the Idakho language. The songs that were translated were analyzed based on the objectives of the study. The researcher analyzed the data descriptively by organizing, recording, and then reviewing and analyzing the data by scrutinizing the number of repetitions for each response. The importance of this research was to keep the songs of the bullfighting in memory since songs that were collected will be preserved in books and on record for the use of teaching and scholarly research in the genre of songs. The existence of these songs and symbols used in bullfighting will serve as memories to facilitate the transmission of attitudes and ideologies of masculinity from one generation to another through bullfighting ceremonies where songs will be used as a tool to remind men and boys about their expectations and how to behave as they promote the culture of the Waidakho community.

## YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINI ............ ii**

**HATILINZI ............ iii**

**TABARUKU ............ iv**

**SHUKURANI ............ v**

**IKISIRI ............ vi**

**ABSTRACT ............ vii**

**YALIYOMO ............ viii**

**ORODHA YA PICHA ............ xii**

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ............ 1**

1.1 Usuli wa Mada ............ 1

1.2 Suala la Utafiti ............ 4

1.3 Malengo ya Utafiti ............ 5

1.4 Maswali ya Utafiti ............ 5

1.5 Umuhimu wa Utafiti ............ 5

1.6 Upeo wa Utafiti ............ 6

1.7 Maelezo Ya Istilahi Muhimu ............ 7

**SURA YA PILI: MWAUO WA MAANDISHI ............ 8**

2.1 Asili ya Waidakho ............ 8

2.2 Historia kuhusu Upiganishaji wa Fahali ............ 11

2.3 Dhana ya Ubabedume ............ 13

2.4 Tafiti za Awali kuhusu Ubabedume ............ 15

2.5 Dhana ya Nyimbo ............ 18

2.6 Msingi wa Nadharia ............ 20

2.6.1 Nadharia ya Ubabedume ............ 20

2.6.2 Nadharia ya Semiotiki ............ 22

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ............ 25**

3.1 Eneo la Utafiti ............ 25

3.2 Uteuzi wa Sampuli ............ 25

3.3 Vifaa vya Utafiti ............ 26

3.4 Ukusanyaji wa Data ........................................................................................ 26
3.5 Uchanganuzi wa Data........................................................................................ 27
3.6 Utafiti wa Awali ................................................................................................ 28
3.7 Maadili ya Utafiti .............................................................................................. 28

**SURA YA NNE: SIFA ZA MWANAMUME KAMA ZINAVYOJITOKEZA KATIKA MIVIGA YA UPIGANISHAJI WA FAHALI KATIKA JAMII YA WAIDAKHO ................................................................ 30**

4.1 Utangulizi ........................................................................................................ 30
4.2 Ubabedume katika Sherehe za upiganishaji fahali ............................................ 30
4.2.1 Mwanaume kutoonyesha Hisia ...................................................................... 31
4.2.2 Mwanaume kama anayemiliki Mali ............................................................... 33
4.2.3 Mwanamume kama mwenye Uwezo na Nguvu ............................................. 34
4.2.4 Mwanamume kama mwenye Busara ............................................................. 35
4.2.5 Mwanamume kama Shujaa na Jasiri ............................................................. 36
4.2.6 Mwanamume kama Mkware ......................................................................... 37
4.2.7 Mwanamume kama Mtu wa kutegemewa ..................................................... 38
4.2.8 Mwanamume kama mtu mkali mwenye msimamo dhabiti ........................... 40
4.3 Hitimisho ......................................................................................................... 41

**SURA YA TANO: MAUDHUI YA UBABEDUME KATIKA NYIMBO ZINAZOIMBWA KATIKA SHEREHE ZA UPIGANISHAJI FAHALI ..................................................... 43**

5.1 Utangulizi ........................................................................................................ 43
5.2 Maudhui ya Ubabedume .................................................................................. 43
5.2.1 Maudhui ya Ukatili ....................................................................................... 44
5.2.2 Maudhui ya Utajiri ........................................................................................ 45
5.2.3 Maudhui ya Ukware ..................................................................................... 46
5.2.4 Maudhui ya Unyanyasaji .............................................................................. 49
5.2.5 Maudhui ya Ukakamavu ............................................................................... 50
5.2.6 Maudhui ya Ujasiri ....................................................................................... 51
5.2.7 Maudhui ya Bidii na Kazi ............................................................................. 52
5.3 Hitimisho ......................................................................................................... 54

**SURA YA SITA: ISHARA ZA KIUNA KATIKA SHEREHE ZA UPIGANISHAJI FAHALI KATIKA JAMII YA WAIDAKHO ........ 55**

6.1 Utangulizi ........ 55

6.2 Fahali ........ 55

6.2.1 Fahali kama Mwanamume Shujaa ........ 55

6.2.2 Fahali kama Ishara ya Utajiri ........ 57

6.3 Kifaa cha Isukuti ........ 58

6.4 Mapambano ya Fahali ........ 60

6.5 Majina ya Fahali ........ 60

6.5.1 Spana ........ 61

6.5.2 Osama ........ 61

6.5.3 Aguero ........ 61

6.5.4 Tinga ........ 62

6.5.5 Master Key ........ 62

6.6 Maandalizi ya mapambano ya fahali ........ 63

6.7 Ishara katika Nyimbo ........ 64

6.8 Klabu na pembe za Swara ........ 66

6.8.1 Klabu ........ 66

6.8.2 Pembe za swara ........ 67

6.8.2.1 Mlio wa pembe za swara kuashiria siku ya mapambano ........ 67

6.9 Hitimisho ........ 67

**SURA YA SABA: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI ........ 69**

7.1 Muhtasari ........ 69

7.2 Hitimisho ........ 70

7.3 Mapendekezo ya Utafiti zaidi ........ 71

**MAREJELEO ........ 73**

**VIAMBATISHO ........ 77**

Kiambatisho 1: Nyimbo zilizokusanywa katika sherehe za upiganishaji katika jamii ya Waidakho ........ 77

Kiambatisho 2: Picha ya Mtafiti katika sherehe za kupiganisha fahali ........ 80

Kiambatisho 3: Ramani ya Eneo la Ikolomani ........ 81

Kiambatisho 4: Maswali ya Hojaji (dodoso) kwa Fanani na Wenyekiti wa Maandalizi ya Upiganishaji Fahali ................................................82
Kiambatisho 5: Orodha ya Wasailiwa......................................................................84
Kiambatisho 6: Idhini kutoka kwenye Tume ya Maadili ........................................85
Kiambatisho 7: Idhini kutoka NACOSTI.................................................................86

## ORODHA YA PICHA

Picha 1: Picha ya fahali kwa jina Aguero ....................................................................55

Picha 2: Ngoma za Isukuti ................................................................................58

Picha 3: Klabu ambazo zimeinuliwa juu katika sherehe ya kupiganisha fahali .........66

Picha 4: Picha hii inaonyesha kifaa kilichoundwa kutokana na pembe za swara ambacho hutumika kuwajulisha watu siku ya mapambano ya fahali. ..........67

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Waidakho ni mojawapo kati ya makundi ya Waluhya. Jamii hii inaishi katika kaunti ndogo ya Kakamega Kusini, kaunti ya Kakamega. Waluhya ni jamii ya tatu kwa ukubwa nchini Kenya na wanaishi sehemu za magharibi ya nchi na pia sehemu za kaskazini mwa Bonde la Ufa haswa sehemu za Kitale na Kapsabet. (Wambunya, 2005). Waluhya pia wanapatikana mashariki mwa Uganda. Waluhya si kundi moja la watu wenye asili moja ila ni neno la msingi kwa vikundi vya lugha kumi na tano zikiwemo; Wanga, Banyole, Kisa, Maragoli, Isukha, Batirichi, Idakho, Kabras, Samia, Bukusu, Banyala, Marama, Marachi, Batachoni, na Bastosto (Wambunya, Keshatajwa).

Kwa mujibu wa Wambunya (keshatajwa), jamii hii hushiriki utamaduni kama sehemu kuu ya kupitisha maadili na matakwa ya jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Tamaduni hizi pia huwakilisha sehemu kuu ya kuwaburudisha wanajamii na kuwaliwaza haswa wanapokumbana na matatizo mbalimbali katika jamii. Mchezo wa upiganishaji fahali ni mojawapo wa tamaduni ambazo zimehifadhiwa na kukuzwa katika jamii ya Waidakho.

Historia ya kupiganisha fahali inafafanuliwa kutoka nchi za Mesopotamia ambapo fahali walikuwa wanyama wenye fahari sana kwani waliabudiwa na kutolewa kama kafara. Kulingana na visasili vya nchi za Mesopotamia, mchezo huu ulitokana na Gilgamesh na Enkidu (2250-1900 KK) walipopigana na wakamuua fahali wa mbinguni (Hemingway,1932). Katika nyakati hizo, kupiganisha fahali kulilinganishwa na falsafa za Wagiriki na visakale vyao pamoja na visaviini. Mitchell (1991) anaeleza kwamba upiganishaji fahali ulihusishwa na Warumi ambapo mapambano ya wanyama na binadamu yalifanywa kuwa mashindano. Ushahidi unadhihirika kutokana na kuwepo kwa fahali hao kupitia kwa pembe zao zilizoangikwa ukutani wakati wa enzi hizo.

Katika nchi za Uhispania, maonyesho ya upiganishaji fahali hufanywa mwezi wa Machi hadi Oktoba kila mwaka. Walijivunia fahali shupavu 'Toreros' ambaye alipigana na alilinganishwa na mchezaji wa mpira ulimwenguni. Mchezo huu ulifadhiliwa na watu mbalimbali ambao pia ni mashabiki sugu wa mchezo huu.

Vyombo vya habari vilitumika kueneza kwa wale ambao hawakuhudhuria na pia kufanya mchezo huu wa upiganishaji fahali kuwa maarufu duniani. Upiganishaji fahali ulienea katika sehemu mbalimbali ikiwemo Ufaransa katika karne ya kumi na tisa na katika bara la Afrika, Uropa na Asia katika enzi za Warumi. (McCornick, 2000)

Kila jamii ilichukulia upiganishaji fahali kuwa wa upekee na hivyo kupelekea haja ya kuenea kwake kote ulimwenguni ( Kabaji ,2005). Kulingana na maoni ya Foley (2014), upiganishaji wa fahali ulianzishwa na Wareno na kupamba moto katika sehemu za Unguja na Pemba. Wakaazi wa sehemu hizi walirejelea mchezo huu kama *mchezo wa ng'ombe.* Mchezo huu ulikuwa na utaratibu na kanuni ambapo fahali alifaa kuvutwa kwa kamba na hakufaa kuumizwa wakati wa vita.

Nchini Kenya katika jamii ya Wawanga Magharibi mwa Kenya, wanajamii hupiganisha fahali baada ya mazishi ya shujaa aliyeaga kama njia ya kuonyesha heshima zake za mwisho na ishara ya ushujaa wake kwa jamii hiyo. Wanajamii walifaa waige mfano wake kupitia kwa fahali mshindi ambaye licha ya makali ya fahali mwenzake aliweza kujikwamua na kushinda vita. Miviga hii ilifanyika kwenye kaburi la marehemu ambapo kaburi lilitandazwa kama njia ya kumuaga na kumtakia mema katika ulimwengu wa pili. Baaada ya miviga hii, walioshabikia fahali mshindi walielekea moja kwa moja hadi shambani mwa marehemu na kukatakata mimea yoyote iliyokuwemo mle shambani. Wakaazi wa eneo hili waliamini kuwa kukata mimea hiyo ni kuondoa vizingiti vyote ambavyo vingezuia ushujaa wake kuenea katika jamii hiyo. Baada ya siku kadhaa mimea ilinawiri tena na kutoa rotuba nyingi zaidi. Mabadiliko haya ya kuwepo kwa mazao maradufu ni ishara ya shujaa wao kuwa na furaha na amani katika ulimwengu wa pili. (Ouma, 2016)

Mapambano ya fahali yalijitokeza kama ishara ambapo yalisawiri jinsi wanajamii wanavyopigana na changamoto zinazowakumba (Kibigo, 2019). Fahali mshindi huwakilisha mwanamume ambaye amejikwamua na kustahimili matatizo anayokumbana nayo katika ulimwengu. Kwa mujibu wa Kibigo (keshatajwa), wanakijiji hata hivyo wasingemudu kungojea hadi kifo cha shujaa mwingine. Kutokana na sababu hii watu walibadili dhima ya mapambano ya fahali na kuwa ya kuburudisha wanajamii. Kwa sasa sherehe hizi hufanyika kila Jumamosi na wakati wa msimu wa

Krisimasi kinyume na ilivyokuwa hapo awali ambapo dhima ilikuwa kuwasifu na kuwadhihaki mashujaa walioaga.

Hata hivyo kuwepo kwa nyimbo katika sherehe hizi ni kuwaliwaza wanajamii na kuwatia nguvu. Nyimbo hizi huandamana na mdundo wa ngoma na watu waliobeba silaha kuashiria ujasiri na jinsi wamejiandaa kupigana dhidi ya changamoto za aina yote maishani. Nyimbo ni istilahi inayoeleza fikra, mawazo na haswa hisia za binadamu zilizopangwa katika beti kimantiki (Miruka, 2003). Nyimbo katika sherehe za upiganishaji fahali huelezea fikra na hisia kulingana na jinsi maneno huteuliwa kusukwa na kufinyangwa na fanani ili kuvutia msikilizaji na mwimbaji. Licha ya nyimbo hizi kuburudisha na kumvutia msikilizaji, hutekeleza dhima kuu katika maisha ya kila siku ya wanajamii na jinsi wanavyohusiana na mazingira yao na katika hafla mbalimbali za kijamii kama vile dini, harusi au jando. Hata hivyo, nyimbo hulenga jamii husika na ni sharti ziwe na ujumbe unaoeleweka.

Nyimbo huwa na nafasi muhimu katika kueleza harakati za maisha ya watu katika jamii inayohusika, desturi, hulka na imani zao na kuwatambulisha kutokana na jamii zingine zilizo na tamaduni tofauti (Kipury, 2002). Madai haya yanajikita katika kueleza ukweli kwamba nyimbo si mali ya mwimbaji tu bali inafaidi jamii kwa ujumla katika kujitambulisha. Kinachorejelewa katika nyimbo hizi ni ujumbe unaosimbwa kwa wanajamii husika kwa kuwa zinaangazia maisha ya jamii kwa ujumla kwa kuangazia matakwa ya jamii, kuwaburudisha na kuwaliwaza hasa wanapokumbana na changamoto mbalimbali katika jamii yao. Kauli hii ilimchochea mtafiti kuchunguza utamaduni wa Waidakho na imani yao kuhusu ubabedume kupitia nyimbo zinazoimbwa wakati wa upiganishaji fahali

Tafiti za awali (Hemingway, 1932) zimeonyesha kuwa sherehe za upiganishaji fahali zilianza kama mashindano kati ya binadamu na fahali. Maendeleo na mabadiliko ya jinsi sherehe huendeshwa yamebadilika haswa katika jamii ya Waidakho kadri muda unavyosonga kuakisi mazingira na wakati. Mabadiliko haya yanajitokeza kupitia jinsi wanajamii huonyesha hisia, mihemko, msimamo, mila na historia kupitia matendo na nyimbo. Kulingana na Kabaji (keshatajwa), kuhusika kwa wanajamii wote katika sherehe za mapambano ya fahali ni ishara tosha ya kuthibitisha kuwa upiganishaji fahali

miongoni mwa Waidakho umepewa nafasi na dhima kuu kutokana na majukumu yake na katika kudumisha utamaduni na hali ya maisha ya Waidakho katika kufanikisha dhima mbalimbali za kijamii kama burudani. Ingawa sherehe hizi hutumika kama burudani; kupitia nyimbo na ishara zinazohusika, husheheni jumbe muhimu kwa wanajamii kwa lengo la kukuza sifa za mtoto wa kiume na suala la ubabedume. Ingawa kuna utafiti uliofanywa kuhusu upiganishaji fahali (McCornick, 2000; Kabaji, 2008; Mutulu, 2014; Kibigo, 2019), wataalamu hawajaangazia utamaduni wa upiganishaji fahali katika jamii ya Waidakho.

Utafiti huu ulichochewa na sababu kuwa, upiganishaji fahali ni kipengele kimojawapo cha fasihi simulizi ambacho hunuia kukuza utamaduni wa jamii ya Waidakho. Aidha, utafiti huu ulichochewa na sababu kuwa sherehe za upiganishaji fahali zina upekee wake kwa kuwa mchezo huu unatokana na utamaduni na mila za jamii ya Waidakho ambazo hupitishwa kwa vizazi vijavyo. Mtafiti alichochewa pia na haja ya kutaka kuhakiki ishara katika sherehe za upiganishaji fahali kupitia sifa za mwanamume na maudhui ya ubabedume katika nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za upiganishaji fahali. Hii ni kwa sababu, nyimbo zilizoimbwa kabla ya kubuniwa kwa mchezo huu wa upiganishaji fahali zilihusu maudhui ya kazi, kufunga ndoa, tohara, bembelezi na kuliwaza waliofiwa. Kwa hivyo majukumu ya mwanamume yalipitishwa kwa kizazi kijacho kupitia mafunzo na wazee haswa wakati wanapopashwa tohara.

### 1.2 Suala la Utafiti

Fasihi simulizi ina mchango mkubwa katika jamii kwa sababu inampa mtoto tajriba ya elimu inayochangia kukua na kumtayarisha katika maisha ya usoni kulingana na fasihi hiyo. Mojawapo ya tanzu za fasihi simulizi ni miviga. Miviga imeshughulikiwa katika utafiti wa fasihi simulizi kutoka jamii za kiafrika. Waidakho wana miviga yao inayoeleza itikadi, falsafa na hali ya maisha wa watu. Mojawapo ya miviga ya Waidakho ni upiganishaji wa fahali. Miviga ya sherehe za upiganishaji fahali imekuwa sehemu kuu katika kudumisha utamaduni na hali ya maisha ya Waidakho katika kufanikisha dhima mbalimbali za kijamii kama burudani. Ingawa sherehe hizi hutumika kama burudani; kupitia nyimbo na ishara zinazohusika, husheheni jumbe muhimu kwa wanajamii kwa lengo la kukuza sifa za mtoto wa kiume na kukuza maudhui ya ubabedume miongoni mwa jamii ya Waidakho. Kutokana na kuwepo kwa pengo hili,

mtafiti alichochewa na haja ya kuchunguza hali ya maisha na tamaduni za Waidakho katika kukuza ubabedume katika sherehe za upiganishaji fahali kupitia nyimbo na ishara.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti uliongozwa na malengo yafuatayo:

i. Kuchunguza sifa za mwanaume kama zinavyojitokeza katika nyimbo zinazoimbwa katika miviga ya upiganishaji fahali katika jamii ya Waidakho.
ii. Kujadili maudhui ya ubabedume katika nyimbo zinazoimbwa katika miviga ya upiganishaji wa fahali katika jamii ya Waidakho.
iii. Kuchunguza ishara- maana za kiuana zinazojitokeza katika miviga ya upiganishaji fahali katika jamii ya Waidakho.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo;

i. Ni sifa gani za mwanamume zinazojitokeza katika nyimbo zinazoimbwa katika miviga ya upiganishaji wa fahali katika jamii ya Waidakho?
ii. Maudhui ya ubabedume hujitokeza vipi katika nyimbo zinazoimbwa katika miviga ya upiganishaji wa fahali katika jamii ya Waidakho?
iii. Ishara-maana zipi za kiuana zinazojitokeza katika miviga ya upiganishaji fahali katika jamii ya Waidakho?

### 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utasaidia kufanikisha uhifadhi wa nyimbo za upiganishaji wa fahali katika jamii ya Waidakho kama kipera muhimu cha fasihi simulizi ambacho ni nyenzo ya kusaidia kuelewa mielekeo ya jamii dhidi ya mwanamume katika jamii kwa ujumla. Matokeo ya utafiti huu yatahifadhi utamaduni, mila na desturi za Waidakho kwa matumizi ya kizazi kijacho. Utafiti huu utaweka nyimbo za upiganishaji wa fahali katika kumbukumbu kwa kuwa matini za nyimbo zitakazokusanywa zitahifadhiwa katika maandishi kwa matumizi ya kufundishia na utafiti wa usomi katika utanzu wa nyimbo. Kuwepo kwa kumbukumbu hizi kutarahisisha kupokeza mahitaji ya jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Katika muktadha wa masuala ya kijamii, utafiti huu utasaidia kizazi kijacho cha Waidakho kuchunguza masuala ya kiuana kwa kina kupitia jicho la fasihi simulizi hasa nyimbo za upiganishaji fahali ambapo atafahamu mwanamume vyema na kuzitambua sifa zao, ishara maana katika sherehe za upiganishaji fahali na jinsi wanavyoathiriwa na tabia za wazazi wao na kizazi cha leo. Hili ni muhimu kwa kuwa wataweza kukuza mtazamo wao na imani yao kuhusu mwanamume na kukuza majukumu ya mwanamume pamoja na sifa zake katika jamii.

Katika uwanja wa fasihi, utafiti huu utawachochea wanafasihi kuzingatia wahusika wa kiume katika utafiti wa fasihi simulizi hasa miviga. Mwanamume angesawiriwa kwa kuzingatia mazingira anamoishi kwa lengo la kusawiri jamii za kiafrika katika uhalisia wake. Utafiti huu utasaidia wahakiki wa fasihi simulizi kuwarejelea wahusika hasa wa kiume hasa katika uhakiki. Hii inatokana na nafasi ya wahusika katika kujenga taswira ya mambo halisi yanayoibuka katika jamii.

### 1.6 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika utanzu wa fasihi simulizi hasa kipera cha miviga ya jamii ya Waidakho. Utafiti huu ulizingatia sherehe za upiganishaji wa fahali katika jamii ya Waidakho kwa kufafanua sifa za mwanamume zinazojitokeza katika nyimbo zinazoimbwa katika miviga ya upiganishaji fahali, kueleza maudhui ya ubabedume katika nyimbo zinazoimbwa katika miviga ya upiganishaji fahali na kutathmini ishara za kiuana zinazojitokeza katika miviga ya upiganishaji fahali. Uwanja wa fasihi simulizi ni pana wenye vipera ambavyo ni vigumu kuvichambua vyote. Hivyo, utafiti huu ulijikita katika kuchambua miviga ya upiganishaji fahali kwa kuangazia nyimbo na ishara. Nyimbo na ishara hizi zilichangia utafiti huu kwa kukusanywa nyanjani.

## 1.7 Maelezo Ya Istilahi Muhimu

**Fahali:** Ni Ng'ombe dume mzima mwenye zaidi ya misuli na fujo ambaye hutumiwa kufanikisha mchezo huu wa upiganishaji fahali na huwa ishara muhimu katika tamaduni za Waluhya haswa Waidakho na Waisukha.

**Ishara:** Ni kitu au dhana zinazobainika katika sherehe za upiganishaji fahali kwa njia ya kutazama na macho kinachodokeza kutokea kwa suala la ubabedume.

**Miviga ya Waidakho:** Ni Sanaa ya maonyesho ya jamii ya Waidakho inayoambatana na shughuli nyingine kama vile: uimbaji, upigaji muziki na uchezaji ngoma.

**Taswira:** Maneno yanayoibua picha akilini mwa msomi au mtafiti katika kutambua nafasi ya mwanamume katika jamii katika kutambua suala la ubabedume katika jamii ya Waidakho.

**Uana**: Ni hali ya kibiolojia inayotokana na tofauti za mwili kama vile viungo vya uzazi. Mara nyingi, Waidakho hugawanywa kulingana na uana wao kuwa wanaume au wanawake.

**Ubabedume:** Mfumo wa jamii ya Waidakho ambao humpa mwanamume nguvu na idhini ya kufanya mambo fulani kama kufuga mifugo na kushinda katika vita.

**Utamaduni:** Ni mbinu ambazo Waidakho hukabili maisha yao katika mazingira wanamoishi kwa kuangazia desturi na imani yao.

# SURA YA PILI

# MWAUO WA MAANDISHI

## 2.1 Asili ya Waidakho

Kulingana na Wambunya (2005) Waluhya ni jamii ya tatu kwa ukubwa nchini Kenya. Jamii hii hupatikana sehemu za magharibi mwa nchi na pia sehemu za kaskazini mwa Bonde la Ufa haswa sehemu za Kitale na Kapsabet. Pia wanaishi mashariki sehemu ya Uganda. Kwa mujibu wa Wambunya (Keshatajwa), Waluhya hawapo kama kundi moja la watu wenye asili moja lakini badala yake ni neno la msingi kwa vikundi vya lugha kumi na nane zikiwemo; Batachoni, Idakho, Samia, Marama, Kisa, marachi, Batsotso, Batirichi, Bukusu, Wanga, Maragoli, Kabras, Banyala, Banyole, Khayo, Gisu, Bayei na Isukha.

Kwa mujibu wa Tamale (2005), mbali na Waluhya kuwa na lugha na lahaja mbalimbali, pia wanashiriki sifa za kawaida za kitamaduni kama vile ndoa, tohara na sherehe za maziko kama sehemu kuu ya utamaduni wao. Jamii ya Waluhya ina asili ya mfumo dume ambapo chini ya mwanamume, wanawake wamesawiriwa kwa kupewa majukumu na sifa ambazo zinawasawiri kuwa wanyonge wakilinganishwa na wanaume kupitia lugha, nyimbo na methali. Utafiti uliofanywa na Khamala (2009) ulionyesha kuwa utambulisho katika jamii ya Waluhya unatokana na ukoo wa wanaume na hivyo kufanya maamuzi ni hifadhi ya mwanaume katika jamii na iwapo mwanaume ameaga basi mwanamke hana budi kuwatafuta baadhi ya wazee katika jamii hiyo kuwapa ushauri au kuwapa mwelekeo. Ilikuwa kinyume cha matarajio kwa mwanamke kutekeleza majukumu ya mwanaume pasipo ushauri wa wazee.

Kwa mujibu wa Wanjala (2007), Waluhya huwa na mila kuhusu miiko ya chakula, uzazi, jando, ndoa na taratibu za maziko ambazo kulingana na tamaduni zao kwenda kinyume na mila hizo ni kukiuka sheria zao za kitamaduni. Hata hivyo, mabadiliko na upinzani katika baadhi ya vipengele vya Ukristo na umagharibi vimezua mabadiliko kwa kiasi fulani ila baadhi ya makundi ya Waluhya kama Waidakho wangali wanafuata mfumo wa ubabedume ambapo inachukuliwa kuwa mwanaume ana nguvu zaidi juu ya mwanamke. Waluhya wanafanya tohara kwa wanaume kama njia ya kuwandaa katika ulimwengu wa utu uzima. Aidha waliopashwa tohara hufunzwa jinsi ya kukabiliana na changamoto mbalimbali katika jamii.

Tohara katika jamii ya Wabukusu ni miviga ambayo imeheshimiwa na kupewa nafasi kuu katika utamaduni wao.  Miviga hii hufanywa baada ya miaka miwili mvulana anapotimiza umri wa miaka kumi na minne. Hata hivyo kipindi cha kupasha tohara hutofautiana katika kabila moja ndogo hadi lingine. Katika kabila ndogo la Idakho, mvulana hupashwa tohara wakati wowote iwapo familia ina uwezo kwa kuwa zoezi nzima ni gharama. Hata hivyo, mvulana akihisi amebaleghe, anafaa kupata idhini kutoka kwa wazazi wake, na waalike jamaa na marafiki nyumbani kwao washuhudie "wakikabiliana" na kisu. (Mbachi, 2013).

Parpart (2016) anaeleza kuwa, wavulana na wanaume kwa ujumla wamesawiriwa kuwa bora kuliko wanawake na wao ndio muhimu zaidi katika jamii ya Waidakho. Wanawake wamehusishwa katika shughuli za malezi na kulinda maboma zao kwa kutekeleza shughuli za kimsingi kama vile kudumisha usafi, kupikia familia zao na kuwapa watoto wasichana mwelekeo mwema kuhusiana na jinsi ya kuwa na maadili mema katika jamii. Katika utamaduni wa jamii ya Waluhya, kama ilivyo tamaduni zingine ulimwenguni, tabia na mitazamo ya kijamii hukuzwa na kupitishwa kwa kizazi kijacho katika viwango mbalimbali vya maisha. Wasichana walifundishwa kuwa wake na akina mama wakati wa sherehe kama vile kujifungua, ndoa, unyago au tohara ili waheshimu waume zao na kuimarisha usalama katika ndoa zao. Kwa hivyo, mke mwema alijulikana kwa uwezo wake wa kuzaa, kulea familia yake na kumtunza mume wake vizuri. Katika suala hili, wanaume walipewa majukumu ya juu katika jamii, na wanawake kushika nafasi ya pili.

Kwa mujibu wa Mwayuuli (2003), Ki-Idakho ni lahaja inayozungumzwa na watu waitwao Waidakho na katika umoja Mwidakho. Jamii hii inaishi katika kaunti ya Kakamega. Mahali wanapoishi panaitwa Ikolomani ambapo ndilo Jimbo la uchaguzi pekee katika eneo hili, mji mkuu ukiwa Malinya. Idakho imegawika katika makundi kumi (10); Bamuhali, Bamanyisi, Bashikulu, Bamusali, Bakhwese, Bamalava, Bashirika, Bashiangala, Bangolori na Bamahani aidakho walihamia maeneo ya Kakamega wakitafuta mashamba ya ukulima miongoni mwa sababu zinginezo. Kunao waliosafiri kutoka sehemu za ziwa la Victoria kama vile Bamuhali and Bamanyisi. Kuna wengine waliotoka katika jamii ya Wanga kwa mfano Bamusali na Bakhwese. Jamii kama vile Bashimuli, Bashikulu wanadai kutoka katika sehemu za Nandi.

Makazi ya kwanza ya Wabantu yanaelezwa kupitia nadharia kadha. Mojawapo ya nadharia hizi ni ile inayosema kuwa, maeneo yaliyo katikati mwa Nigeria na Cameroon ndiyo makazi ya awali ya Bantu. Kutoka maeneo ya Cameroon, kundi hili la Bantu lilihamia misitu ya Kongo ambako baadaye lilihamia maeneo ya Afrika Mashariki kupitia Uganda na mlima Elgon. Jamii ya Waluhya ambayo inajumuisha Waidakho ilihamia sehemu zilizo karibu na mlima Elgon kati ya miaka 1400 na 1600. Waidakho walikuwa wakifuga mifugo na pia walikuwa wakulima. Katika karne ya kumi na sita, iliwabidi Waluhya kuhama na kusambaa kuelekea maeneo mengine magharibi mwa Kenya hadi maeneo ya Ziwa Victoria kutokana na mavamizi ya Wanandi na mizozo ya shamba. Kundi hili la Waluhya lilihamia sehemu za Bunyore, Nandi na Bungoma. Jamii ya Waidakho ilianza kujitenga na kuhamia sehemu za Kakamega Kusini kwa lengo la kuyatafuta mashamba ya ukulima na vyakula vya kulisha mifugo wao (Kiruthu, 2011).

Jina Waidakho linatokana na mitazamo miwili. Mtazamo wa kwanza unashikilia kwamba Mfalme Mumia ambaye alitawala katika jamii ya Wawanga haswa wakati wa sherehe za kifalme angewaitisha watu waende katika *bonde la Mwitokho* ambalo lilikuwa limejulikana sana katika uuzaji wa ng'ombe (Masingu, 2013). Ng'ombe hawa walinunuliwa ili wachinjwe katika sherehe hizo. Watu hawa wangesema kuwa, "Tumetoka Mwitokho." *Bandu bu Mwitokho bakhuhele tsingo'mbe* (watu wa Mwitokho wametupa ng'ombe za mfalme). Kutokana na misafara hii, watu hawa waliamua kuwa wasingerudi kwao na kisha wakaanza kuishi *Mwitokho*. Watu hawa wakaanza kujiita watu wa *Mwitokh*o na baadaye jina hili likaenea na kuwa Idakho.

Mtazamo wa pili unashikilia kwamba kulikuwa na msafiri ambaye alikuwa mtu tajika. Mtu huyu alinuia kuwatembelea jamaa yake katika eneo hili la Idakho. Katika safari hii alikuwa na wafuasi wake waliompa ulinzi. Walipokuwa safarini, walishambuliwa na simba. La kushangaza ni kwamba wafuasi wake walitoweka akabaki peke yake. Simba yule alimzidi na nguvu na kisha kumuuma sehemu ya makalio. Aliporudi kwao aliweza kuwasimulia jamaa zake yaliyomkumba. Watu walihusisha hadithi hiyo na sehemu hii ya Idakho kwa jina Idakho na wakaanza kuita wakaazi wa eneo hilo Waidakho. Kumaanisha watu wanaoliwa matako (Shiracko, 2016).

Historia ya Waluhya ilikuwa na manufaa kwa mtafiti kwa kuonyesha nafasi ya mwanamume kwa kurejelea sifa na majukumu ambayo yamekuwepo na kupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Aidha, historia hii ilimpa mtafiti mwelekeo wa tamaduni ya Waidakho kwa kuangazia uhusiano uliopo kati ya mwanamume na mwanamke kwa kujikita kwa imani na desturi za Waluhya. Aidha historia ya Waidakho ilimpa mtafiti msukumo wa kuelewa dhana mbalimbali katika sherehe za upiganishaji fahali zinazodhihirisha ubabedume.

## 2.2 Historia kuhusu Upiganishaji wa Fahali

Historia ya mapambano ya fahali imeelezwa kupitia mtazamo kuwa, jamii ya Waidakho iliunganishwa na mchezo wa jadi wa mashindano baina ya watu wawili waliodaiwa kuwa mashujaa. Viongozi katika jamii kumi na sita waliandaa sherehe hizi baada ya kila mwaka. Viongozi hawa walipaswa kuwachagua watu walioaminika kuwa hatari na wenye nguvu mno waende kuwakilisha jamii yao kama mashujaa. Shujaa aliyeshindwa kwa kuwa na hasira angempiga mshindani wake bila kutarajia na kumsababishia majeraha. Wafuasi wa aliyeumizwa kwa hasira wangeanza kupigana wenyewe kwa wenyewe. Kutokana na hali hii watu waliweza kuumizana na wengine kufariki kutokana na vita hivyo. (Jakinda, 2005).

Viongozi katika jamii hizi kumi na sita za Waidakho waliweza kutazamia suala hilo na kutafuta njia mbadala ya kuendeleza michezo yao. Waliweza kuamua kuwa badala ya watu kupigana na kuumizana ni heri wapiganishe wanyama ambao ni fahali (Bearak, 2014). Watu katika jamii mbili za Bashimuli na Bamusali waliamua kuandaa mapambano ya fahali kama mchezo wa kuwaburudisha wanajamii badala ya mapambano ya watu. Fahali aliyeshindwa angetoroka na hivyo hakukuwepo na mgogoro kuhusiana na fahali mshindi na yule aliyeshindwa. Ili kuimarisha mchezo huu, orodha ya miviga hii iliandaliwa katika jamii ya Waidakho kila Jumamosi.

Mutulu (2014) anafafanua kuwa, mapambano ya fahali yalipewa dhima kuu na fasili mbalimbali katika jamii ya Waidakho; kwanza, yalitokea kama vita vya kumdhihaki aliyeaga na aliyewahi kuwa shujaa. Iwapo shujaa yeyote katika jamii hii aliaga, baada ya mazishi ya shujaa yule, wanakijiji walijumuika na fahali wawili wakiwa na wafuasi wake. Fahali hawa walipopigana, wafuasi walihakikisha kuwa kaburi la marehemu

limetandazwa kwa mchanga kama njia ya kuonyesha ubingwa aliokuwa nao na kumtunuku heshima zake za mwisho. Pia wanajamii walifaa waige ubingwa wake ili kuendeleza ushujaa wa marehemu. Kwa kufanya hivi aliyeaga angekuwa na amani na iwapo haya yasingetukia basi angebakia kuwa kikwazo katika familia yake na jamii kwa ujumla. Wanakijiji hawa walijihami kwa silaha kama vile panga, rungu na baada ya mapambano haya walikatakata chochote kilichokuwepo katika boma la shujaa aliyeaga huku wakiimba nyimbo za kumsifu shujaa wao. Inaaminika kwamba mimea iliyokatwa ilinawiri tena na kutoa mazao mengi.

Upiganishaji wa fahali ulianza kujitokeza kama ishara ya kujikwamua kutokana na matatizo ya kijamii (Ouma, 2016). Kulingana na fasihi simulizi ya Waidakho mapambano haya yalisawiri jinsi wanajamii wanavyopigana na changamoto zinazowakumba. Fahali mshindi ni ishara tosha ya mwanajamii ambaye amejikwamua na kustahimili matatizo anayokumbana nayo. Nyimbo huambatana na miviga hii ya upiganishaji fahali ili kuwaliwaza wanajamii, kusifu shujaa wa kiume wa kizazi kijacho baada ya marehemu na kuwatia nguvu. Nyimbo hizo pia hukashifu na kuonya dhidi ya tabia hasi. Nyimbo hizi huandamana na mdundo wa ngoma na watu waliobeba silaha kama ishara ya ujasiri dhidi ya changamoto za aina yoyote maishani. Wanakijiji wasingemudu kungojea hadi kifo cha shujaa mwingine. Kutokana na sababu hii watu walibadili dhima ya mapambano ya fahali na kuwa ya kuburudisha wanajamii. Kwa sasa sherehe hizi hufanywa kila Jumamosi kupitia mwaliko kinyume na ilivyokuwa hapo awali ambapo dhima ilikuwa kuwasifu na kuwadhihaki mashujaa walioaga.

Ni lazima fahali apewe dawa za kienyeji kila mara ili kuepuka kudhulumiwa na washindani wake. Dawa hizi huwa kama kinga kutokana na mabaya anayopangiwa na washindani wake. Shughuli hii hufanywa kisiri ili wapinzani wasijue kuhusiana na matayarisho haya. Kujulikana kwa siri hii basi huchangia fahali kushindwa ama fahali watoshane kwa nguvu. Mlinzi wa fahali huwa mtu mmoja aliyeteuliwa na huvalia nguo teule zisizo na makali ya rangi na madoa doa. Inaaminika kuwa fahali waliotengwa kwa kusudi la kupigana hawapendi kuhusiana na watu walevi au mwanamke karibu. Madai haya ni ya kimila kwa maana ya kuwa mtu mlevi au mwanamke ni viumbe dhaifu. Kwa hivyo mlinzi anatahadharishwa asinywe pombe ili asije akajeruhiwa na fahali haswa katika awamu ya maandalizi ya mapigano (Travel, 2020).

Kwa mujibu wa Nyotuoro (2021), fahali wa kupigana hutengwa na ng'ombe wengine ili awe mkali zaidi na ajione kama mnyama shupavu kuliko yeyote yule. Pia inaaminika kuwa hafai kutangamana na ngombe wa kike kwa kuwa atawazoea na iwapo kutakuwa na mapambano atawaona fahali wengine kama ng'ombe wa kike na hivyo ni rahisi kupata majeraha na fahali anayeshindana naye. Aidha, maandalizi ya sherehe ya mapambano ya fahali huanzia kwa yule anayemiliki fahali ambapo hafai kushiriki mapenzi nje ya ndoa ama na bibiye, inaaminika kuwa fahali hupoteza nguvu na kushindwa katika mapambano. Ili kuepuka majaribio haya, mwenye fahali hukesha usiku kucha akizungumza na fahali wakiimba nyimbo za kumtia nguvu fahali wao.

Utafiti kuhusu historia ya upiganishaji wa fahali kutoka jamii ya Waidakho iliufaidi utafiti wa mtafiti kwa kutimiza malengo ya utafiti haswa kwa kurejelea miktadha ya uamilifu wa dhana zinazohusiana na fahali pamoja na maandalizi ya fahali kwa ajili ya mapambano kwa kuzingatia upekee wa ishara zinazojitokeza kama kipengele muhimu cha mawasaliano. Aidha, historia ya upiganishaji fahali ilimpa mtafiti mwelekeo wa kujua jinsi mapambano ya fahali yamebadilika na kuendelea kuakisi mahitaji ya wanajamii pamoja na kuathiri maisha ya kisasa ya Waidakho kwa kuangazia sifa za mwanamume katika jamii ya Waidakho.

### 2.3 Dhana ya Ubabedume

Kulingana na Edwards (2004), suala la ubabedume ni uwanja wa utafiti ulioimarika na umehusisha taaluma mbalimbali zinazohusika kwa mapana na ujenzi wa kijamii wa maana ya "kuwa mwanamume." Wasomi wa masuala ya kiume huchunguza dhima na maana za kijamii za wanaume. Idadi kubwa ya usomi unaohusu ukosefu wa usawa wa kijinsia huzingatia wanawake na njia ambazo kimuundo na utaratibu wamewekwa chini ya wanaume na wasio na uwezo. Kulingana na Matinde (2006), katika kuratibu majukumu ya kiuana na kutathmini thamani ya kila jinsia, ni sharti kuzingatia jinsi mitazamo na mielekeo ya jamii huchukuliwa na kupewa nafasi kuu katika uainishaji wa mwanamume au mwanamke hutokea wakati wa kuzaliwa na ni hatua ya kwanza katika mchakato wa kuongeza na kuendeleza utambulisho wa kijinsia katika jamii.

Asili huamua jinsia ya mtu binafsi wakati utamaduni huathiri mitazamo, tabia na mifumo ya tabia inayofaa kwa kila jinsia (Mutunga, 2009). Kihistoria, watu binafsi

wamejifunza kukabiliana na matarajio haya huku yakitengeneza maisha yao ya kibinafsi na kitaaluma. Hali hii inasababisha majukumu ya kijinsia ambayo yanadhihirisha uanaume na uke ingawa mitazamo na tabia zinazotarajiwa za wanaume na wanawake zinahusiana na mazingira anamoishi mtu. Mwanamume anahusishwa na mkusanyiko wa sifa zinazojengeka katika jamii zinazohusiana na wanaume. Sifa hizi hufafanuliwa kuwa za kiume kwa sababu ya mtazamo wa kijamii wa maana ya kuwa mwanamume. Kutokana na kauli hii mwanamume halisi ana sifa za kitabia za wanaume ambazo lazima wakubaliane na viwango vilivyoainishwa vya kitamaduni vya uanaume katika jamii yao.

Njia moja ya kuzingatia jinsia ya wanaume ni kupitia uchunguzi wa suala la ubabedume. Ubabedume una maana tofauti kuhusu kuwa mwanamume kwa kuangazia utamaduni kote ulimwenguni (Rita, 2014). Anaeleza kuwa wanaume ni viumbe vya kibiolojia ambapo kila mmoja wao ni tofauti na mwingine na hivyo jina mwanaume ni hadithi na mazungumzo kuwahusu kulingana na jinsi wanavyopaswa kuishi katika mazingira fulani. Utafiti kuhusu ubabedume basi, husaida kufafanua sifa za mwanamume katika kuelewa maadili tofauti kuhusu uanaume ambayo humfahamisha tabia za wanaume katika kutekeleza ukatili dhidi ya mwanamke.

Edell (2015) anaeleza kuwa ubabedume ni dhana inayorejelea mfumo dume ambapo wanaume huonekana bora na huwa na nguvu ikilinganishwa na mwanamke. Ingawa katika jamii hiyo mwanamume hutambuliwa kulingana na idadi ya wanawake anaomiliki, lakini kipimo halisi cha "ujanadume" wake hupimwa kulingana na mahusiano yake na wanaume wenzake. Ubabedume miongoni mwa wanaume ni zao la fikra akilini mwake kuhusu tafsiri za kiutamaduni na mazingira aliyolelewa yanayokuza ujanadume. Mwanamme hafai kuonyesha udhaifu alionao kwa jamii ila anafaa kuonyesha ujanadume wake hata katika ya kudunisha. Hivyo, mara nyingi hufundishwa tangu utotoni mwake kwa kuambiwa kuwa mwanamume hafai kuonyesha hisia za kulia bali anafaa astahimili hali anayokumbana nayo.

Kobia na Mung'ahu (2017) wanaeleza kuwa jamii nyingi za Kiafrika humtukuza mwanamume kupitia mila, desturi na itikadi zao. Matokeo ya utafiti wa wataalam hawa ni kuwa kuna taswira chanya na hasi kuhusu mwanamume ambazo mwanamume

hukuzwa nazo kitamaduni. Taswira chanya ni kuwa mwanamume amesawiriwa kama shujaa na jasiri, mwenye kumiliki nyenzo za uzalishaji mali, mkarimu na mwenye busara. Kwa upande wa hasi ni kuwa, mwanamume anatazamwa kuwa mchafu, mkware na kahaba asiye na huruma.

Katika hali ya mwanamume kutukuzwa, ni lazima awe na nafasi kuu katika shughuli zinazohusu maamuzi ya kijamii. Hali hii imesababisha mwanamume kujisahau na kufanyiana ubabe kwa wenyewe. Hata hivyo jamii nyingi zimetoa msimamo mkali kuhusiana na kutoa kashfa dhidi ya mwanamume mwenziwe kama njia moja ya kuonyesha udume wake (Mohammed, 2018). Haya yamedhihirika kutokana na hali ambapo mwanamume anaweza kujihusisha katika ugomvi na mwanamume mwenzake ambapo matokeo yake huwa ni kupigana kati yao hata pasipo na sababu za kimsingi ili kuonyesha umahiri wake. Aidha, kunao wanaue ambao hukusudia kuwanyanganya wanaume wenzao wake zao kama njia moja ya kujitambulisha kuwa mwenye nguvu na uwezo. Kwa vile mambo yaliyoelezwa hujitokeza katika jamii, kazi ya fasihi humulika jamii na kueleza yanayotendeka. Mwanamume kuwa na nguvu na uwezo dhidi ya mwanamume mwenzake au mwanamke umejitokeza mpaka kwenye nyimbo.

Kwa mujibu wa Kimmel (2014), wasomi wa ubabedume hujadili wanaume na uanaume kama ilivyojengwa kijamii. Badala ya kuzingatia ulimwengu wa kibiolojia, wanasayansi wa kijamii na tabia huchunguza maana tofauti ambazo uanaume na uke husawiri katika mazingira tofauti. Wakati "uume" wa kibiolojia hutofautiana kidogo sana, majukumu, tabia, miili, na utambulisho ambao unafikiriwa kama "kiume" hutofautiana sana. Tofauti hii inaruhusu wasomi kusema kwamba uanaume umejengwa kijamii. Wasomi wa uanaume hutokana na taaluma mbalimbali, na asili hizi mbalimbali zinaonyesha viwango vingi vya tofauti katika uanaume. Kwanza, uanaume hutofautiana kihistoria-kile kinachofikiriwa kama mabadiliko ya kiume kwa muda. Pili, uanaume hutofautiana kiutamaduni. Tatu, uanaume hutofautiana ndani ya kisaikolojia-maana ya kuwa mwanadamu hubadilika katika kipindi cha maisha ya mtu.

### 2.4 Tafiti za Awali kuhusu Ubabedume

Baadhi ya tafiti zimedhihirisha ubora wa mila na desturi za jamii katika juhudi zao za kujenga na kuimarisha ubabedume. Tafiti hizi zimeshughulikiwa katika jamii nyingi

nchini Kenya kwa malengo tofauti na utafiti huu. Mwamzandi (2001) alichunguza uana katika nyimbo za taarab ambapo aligundua kuwa nyimbo za taarab zilimsawiri mwanamume kama mtu wa kutegemewa katika familia. Mwanamume aliyeshindwa kukidhia mahitaji ya familia yake alibezwa. Utafiti wa Mwamzandi (keshatajwa) ulimfaa mtafiti katika kuchunguza ubabedume katika nyimbo za upiganishaji wa fahali katika jamii ya Waidakho kwa kumsawiri mwanamume katika nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za kupiganisha fahali kama mwenye kuwajibika katika kuikimu familia yake. Kazi ya Mwamzandi (keshatajwa) inatofautiana na utafiti huu kwa kuwa mtafiti aliangazia sifa za mwanamume na maudhui ya ubabedume kupitia kwa nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za upiganishaji fahali.

Waita (2004) alitafitia suala la kijinsia kwa kuchunguza fasihi simulizi ya Wakikuyu huku akilenga mabadiliko na mikakati ya kuendeleza usawa wa kijinsia. Alichunguza ngano, methali, nyimbo na mashairi simulizi. Utafiti wa Waita (keshatajwa) uligundua kuwa, wanaume walidhulumiwa kwa kiasi kikubwa na wanawake. Dhuluma hii iliwapelekea wanaume kupanga njama ya kuwatia wanawake mimba ili wapate nafasi ya kuwatawala wakiwa katika ulegevu wa ujauzito. Utafiti wake unatofautiana na huu kwa kuwa mtafiti alijikita katika nyimbo za Waidakho na pia jamii hizi zina tamaduni tofauti.

Kabaji (2005) alichunguza ngano miongoni mwa jamii ya Wamaragoli ambapo alieleza kuwa wanaume wamesawiriwa kuwa wenye tabia njema, wenye nguvu na ujasiri. Kufanyika kwa miviga kama vile ya tohara hulenga kuwafanya wanaume kuwa wanaowajibika. Kazi yake ilimfaa mtafiti katika kuchunguza ubabedume unaohusiana na tamaduni za Waidakho na maumbile yao ya wanaume kama ilivyo katika nyimbo za Waidakho. Licha ya kuwa na usawa kimalengo, kazi ya mtafiti ilitofautiana na yake kwa kuwa mtafiti alijikita katika kipera cha nyimbo na ishara kwa ujumla haswa za upiganishaji fahali kinyume na Kabaji (keshatajwa) ambaye ameangazia kipera cha ngano.

Utafiti uliofanywa na Uchendu (2007) ulilenga kuwa, ubabedume miongoni mwa vijana wa kiume ulihusishwa na sifa za kimwili, sifa za kibaolojia, na kisaikolojia, pamoja na vipengele vya utu kama kutoogopa, uamuzi, na uwezo wa kulinda

wanyonge, kuwa na kanuni, kudhibiti, kushinda, kuchukua hatari, kutoa uongozi, kuwa na msimamo, kufurahia hali ya juu ya kijamii, na kuonyesha ustadi katika sanaa ya kijeshi. Uchendu (keshatajwa) anasema kuwa ubabedume ulichangia kuelewa kwa watoto wa kiume na wanaume kuhusu namna wanavyostahili kutenda ili kukubalika kama wanaume katika jamii. Kazi hii ilifaa utafiti huu katika kuchanganua taswira za mwanamume zinazohusu namna mwanaume anavyofaa kutenda ili aonekane bora zaidi katika nyimbo za upiganishaji fahali za Waidakho. Kulingana na nyimbo za Waidakho katika sherehe za upiganishaji fahali, ili mwanamume awe na sifa za kiume aliyekamilika alifaa awe shujaa asiye onyesha hisia na ambaye yuko tayari kuhatarisha maisha yake katika kulinda jamii yake.

Onyango (2007) alichunguza ubabedume katika fasihi ya watoto kwa kurejelea vitabu teule. Alichanganua vitabu vitatu vya watoto vya Ken Walibora: *Mtu wa Mvua*, *Ndoto ya Amerika* na *Mgomba Changaraweni*. Utafiti wake uligundua kuwa fasihi ya watoto hufafanua majukumu ya watoto yanayohusiana na jinsia. Utafiti wake unatofautiana na utafiti huu kwa kuwa ameegemea katika fasihi andishi. Onyango (keshatajwa) aliangazia ubabedume miongoni mwa watoto kwa kuchunguza majukumu yao kijinsia kinyume na kazi ya mtafiti ambayo ilimulika fasihi simulizi ya Waidakho kwa kuangazia sifa za mwanamume na jinsi anavyomtazama mwanamke. Utafiti huu ulikuwa na manufaa licha ya tofauti zilizopo kwa kumsaidia mtafiti kumchora mwanamume kisifa na kimajukumu. Hii ni kwa kuwa tafiti zote zinagusia suala la ubabedume.

Kobia (2008) alitafiti kuhusu taswira za kiuana katika nyimbo za tohara za wanaume miongoni mwa Waigembe. Matokeo ya utafiti wake ni kuwa kuna taswira chanya na hasi kuhusu mwanamume. Taswira chanya ni kuwa mwanamume amesawiriwa kama shujaa na jasiri, mwenye kumiliki nyenzo za uzalishaji mali, mkarimu na mwenye busara. Aidha, taswira hasi ni kuwa, mwanamume amesawiriwa kuwa mchafu, mkware na kahaba asiye na huruma. Utafiti wake unalingana na utafiti huu kwa kiasi fulani kwa kuwa tafiti zote zinachunguza wahusika wanaume. Mtafiti alijikita katika jamii ya Waidakho kwa kuangazia taswira za mwanamume katika nyimbo zinazoimbwa katika sherehe ya upiganishaji wa fahali. Utafiti wake ulimfaa mtafiti kuchunguza sifa za

mwanamume na maudhui ya uabebedume katika jamii ya Waidakho kupitia nyimbo wanazoimba katika mapigano ya fahali.

Kibigo (2019), alichunguza ubabedume katika majigambo ya miviga ya *Shilembe* na *Mchezasili wa mayo* miongoni mwa Waisukha ambapo alijikita katika kuchunguza jinsi vipashio vya lugha haswa; vishazi, vitenzi na nomino husawiri ubabedume. Utafiti huu ulitofautiana na utafiti wa mtafiti kwa kuwa ulihakiki jinsi ubabedume unavyojitokeza katika nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za upiganishaji wa fahali katika jamii ya Waidakho na ishara maana zinazojitokeza katika sherehe za mapambano ya fahali.

Bayyo (2020) alitafiti kuhusu usawiri wa jinsia ya kiume katika riwaya teule za Shafi Adam Shafi ambapo aliangazia mbinu zilizotumiwa na mwanamume katika kukabiliana na changamoto anazokumbana nazo. Utafiti huu ulitoa mchango mpya wa kumpa mwanamume nafasi ya kutazamwa sawia na mwanamke. Katika utafiti huu mtafiti alilenga kuchunguza jinsi mwanamume alivyotukuzwa na kumkandamiza mwanamke kinyume na utafiti wa Bavyo (keshatajwa) ambao ulihakiki nafasi ya mwanamume katika kujikomboa kutokana na changamoto anazokumbana nazo.

## 2.5 Dhana ya Nyimbo

Nyimbo ni tungo za maneno yaliyopangwa kwa utaratibu na yanayotamkwa kwa sauti ya kuvutia na kwa mahadhi ya kupendeza (Wamitila, 2003). Aidha, Magambo (keshatajwa) anafasili nyimbo kuwa aina ya shairi zinazoimbwa pekee au kuhusishwa na ngoma. Inabainika wazi kuwa nyimbo zimekuwa zikitumika katika maisha ya binadamu hata kabla ya maandishi kuvumbuliwa na imekuwa ni mojawapo ya njia za watu kuelezea hisia zao na kujitumbuiza katika sekta mbalimbali za maisha yao katika jamii.

Nyimbo vilevile hutumiwa kupitisha ujumbe kwa watu wenye umri tofauti katika jamii kwa kuwatambulisha na jamii yao na kuwakumbusha jinsi wanavyofaa kutenda kulingana na matakwa ya jamii. Nyimbo ni aina ya tanzu za fasihi simulizi. Fasihi simulizi ni sanaa ambayo hutumia lugha hasa maneno ambayo yametamkwa kupitia kinywa cha binadamu. Nyimbo ni mali za jamii. Rekodi za matukio muhimu katika jamii huhifadhiwa kwa nyimbo na kupokezwa kwa vizazi vijavyo. Nyimbo hutumiwa

kupitisha amali na mambo ambayo jamii inayothamini. Amali hizo hurekodiwa katika nyimbo mbalimbali kama vile za kazi na kurithishwa vizazi vya jamii hiyo. Mawaidha na thamani za jamii hukaririwa katika nyimbo (Wanjala, 2013).

Magambo (2019) anaeleza kuwa nyimbo hutokana na mazingira. Mazingira ndiyo yanayozalisha hisia na hatimaye kwa msanii. Hivyo basi, katika nyimbo panapaswa kuwa na wazo maalum ambalo linawasilishwa kwa hadhira husika kwa njia ya sauti. Nyimbo ni utanzu wa kishairi zinazoimbwa kwa muwala fulani. Umaarufu wa muziki katika wimbo huruhusu maana ya maneno kuchukuliwa sawa na uimbaji wa muziki.

Nyimbo ni zao la shughuli za binadamu na hisia zake na hivyo huzingatia muktadha mbalimbali. Nyimbo zimefunganishwa na muktadha fulani pale ambapo pana hadhira na matini (Waswa, 2022). Hadhira huwa ni wale wanaosikiliza au kutazama nyimbo nayo matini yakiwa ni yale matamshi yenyewe kwa njia ya uimbaji. Fasihi simulizi ni sanaa inayotumia lugha, hasa maneno ambayo yametamkwa kupitia kinywa cha binadamu. Nyimbo ni mali za jamii mbalimbali zenye manufaa mengi kwa binadamu na kupitia uwezo wake wa kutamka maneno huwasilisha ujumbe kwa njia ya mazungumzo, kughani na kuimba.

Nyimbo zinaweza kuainishwa katika makundi tofauti kwa kuzingatia vigezo mbalimbali. Kuna nyimbo za watoto, za kazi au hodiya, za mapenzi, za dini, za sifa, za mbolezi na za jando au nyiso. Utafiti huu unashughulikia nyimbo za sifa zinazoimbwa katika sherehe za upiganishaji fahali katika jamii ya Waidakho (Chepkwony, 2020)

Wanjala (2013) anasema kuwa, nyimbo hunuia kuwaelekeza watu katika jamii kwa kuwaelimisha kuhusu itikadi na desturi za jamii ya Waidakho au kuwatia moyo dhidi ya changamoto wanazokumbana nazo katika shughuli zao za kawaida katika juhudi za kuboresha maisha yao. Nyimbo hizi vilevile huimbwa katika muktadha tofauti kama vile matanga haswa yanayohusu ushujaa. Huimbwa kwa kuambatanishwa na mdundo wa ngoma *isukuti*. Sifa za nyimbo za upiganishaji fahali ni kama vile: Huimbwa na watu walio na imani fulani kuhusu jamii ya Waidakho wao na huimbwa katika kumbi za kupiganisha fahali na mahali wanaume wamejumuika. Aghalabu huandamana na ala

mbalimbali za muziki kama vile Klabu na ngoma ya *isukuti*. Nyimbo hizi hutaja sifa za wanaume Waidakho, matendo yao na uhusiano wao na watu katika jamii.

### 2.6 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili; nadharia ya Uwezo- uume ya Connell miaka ya 1995 na nadharia ya Semiotiki ya Ferdinand de Saussure miaka ya 1970. Nadharia ya uwezo- uume ilikuwa na manufaa katika kueleza uhusiano kati ya wanawake na wanaume katika jamii na nadharia ya Semiotiki ilikuwa na manufaa katika kuchunguza maana, ishara-maana na misingi ya kitamaduni ya jamii ya Waidakho.

#### 2.6.1 Nadharia ya Ubabedume

Nadharia ya Ubabedume iliasisiwa na Connell mwaka ya 1995. Kulingana na Connell (keshatajwa) dhana ya uana inatokana na fasili na fasiri ya masuala yanayohusiana na uwezo wa kijinsia. Kwa hivyo dhana ya kumkuza mwanamume na kumdunisha mwanamke inaweza kueleweka kama matokeo ya ufasiri na ufasili wa kimwili kwa watu na kwa utamaduni kijamii. Kwa mujibu wa Connell (keshatajwa), katika nadharia ya ubabedume, mwanamume hupewa hadhi kuliko mwanamke katika jamii za Kimagharibi. Katika nadharia hii, wanaume wanachukuliwa kuwa na uwezo, nguvu na ukakamavu. Aidha, katika hadhi ya juu huwa kuna wanaume, na katika hadhi ya chini huwa kuna wanawake. Vilevile, kwa mujibu wa Connell (keshatajwa), ubabedume si sawa na nguvu za kimwili bali ni matendo yao ya kijamii. Hivyo anapendekeza kuwa ubabedume hutazamwa kwa njia zaidi ya moja kama vile mahusiano ya kijinsia, ukatili, malezi na kazi.

Nadharia hii huchota mawazo kutoka kwa nadharia ya tamaduni ya ubabedume iliyoasisiwa na mwananadharia anayejulikana kama Antonio Gramsci akiwa gerezani kati ya mwaka wa 1923 na 1936 ilihusu mahusiano miongoni mwa matabaka ya kijamii. Nadharia hii hubainisha na kuelezea namna mwanamume anamiliki nguvu na mamlaka dhidi ya mwanamke au mwanamume mwenza, hasa kutokana na matakwa na mielekeo ya jamii husika. Kulingana na Walsh (1997), ubabe huhusishwa na uwezo wa mwanamume kuwa na uwezo wa kukimu na kutosheleza mahitaji ya familia. Nadharia hii imejengeka kutokana na misingi kwamba utamaduni ni dhana muhimu na ni uti wa mgongo katika ujenzi na matumizi yake kutegemea jamii husika kwa vile, kila jamii

ina utamaduni wake. Nadharia hii ina mihimili minne mikuu. Ili kufanikisha malengo ya utafiti mtafiti atatumia mihimili miwili kama ifuatavyo:

i. Itikadi za kijamii huongoza mielekeo, fikra na mitazamo ya wanajamii ambazo hufafanua majukumu sahihi ambayo mwanamume anastahili kutimiza. Mhimili huu ulikuwa na manufaa katika utafiti kwa kuwa ulimsaidia mtafiti kubainisha majukumu wanayopewa watoto wa kiume katika jamii ya Waidakho kama inavyojitokeza katika sherehe za upiganishaji fahali. Aidha, ilimsaidia mtafiti kujua namna jamii ya Waidakho humtukuza mwanamume na kuonekana kama tegemeo la jamii kimajukumu kupitia kwa nyimbo zinazoimbwa. Mhimili huu ulikuwa na manufaa katika utafiti huu katika kuchunguza namna ubabedume hukuzwa na kupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia sherehe za upiganishaji fahali ambapo nyimbo hutumiwa kama nyenzo ya kuwakumbusha wanaume na watoto wa kiume kuhusu misimamo na mitazamo ya jamii ya Waidakho.

ii. Utamaduni hudhibiti maisha ya jamii pamoja na mielekeo na mitazamo yao. Utamaduni wa jamii hujikita katika desturi, lugha na imani ambazo hutamalaki katika mfumo mzima wa jamii katika kujitambulisha. Mhimili huu ulimfaa mtafiti katika kujua jinsi jamii ya Waidakho huweza kuwajenga watoto wa kiume kupitia kushughulikia sifa za mwanamume kama zinavyojitokeza katika nyimbo za upiganishaji fahali na pia jinsi mwanaume anavyomtazama mwanamke kulingana na tabia na mienendo yake katika jamii ya Waidakho. Nadharia ya Ubabedume inasisitiza umuhimu wa kuchunguza utamaduni wa maisha ya jamii kwa ujumla ili kufahamu jinsi mwanamume anavyojengwa, kuendelezwa na kudumishwa. Nadharia hii inashikilia kwamba ni vigumu kuchunguza jamii yoyote ile kabla ya kufahamu na kuelewa mila na desturi za jamii husika.


Mihimili ya nadharia iliyotajwa na mtafiti ilikuwa na manufaa kwa kuwa iliuongoza utafiti huu katika kuchanganua data ili kuibua sifa na maudhui yanayojitokeza katika sherehe za upiganishaji fahali katika jamii ya Waidakho. Nadharia ya ubabedume inamwelekeza mwanamume katika kutambua sifa zake na mahusiano yake na wanaume wenzake na katika kutekeleza majukumu yake katika kuboresha mfumo dume. Nadharia hii iliufaidi utafiti huu katika kutambua umuhimu wa kuchunguza

masuala ya kihistoria na mila za kijamii ili kujenga, kuchipua, kudumisha na kuendeleza sifa za ubabedume katika nyimbo za Waidakho wanapopiganisha fahali. Nadharia hii ilinuia kueleza nafasi ya wanaume katika jamii na jinsi wanavyomiliki uwezo dhidi ya wanawake.

### 2.6.2 Nadharia ya Semiotiki

Nadharia ya semiotiki iliasisiwa na Ferdinand de Saussure miaka ya 1970. "Semiotiki" ni neno la Kiyunani lenye maana ya ishara. Semiotiki ni nadharia inayoshughulika na ishara pamoja na uashiriaji katika kazi za kifasihi. Nadharia hii hueleza kuwa, ishara zinazojitokeza hufafanuliwa kutegemea muktadha wa jamii. Alama hizi huundwa na binadamu ili azitumie katika kurahisisha mawasiliano yake na binadamu wenzake Mwasisi huyu anafafanua semiotiki kama kanuni za ishara ambazo hutumiwa na binadamu katika kuwakilisha kitu au hali fulani na hutumika kurejelea vitendo au dhana maalumu na maana ya ishara hiyo itatokana na sheria fulani za tamaduni.

Nadharia hii ilinuia kuchunguza uhusiano uliopo baina ya X =Y. X ni kitu kilichopo kinachoweza kuwa neno, fahali, ngoma inayochezwa katika sherehe za Waluhya ama chochote kinachobuniwa na binadamu. Y ni maana inayotokana na kitu hicho. Kuchunguza dhana zinazohusiana na ubabedume katika nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za upiganishaji fahali zitachukuliwa kama umbo X lenye maana Y. Kulingana na Ellis na McClintock (1990), wafuasi wa nadharia ya semiotiki hujikita zaidi kwenye fasili ya ujumbe kuliko vile mchakato wa uwasilishaji wa ujumbe huu hufanyika. Mtafiti alijikita zaidi kuchunguza jinsi ujumbe ulioko kwenye sharehe za mapambano ya fahali pamoja na dhana mbalimbali zilivyofasiriwa na kuibua suala la ubabedume. Nyimbo za mapambano ya fahali zilitumika kama maneno yaliyofinyangwa kuzua mawasiliano yenye ishara zinazobeba ujumbe kwa mwanajamii. Pierce (keshatajwa) anaihusisha Nadharia ya Semiotiki na kielelezo cha pembe tatu: Kiashiria (kitu), ishara (maneno), na kiashiriwa.




Umbo hili linaloonyesha uhusiano uliopo baina ya ishara, kitu/jambo linalowasilishwa na mfasiri anayeipa ishara maana. Mfasiri anaweza kuwa aliyesimba ujumbe au atakayesimbua ujumbe huo.

Barthes (1994) anaibua misimbo mitano ya semiotiki inayotumika katika kuchambua kazi za kifasihi; kiurejelezi, ki-ishara, kihementiki, kimatukio na kiseme. Kujumlisha misimbo hii katika kubaini maana katika kazi za kifasihi hutegemea mada, utanzu na nia ya mtafiti. Ili kufanikisha lengo la tatu, mtafiti atatumia misimbo minne ambayo ni: msimbo wa kiurejelezi, kihementiki, ki-ishara na wa kiseme.

i. Msimbo wa kihementiki ulimsaidia mtafiti katika kuibua anwani za nyimbo zinazotumika katika mapigano ya fahali pamoja na kuibua maana katika anwani 'upiganishaji fahali'. Katika kuibua maana za anwani katika nyimbo hizo ilikuwa rahisi kutofautisha nyimbo zinazomsawiri mwanaume.

ii. Mtafiti alitumia msimbo wa kiseme. Wamitila (2002) anarejelea neno 'sema' kama elementi nasibishi ya kisemantiki. Kumaanisha kuwa, sifa mbalimbali za mhusika fulani zinaweza elezwa kwa kutumia viashiria mbalimbali. Msimbo huu ulikuwa na manufaa kwa mtafiti kwa kuwa alikuwa makini kusikiliza nyimbo ili kupata viashiria vinavyomrejelea mwanaume ili kuibua sifa zake pamoja na jinsi alivyomchukulia mwanamke kwa misingi ya kujiona mwenye nguvu dhidi ya mwanamke.

iii. Mtafiti alitumia msimbo wa ki-ishara kubaini maana mbalimbali baada ya kufumbua ishara katika kutazama baadhi ya vifaa na dhana mbalimbali zilizotumiwa katika sherehe ya upiganishaji fahali. Msimbo huu ulimfaa mtafiti kwa kuhusisha jinsi vifaa na dhana katika nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za mapambano ya fahali zinawakilisha maana baada ya kufumbua ishara husika katika vifaa na dhana hizo kwa misingi ya ubabedume.

iv. Mtafiti alitumia msimbo wa kiurejelezi katika kuvibainisha viashiria vya utamaduni wa jamii ya Waidakho. Urejelezi katika upiganishaji fahali ulidhihirisha uhalisia mahususi kutokana na matumizi ya dhana au vitu vilivyotumika kwa lengo la kuwasilisha ujumbe fulani unaoeleweka kwa wanajamii wa Idakho.

Misimbo yote minne ilitumika katika uchanganuzi wa nyimbo teule ili kutimiza malengo ya utafiti. Nadharia hii ilimsaidia kufafanua miktadha ya uamilifu wa nyimbo za mapambano ya fahali pamoja na dhana zilizohusiana na sherehe ya mapambano ya fahali kama vile ngoma za *isukuti,* silaha zilizobebwa na fahali kwa kuzingatia upekee wa ishara uliojitokeza kama kipengele maalum cha mawasiliano kwa kuangazia msimbo wa kihementiki, msimbo wa kiseme, msimbo wa Ki-ishara na msimbo wa kiurejelezi.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika jamii ya Waidakho inayopatikana katika kaunti ya Kakamega nchini Kenya. Jamii hii inapakana na Isukha, Maragoli na Kisa. Jamii hii hujivunia kuwepo kwa kilimo, uzalishaji wa mahindi, miwa na kuchimba migodi. Waidakho hujivunia utamaduni wa upiganishaji fahali ambao hufanyika kila Jumamosi na siku kuu ya Krisimasi. Katika upiganishaji fahali, nyimbo zinazohusu jamii ya Waidakho huimbwa ili kuwatumbuiza mashabiki na kumfanya fahali awe na ari ya kushindana (Kabaji, 2005). Utafiti ulifanywa katika eneo la Ikolomani; Idakho Kusini kwa sababu eneo hili ndilo maarufu katika upiganishaji fahali.

## 3.2 Uteuzi wa Sampuli

Usampulishaji katika utafiti huu uliteua nyimbo na ishara ambazo mtafiti alitumia kupata data katika utafiti. Kulingana na Kothari (2004) sampuli ni sehemu ndogo iliyochaguliwa kutoka kwenye jumuia ambayo imeteuliwa kutoka kwenye kundi kubwa ili itumiwe katika utafiti. Kulingana na Onyango (2001) ukubwa wa sampuli unaolingana na ukubwa ukubalikao katika utafiti wa kimaelezo huwa ni wa asilimia 10 - 30 ya watu wote wa eneo la utafiti. Hata hivyo miviga ya upiganishaji fahali ina nyimbo nyingi ambazo huwa na dhima mbalimbali kutegemea muktadha wa matumizi. Kwa misingi ya wataalamu hawa (washatajwa) mtafiti alitumia mbinu ya uteuzi maksudi wa kinasibu kuteua sampuli ya nyimbo kumi kutoka kwa mkusanyiko wa nyimbo mia moja ambazo zilikusanywa kutoka kwa waimbaji saba ambao waliimba zaidi ya nyimbo kumi zinazoimbwa katika miviga ya upiganishaji fahali waimbaji hawa waliteuliwa kimaksudi nasibu katika jamii zilizokuwa maarufu katika miviga ya upiganishaji fahali.Aidha, mtafiti pia alitumia mbinu ya uteuzi maksudi wa kinasibu kuteua sampuli ya ishara saba kutoka kwa jumuiya ya vifaa na dhana ambazo zilikusanywa kutoka kwa washiriki saba wa miviga ya upiganishaji fahali ambao walitaja majina ya vifaa na dhana zinazotumika katika miviga ya upiganishaji fahali. Kiwango hiki cha sampuli kilizingatia mapendekezo ya Onyango (keshatajwa) kwamba asilimia kumi (10%) ya nyimbo lengwa inaweza kuteuliwa kuwa sampuli ya utafiti.

Aidha, uteuzi wa kimapokezano ulimfaa mtafiti kuteua nasaba za Idakho, fanani na mwenyekiti wa sherehe za upiganishaji fahali. Nasaba za Idakho ziliteuliwa kutokana na umaarufu wa upiganishaji fahali katika sehemu hizo. Aidha maeneo haya ya Idakho hutoa mazingira bora ya mashinani ambako mashindano hufanyika bila kuathiri shughuli zingine rasmi za Kaunti ya Kakamega. Nao waimbaji na wenyekiti wa kuandaa sherehe za upiganishaji waliteuliwa kimakusudi kutoka kila jamii nane zilizo maarufu katika kupiganisha fahali ili kutoa data kamili ya utafiti kwa sababu wao huwa na orodha kamili katika kalenda inayoonyesha jinsi fahali watakavyopigana. Mwenyekiti aliufaa utafiti huu kwa kuhusika katika kumwimbia mtafiti baaadhi ya nyimbo zilizofanikisha utafiti huu. Pia kutokana na tajriba yake katika kuendesha sherehe za upiganishaji fahali alimfaa mtafiti katika kutambua baadhi ya ishara au dhana mbalimbali ambazo kulingana na utamaduni wa Waidakho hudhihirisha ubabedume. Jumla ya nyimbo kumi na ishara saba zilitumiwa katika utafiti huu kama kiwakilishi cha nasaba ishirini za Waidakho ili kuweza kupata data ya uhakika na ya kuaminika.

### 3.3 Vifaa vya Utafiti

Mtafiti alitumia hojaji, usaili, utazamaji na uchunzaji- shiriki. Utazamaji na uchunzaji –shiriki ulishirikisha kushuhudia, kushiriki, kuchunguza, kutazama, kusaili na kuhoji alipokuwa akikukusanya data. Mtafiti alitumia hojaji kwa kuwapa waliohojiwa nakala ambapo walinakili majibu ambayo yalikuwa ya maana katika kujibu maswali ya utafiti. Aidha, katika kusaili na uchunzaji shiriki, kinasasauti katika kurekodi nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za upiganishaji ambazo zilimsawiri mwanamume. Rekodi hii ilimsaidia mtafiti kutafsiri katika lugha ya Kiswahili kwa kuwa zilikuwa katika lahaja ya ki-idakho kama kumbukumbu wakati wa kuchanganua data na wakati wa kuandaa tasnifu.

### 3.4 Ukusanyaji wa Data

Ili kuweza kuchunguza ubabedume katika nyimbo za upiganishaji fahali katika jamii ya Waidakho, utafiti huu ulifanywa nyanjani kwa kuangazia sehemu ambazo ni maarufu katika kupiganishaji fahali. Sehemu hizo ni; Malinya, Kaluni, Lusiola, Musali, Musoli, Eregi, Shieywe na Luvambo. Mtafiti alitumia mbinu ya utazamaji na uchunzaji – shiriki.

Mtafiti alilenga nyimbo 10 kutoka kwa asilimia kumi (10%) ya mkusanyiko wa nyimbo mia moja ambazo zilikusanywa kutoka kwa waimbaji saba ambao waliimba zaidi ya nyimbo kumi zinazoimbwa katika sherehe za upiganishaji fahali na ishara 7 ambazo ziliteuliwa kimaksudi kutokana kutoka kwa asilimia kumi (10%) ya jumuiya ya vifaa na dhana ambazo zilikusanywa kutoka kwa washiriki saba wa sherehe za upiganishaji fahali ambao walitaja majina ya vifaa na dhana zinazotumika katika sherehe za upiganishaji fahali. Mbinu ya uchunzaji-shiriki iliufaa utafiti huu kwa vile ilijumuisha kutazama na kushiriki.

Katika kufanikisha mbinu hii, mtafiti alitumia mpangilio au ratiba ya utazamaji na uchunzaji-shiriki aliyopewa na mwenyekiti wa kuandaa mapambano ya fahali kama kifaa muhimu katika ukusanyaji wa data ambacho alikabidhiwa na mwenyekiti wa maandalizi ya mapambano ya fahali. Mtafiti alitumia mbinu ya uchunzaji-Shiriki katika kushuhudia, kushiriki, kuchunguza, kutazama, kusaili na kuhoji alipokuwa akikukusanya data. Mtafiti alishiriki sherehe za upiganishaji fahali katika sehemu mbalimbali kama vile, Malinya, Lusiola, Musoli, Musali, Eregi, Shieywe, Luvambo na Kaluni.

Kisha mtafiti alizinasa nyimbo na kupiga picha vifaa vilivyotumika kumsawiri mwanaume kwa kutumia kinasa sauti na kamera. Mtafiti alitumia mbinu ya uchunzaji shirikishi kwa kuwa ndiyo mbinu mwafaka katika kukusanya data ambayo haijaathiriwa na mitazamo ya watafitiwa nyanjani. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kuepuka changamoto kama vile kukumbana na wasailiwa ambao wanatoa habari na ujumbe usiohusiana na mada ya utafiti au wanakataa kutoa taarifa muhimu kwani mtafiti alijionea yeye mwenyewe.

### 3.5 Uchanganuzi wa Data

Mtafiti alizingatia tu nyimbo na ishara zile alikuwa ameteua kutokana na jumla ya nyimbo 20 na ishara 15 kwa kutumia asilimia 10 ya jumla ya sampuli kimaksudi akiongozwa na malengo ya utafiti. Mtafiti alitafsiri data aliyokusanya kwa umakini huku akipigilia mistari maneno au vifungu vya maneno na sentensi zinazoonyesha sifa za mwanamume na maudhui ya ubabedume. Aidha, mtafiti alichambua ishara alizokuwa amekusanya kwa makini kwa kutafutia maana ya hizo ishara kutegemea

matumizi yake katika sherehe ya upiganishaji fahali na kuelewa kwake kutegemea utamaduni wa Waidakho.

Mtafiti aliongozwa na malengo ya utafiti ambayo ni kuchunguza sifa za mwanamume, kujadili maudhui ya ubabedume na kuchunguza ishara-maana za kijinsia kama zilivyojitokeza katika nyimbo alizoteua. Uchanganuzi wa data uliongozwa na misingi ya nadharia ya ubabedume katika kutambua sifa za mwanamume na maudhui ya ubabedume katika nyimbo na nadharia ya semiotiki katika kutambua maana, ishara-maana na misingi ya utamaduni. Data iliwasilishwa kwa kutumia uchanganuzi elezi. Kwa sababu utafiti ulikuwa wa kimaelezo, data ilichanganuliwa kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo: kupanga, kuweka katika kanda za kunasa sauti, kisha kuihakiki na kuchanganua kwa kutazama idadi ya marudio kwa kila jibu.

### 3.6 Utafiti wa Awali

Mtafiti alifanya utafiti wa awali katika maeneo ya Bushirika na Madivini na jimbo dogo kwa kuwa maeneo haya yana data sawia na maeneo lengwa ya upiganishaji fahali. Lengo la utafiti huu wa awali lilikuwa kukadiria ubora na utegemewaji wa vifaa vya utafiti na kumwezesha mtafiti kuwa na uzoefu wa vifaa hivyo. Aidha utafiti wa awali ulimtayarisha mtafiti kukabiliana na changamoto zilizoweza kutokea katika kumbi za upiganishaji fahali. Aidha, mtafiti alikuwa na uhakika zaidi wa vyombo alivyovitumia kukusanya data.

### 3.7 Maadili ya Utafiti

Kulingana na Bell na Bryman (2007), maadili ni uelekevu wa tabia ambazo zinahusu haki za watafitiwa wote mtafiti atashirikiana nao katika harakati za kufanya utafiti wake. Aidha, ni uelekevu unaohusiana na lengo la utafiti pamoja na namna ya kutumia matokeo ya utafiti kwa njia ya uadilifu ili yaweze kuwa na manufaa kwa jamii. Mtafiti alilipa suala hili kipaumbele katika utafiti wake ili atimize malengo ya utafiti wake. Utafiti ulidumisha viwango vya juu vya uadilifu ili kuhakikisha faragha, usiri wa maelezo ya mhojiwa na kutowalazimisha kujibu mahojiano au hojaji. Aidha, mtafiti alitambua kazi za wasomi wengine ambazo alitumia katika kazi yake. Mtafiti alichanganua data aliyokusanya nyanjani wala si nyingine ili kudumisha ukweli na uaminifu. Mtafiti alipata kibali kutoka katika Tume ya Maadili ya Chuo kikuu cha

Chuka, alitafuta kibali cha kufanya utafiti kutoka katika Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi cha kufanya utafiti (NACOSTI). Mtafiti aliepuka kashfa za kielimu pamoja na udanganyifu, upotoshaji wa data na wizi wa kazi za wengine. Mtafiti alichanganua data ile alikuwa amepata nyanjani na wala si nyingine ili kujibu maswali ya utafiti.

# SURA YA NNE

# SIFA ZA MWANAMUME KAMA ZINAVYOJITOKEZA KATIKA MIVIGA YA UPIGANISHAJI WA FAHALI KATIKA JAMII YA WAIDAKHO

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii, kuna uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo yaliyokusanywa uwanjani kwa kutumia uchunzaji-shiriki na utazamaji, kinasasauti, kamera za picha. Data imechanganuliwa kwa mtindo wa kimaelezo kwa kutumia maelezo ya kifafanuzi na mifano. Aidha, data hii imejikita katika kuchunguza sifa za mwanaume zinazojitokeza katika nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za upiganishaji fahali katika jamii ya Waidakho husawiri ubabedume.

## 4.2 Ubabedume katika Sherehe za upiganishaji fahali

Kutokana na nadharia ya uwezo- uume mtafiti aliyoitumia katika kufanikisha malengo yake, sifa wanazoonyesha zina ukweli kwamba hakuna mwanaume wa kawaida katika jamii nyingi za kiafrika. Hii ni kwa sababu jamii nyingi nchini Kenya huwa na mwelekeo na mtazamo tofauti kumhusu mwanaume kutokana na njia mbalimbali kama vile majukumu, vita na kulinda mifugo kama ilivyo katika jamii ya Waidakho ambapo fahali huwa na dhamana kubwa haswa kwenye mazingira alimo mwanaume.

Asili huamua jinsia ya mtu binafsi wakati utamaduni huathiri mitazamo, tabia na mifumo ya tabia inayofaa kwa kila jinsia (Mutunga, 2009). Kihistoria, watu binafsi wamejifunza kukabiliana na matarajio haya huku yakitengeneza maisha yao ya kibinafsi na kitaaluma. Hali hii inasababisha majukumu ya kijinsia ambayo yanadhihirisha uanaume na uke ingawa mitazamo na tabia zinazotarajiwa za wanaume na wanawake zinahusiana na mazingira anamoishi mtu.

Kwa mujibu wa msailiwa 1, mwanamume katika jamii ya Waidakho anahusishwa na mkusanyiko wa sifa zinazojengeka katika jamii ya Waidakho. Sifa hizi hufafanuliwa kuwa za kiume kwa sababu ya mtazamo wa Waidakho wa maana ya kuwa mwanamume. Kutokana na fasili ya jamii hii, mwanamume halisi ana sifa za kitabia za wanaume ambazo lazima wakubaliane na viwango vilivyoainishwa vya kitamaduni vya uanaume katika jamii yao. Ubabedume umebainishwa katika sherehe za upiganishaji fahali na kuelezwa kulingana na utamaduni, falsafa, imani, itikadi, mila na desturi za

jamii ya Waidakho. Ubabedume unaobainika katika sherehe za upiganishaji fahali ni kiwakilishi kamili cha itikadi ya jadi ya Waidakho kuhusu mwanamume. Ubabedume huu umejengwa kwa misingi ya taasubi ya kiume ambapo mwanamume ni mtawala na mwanamke ni mtawaliwa. Ubabedume katika jamii ya Waidakho umepitishwa kupitia nyimbo ambazo hujitokeza katika sherehe za upiganishaji fahali.

Nyimbo ni vyombo muhimu sana ambavyo msanii yeyote yule huvifumbata ili kumwezesha kuyapitisha maudhui, ujumbe na matakwa yake hadi kwa hadhira husika. Vilevile, husheheni mila, utamaduni, desturi, itikadi, mitazamo, matarajio na mielekeo mbalimbali ya jamii. Utafiti ulijikita katika kuchunguza ubabedume katika sherehe za upiganishaji fahali katika jamii ya Waidakho magharibi mwa Kenya. Ili kulifikia lengo hili, tumetumia nyimbo mbalimbali zilizoimbwa na wasanii wakati wa sherehe za upiganishaji fahali na ishara zilizodhihirika kama ithibati mwafaka ya kuendeleza uchanganuzi na mjadala huu.

### 4.2.1 Mwanaume kutoonyesha Hisia

Kulingana na msailiwa 2, ubabedume miongoni mwa wanaume Waidakho ni zao la fikra akilini mwao kuhusu tafsiri za kiutamaduni na mazingira waliyolelewa nayo yanayokuza ujanadume. Mwanamme katika jamii ya Idakho hafai kuonyesha udhaifu alionao kwa jamii ila anafaa kuonyesha unajanadume wake hata katika hali ya kudunisha. Hivyo, mara nyingi watoto wa kiume hufundishwa na kujulishwa kila mara tangu utotoni mwao kuwa mwanamume hafai kuonyesha hisia za kulia bali anafaa astahimili hali anayokumbana nayo.

Ubabedume una sifa ya kutoonyesha hisia haswa wakati mwanaume anapokumbana na hali ngumu au changamoto inayomsababishia uchungu (Edell, keshatajwa). Ubabedume hutokea haswa mwanaume anapostahimili uchungu na kutoonyesha hisia zake. Mwanaume aliyemkali hupewa heshima na kuonekana mwanaume kamili katika jamii yake. Hata hivyo, hutumiwa kama mfano katika mafunzo ya kijamii katika tohara ili aonekane kama mfano bora kwa mtoto wa kiume ambaye anakua. Kielelezo kifuatacho kinaonyesha sifa ya mwanaume ya kutoonyesha hisia zake licha ya kukabiliwa na changamoto katika kufanikisha shughuli za kijamii kupitia sherehe za upiganishaji fahali.

**Wimbo 1 : Vasatsa vali he**

| Kiluhya | Tafsiri |
|---|---|
| *Vandu varevananga vasatsa vali he* | Watu wanauliza wanaume wako wapi |
| *Vasatsa yavo ×2* | Wanaume ndio hao ×2 |
| *Nutsia wavamenya vasatsa valulayo* | Ukienda kwa maboma zao wanaume ni wakali |
| *Vasatsa yavo ×2* | Wanaume ndio hao ×2 |
| *Ulihe lili vasatsa vasinjila* | kwenye vita wanaume wamesimama tisti |
| *Vasatsa yavo ×2* | Wanaume ndio hao ×2 |

Kwa mujibu wa wimbo 1, mwimbaji ameonyesha sifa ya mwanaume kupitia nafasi yao ya kulinda jamii wakati vita vinatukia kutokana na tendo lao la kusimama tisti. Mwimbaji ameimba wimbo huu katika sherehe za upiganishaji fahali kumkumbusha mwanaume hafai kuwa dhaifu anafaa kuonyesha ubora wake na kustahimili uchungu ili kuepuka mshindi.

Kulingana na msailiwa 2 (keshatajwa), katika jamii ya Waidakho, mtoto wa kiume hufunzwa akiwa mchanga kuwa hafai kulia. Kulia kumetengewa wanawake kwa kuwa huwa wepesi wa hisia haswa wakati wa vita au msiba. Baadhi ya wanawake huomboleza waume zao wakitamka w***oi musatsa wanje ukhutsi*** kwa maana kuwa mume wangu amefariki. Wanaume katika jamii ya Waidakho kupitia nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za upiganishaji fahali wanaonywa dhidi ya kulia ila heri wafe katika uchungu kuliko watende kitendo kitakachowalinganisha na wanawake. Anafaa kuvumilia asionyeshe udhaifu wake. Mtoto wa kiume anapokua hukumbana na hali mbali mbali kama vile kuanguka katika harakati za michezo. Katika hali hii, mlezi hukuza ujasiri kwa kumwonya dhidi ya tabia za kulia ovyo ovyo kama mwanamke. Tendo hili la kuonyesha hisia huwafanya kuonekana dhaifu mbele ya wenzao.

Kwa kurejelea Wimbo 1, mwimbaji anasisitiza kuwa wanaume wanapaswa kuwa wakali wanakoishi; wawe na msimamo na msimamo dhabiti kutokana na yale wanayotenda. Katika jamii ya Waidakho mwanaume asiyeonyesha hisia katika hali ya uchungu humiliki sifa ya kuwa mkali na kuheshimiwa katika familia yake na katika jamii kwa ujumla na kuonekana kama mwanamume kamili.

### 4.2.2 Mwanaume kama anayemiliki Mali

Jamii ya Waidakho inamtambua mwanamume kama mumiliki wa ardhi na mali. Hivyo, mwanamume ana jukumu la kukimu familia yake na kutegemewa katika sekta ya maisha katika familia. Jukumu hili huwa ni tamaduni na itikadi ambayo ni sharti itekelezwe. Familia ya mwanawake hutazamia suala hili sana ambapo kabla ya kuoza mwanao ni sharti wajue historia ya familia ya mwanamume na kule atokako. Aidha, ili mwanamume aonyeshe uwezo wake wa kukimu familia yake ni sharti ashirikishwe katika kulipa mahari kwa familia ya msichana anayeoa.

Kulingana na Wash (1997), nadharia ya ubabedume huhusisha uwezo wa mwanamume kuwa na uwezo wa kukimu na kutosheleza mahitaji ya familia. Wash (keshatajwa) anauona ubabedume kama tabia ambazo zimejengwa kutokana na misingi ya kitamaduni ya jamii ambao utazidi kupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Jamii ya Waidakho wanaume wamesawiriwa kuwa wa kutegemewa na wenye kutegemewa na wenye kumiliki mali kama inavyojitokeza katika Kielelezo 2.

Wimbo 2 : **Mang'ondo mu Posta**

| **Kiluhya:** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Inzi musatsa ndarumila* | mimi mwanamume nilituma |
| *mangondo muposta* | pesa kwa posta |
| *Mama wanje na mukhali nu wanje* | mama yangu na mke wangu |
| *vakuli khanyama* | Wanunue nyama |
| *Khandi nindumila khandi mukamba papa wanje* | tena nikatumia baba yangu |
| *akuli isuti* | Anunue suti. |

Sifa ya mwanamume kumiliki mali inatokea katika Wimbo 2 anapoamua kuwacha familia yake na kuenda kutafuta riziki mjini. Mwanamume anapopata mali yeye huhakikisha kuwa ni lazima aikimu familia yake. Katika mshroro wa tatu, *mama wanje na mukhali wanje vakuli khanyama kumaanisha* mama yangu na mke wangu wanunue nyama. Hii ni idhibati tosha kwamba mwanamume anajali familia yake kwa kuhakikisha mkewe pamoja na mama yake ambaye amezidi umri wanapata chakula.

Kulingana na Msailiwa 3, Jamii ya Waidakho inaamini kuwa mwanamume akikosa mali hawezi tunza mkewe kutokana na sababu wanawake hawaruhusiwi kumiliki mali ila kutunza mumewe na katika kutekeleza shughuli za nyumbani. Mwanamke

hulazimika kutafuta mume mwingine nje ya ndoa ili aweze kuisaidia familia yake. Kilingana na Kielelezo hiki ambacho kinafasiliwa na mila na desturi za Waidakho, ni dhahiri kuwa mwanamume hudharauliwa na kuonekana asiye miliki sifa ya ubabe. Mwanaume alitarajiwa kulipa mahari kwa wazazi wa msichana anayeoa kwa njia ya fahali. Hii ni kwa sababu, fahali walikuwa mali ya mwanamume.

### 4.2.3 Mwanamume kama mwenye Uwezo na Nguvu

Kulingana na Connell (1995), nadharia ya ubabedume hubainisha na kuelezea namna mwanamume anamiliki nguvu na mamlaka dhidi ya mwanamke au mwanamume mwenza kutokana na matakwa na mielekeo ya jamii husika. Sifa ya mwanamume kama mwenye uwezo na nguvu inajitokeza katika wimbo unaoimbwa katika sherehe za upiganishaji fahali kama inavyoonekana katika kielelezo 3.

Kielelezo 3 : **Mama yangaya**

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Mama yangaya ×2* | mama alinikataza |
| *Mama yangaya khale* | mama alinikataza kitambo |
| *Mama yangaya khale* | mama alinikataza kitambo |
| *Mama yangaya khale makhuba* | mama alinikataza kitambo mambo |
| *Ka vakhali vavili* | ya kuoa wake wawili |
| *Nuhila vakhali vavili ukona manya shihuvi* | ukioa wake wawili utalala kama mwizi |
| *Mbukono.* | Kwa malazi |
| *Mama yangaya khale ×2* | mama alinikataza kitambo |
| *Yangaya khale makhuva ka vakhali vavili ×2* | alinikataza mambo ya kuoa wake wawili |
| *Nuhila vavili ukona ninzala munda* | ukioa wawili utalala na njaa |

Mwimbaji anadhihirisha kuwa mwanamume anajitambulisha kutokana na kuoa wake zaidi ya wawili. Mwimbaji anamsawiri mama yake mzazi katika juhudi za kumkataza na kumwonya mwanawe kuoa wake zaidi ya wawili atalala njaa. Fasili ya mwimbaji katika wimbo huu ni kuhatarisha wanaume kuoa wake wengi ambapo athari yake ni kuwepo kwa majukumu mengi katika familia yake. Ushauri wa mwimbaji hata hivyo unakinzana na matarajio ya mwanamume katika jamii ya Waidakho ambayo inasisitiza umuhimu wa wanaume kuwa na watoto wengi kama njia moja ya kuzalisha utajiri.

Mwimbaji anaonyesha wazi kuwa, licha ya ushauri anaopewa mwanamume huyu anampuuza mamake kutokana na mila na desturi za Waidakho. Mila hizi huwadunisha

na kuwanyima nafasi wanawake ya kuwashauri wanaume ila wanafaa kuwatii wanaume hata kama wanatenda kinyume. Mwanaume atakosolewa na mwanaume mwenza ambaye amemzidi umri. Mwanaume atakosa kufuata ushauri wa mwanamke katika jamii ya Waidakho kama njia ya kuonekana wenye ubabe na wasio na dosari. Wanaume katika jamii ya Waidakho wana nguvu na uwezo wa kuoa wake wengi kama njia ya kujitambulisha miongoni mwa wanaume wenzake. Mwanaume aliyeoa mke mmoja au asiyeoa huhesabiwa kuwa mwanaume asiye na nguvu na uwezo. Wanaume hawa walisutwa na kutohusishwa katika shughuli muhimu za kijamii (Rita, 2014).

### 4.2.4 Mwanamume kama mwenye Busara

Mwanamume ni kiumbe cha maana katika jamii ya Waidakho kama mwenye busara zaidi katika kutekeleza mahitaji mbalimbali ambayo yanafungamana na utamaduni na itikadi za jamii. Kulingana na nadharia ya ubabedume, wanaume ambao hufuata itikadi na utamaduni wa ubabedume na kujitambulisha kama wanaume huonyesha ufanisi mkubwa wa kibinafsi. Kauli hii ina maana kuwa wanaume hawa hudhihirisha fikra na mawazo ya kiume na huonekana kama wenye bidii katika kutenda kazi zao kikamilifu. Sifa hii ya kufanya maamuzi ya busara yanatukia katika wimbo unaoimbwa katika sherehe za upiganishaji fahali kama inavyodhihirika katika Wimbo 4.

Kielelezo 4 : **Khutsi khungo**

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Khwenyanga khutsi khungo* | Tunataka twende nyumbani |
| *Hango hu khwalekha vulimu vyayumba* | nyumbani tulikotoka pamegeuka msitu |
| *Khwenyanga khulikorela Mombasa ×2* | unataka tupotelee Mombasa ×2 |
| *Mushiele wanje khutsi khungo* | mke wangu twende nyumbani |
| *Ooh mukhali wanje* | ooh mke wangu |
| *Khutsi khungo* | twende nyumbani. |

Kwa mujibu wa Wimbo 4, mwimbaji anamrejelea mwanamume ambaye alihama kutoka kwenye jamii ya Waidakho akahamia mjini Mombasa pamoja na mkewe. Akiwa huko anawazia boma lake jinsi lilivyo baada ya siku nyingi alipohama. Mwanamume huyu anafanya uamuzi wa busara wa kumwambia mkewe warudi nyumbani walikotoka wajenge boma lao linalogeuka kuwa msitu.

Mwimbaji katika Wimbo 4 alinuia kuonyesha nafasi ya mwanaume kuwa anafaa kuhakikisha kuwa boma lake ni nadhifu pasipo na misitu inayosababisha wanyama hatari kujificha na kumdhuru yeyote. Kulingana na kauli hii sifa ya ubabedume inajitokeza. Kama inavyojitokeza kwenye wimbo 4, mwanamume kamili anaonekana kupitia juhudi anazofanya katika kuboresha Boma Lake. Mwanamume atapanda ua kwenye boma lake kulinda mkewe pamoja na watoto wake kutokana na adui. Boma la mwanamume kamili katika jamii ya Waidakho linafaa kufyekwa, apande chakula kingi shambani na afuge mifugo wengi ili kuzalisha mali.

Mwimbaji anatambua mwanaume kama mwenye busara na anafaa kufikiria mambo kwa undani bila kushurutishwa na mwanamke. Akilini mwake anafaa kuwa na masuala mengi kuhusu maisha yake na maisha ya familia yake ambayo hana budi kuyatatua na kuyaboresha. Anafaa kuwa tayari kuipokea na kuifuata fikra yoyote inayobadilisha mtindo wake wa maisha japo iwe ya hatari.

### 4.2.5 Mwanamume kama Shujaa na Jasiri

Katika sherehe za kupiganisha fahali, ni sharti anayeshiriki awe na klabu ambayo kila mtoto wa kiume anaulizwa kujitengenezea mwenyewe ambapo anatarajiwa kuiweka hadi uzeeni. Wazee pia wana mamlaka ya kuonekana wakibeba klabu hizi. Utamaduni huu hauhusiani na Waidakho pekee. Katika utamaduni wa Waidakho hii inaashiria uanaume, mamlaka na nguvu (Kabaji, 2008). Viongozi wengi katika siku ya kuadhimisha utamaduni hubeba vilabu vyao kuonyesha wana nguvu katika kuongoza jamii hii ya waidakho. Mara kwa mara ataibeba popote anapokwenda kama njia ya kujitambulisha. Ushujaa na ujasiri wa mwanamume unatokea katika Wimbo ufuatao katika sherehe za upiganishaji fahali.

Wimbo 5 : **Vandu varia**

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Ulwa ingwe ulwa isimba nihuma* | Ukiwaskia chui na samba wakiguruma |
| *Vandu vasatsa vechanyanga vandu varia* | Wanaume wanashangaa watu ni waoga |
| *Khali kuve vutukhu ama mbasu vandu varia* | Hata iwe usiku ama mchana watu ni waoga |
| *Musatsa nachingi shikong'o shie* | Mwanamume akibeba klabu yake |
| *Vandu varia* | Watu ni waoga |
| *Khali vasatsa valangwa mulihe* | Ata wanaume wakiitwa vita |
| *Vatsiku varia* | Maadui wanaogopa |

Kwa mujibu wa 5, mwimbaji anamrejelea mwanamume kama mwenye kutegemewa haswa jamii inapokumbwa na maadui. Mwimbaji anamlinganisha mwanaume na simba ambaye ni hatari sana. Mnyama huyu ana sifa za kuogofya za kimaumbile na pindi tu anapoguruma watu hujawa na hofu. Mwimbaji anasisitiza kuwa mwanaume kamili anafaa awe jasiri kama inavyojitokeza kwenye wimbo 5 ambapo kuonekana kwake na klabu kunawafanya watu wajawe na wasiwasi.

Kulingana na msailiwa 4, maandalizi ya mwanamume yalianza akiwa mchanga kwa kupewa chakula kingi kama njia ya kumfanya awe na nguvu na uwezo. Ili sifa za mwimbaji zionekane ni sharti ujasiri ukuzwe baada ya vijana kupashwa tohari ambapo walijiunga na kundi la umri kufunzwa mambo ya kivita na jinsi ya kuwa tegemeo kwa jamii haswa wakati wa mashambulizi na maadui. Wanamume mashujaa katika jamii ya Waidakho waliishi maisha ya kutengwa ili wasije wakajulikana kwa udhaifu wao. Mwanaume kamili wa Kiidakho hajitahidi kupata chakula. Anakula pekee yake wakati mke wake anakula pamoja na watoto

### 4.2.6 Mwanamume kama Mkware

Kulingana na Connell (1995), utamaduni wa jamii hudhibiti maisha ya jamii pamoja na mielekeo na mitazamo yao. Utamaduni wa jamii ya Waidakho hujikita katika desturi zao, lugha na imani ambazo hutamalaki katika mfumo mzima wa jamii katika kujitambulisha. Mwanamume katika jamii ya Waidakho hufurahia unyanyasaji wa bure wa ngono kama uthibitisho wao wa uanaume. Hata hivyo mwanamume anayezaa nje ya ndoa alichukuliwa kama mwanaume aliyekomaa. Mwanamke haruhusiwi kuolewa na mtoto kwa kuwa yeye husawiriwa kama kahaba. Mwanamume kama mkware inajitokeza katika Wimbo 6 kama ifuatavyo;

Wimbo 6 : **Shikong'o shianje**

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Kuka mbe shikongo shiange* | Babu nipe klabu yangu |
| *Mbee shikong'o shianje ×2* | Nipee klabu yangu ×2 |
| *Nzi khuserera isecheli* | Niende kushiriki ngono na wanawake *Isecheli* |
| *Ukhasera tawe ×2* | Usishiriki ngono nao ×2 |
| *Ulasila khumurego* | Utaanguka mtegoni |
| *Nukhurikale na vina.* | Tutabaki na nani. |

Kwa mujibu wa wimbo 6, mwimbaji anarejelea umuhimu wa ishara ya klabu katika harakati za mwanaume kujitambulisha na ubabe. Kwa mujibu wa msailiwa 1, Klabu ilitumika katika muktadha huu kuashiria mamlaka na nguvu. Mwimbaji katika wimbo wa 6 anamwomba Babu ampe klabu ili aende *isecheli* ili aende aridhishe tamaa yake ya kushiriki ngono na wanawake wa *isecheli*. Kujihusisha na wanawake katika sehemu ya i*secheli* inazua suala la ukware kwa kuwa sehemu hii inajulikana kutokana na shughuli za ukahaba ambapo wanawake walishiriki ngono kama njia moja ya kujikimu baada ya mabwana zao kupoteza maisha yao katika harakati za kulinda jamii dhidi ya adui. Msailiwa 4 anaeleza kuwa kutambuliwa kwa mwanamume kulitokana na juhudi za unyonyaji wa ngono. Pia mwimbaji anaibua sifa ya ukware kupitia wimbo wa 7 ifuatavyo

Wimbo 7 : **Fwala ikondomu**

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Nunyoli lingangule* | ukipata malaya |
| *Fwalaa* | Vaa |
| *Fwala ikondomu* | vaa kinga |
| *Khali nali mukhali wa mundu* | hata akiwa bibi ya mtu |
| *Fwalaa* | vaa |
| *Fwala ikondomu* | vaa kinga |

Katika wimbo 7,mwimbaji anaonyesha jinsi mwanamume amekubaliwa kufanya ngono bila kujali ni malaya au mke wa mtu ila ni sharti ajikinge. Kwa hivyo, mwimbaji anaonyesha sifa ya kuwa mkware kutokana na kujulikana kwa mwanamume kuwa na uwezo wa kushiriki ngono kwa kuangazia idadi ya wanawake alioshiriki nao. Wanaume ambao hawana sifa hizi za ukware walirejelewa kama wasio kuwa na uwezo na wasio na sifa za ubabedume.

### 4.2.7 Mwanamume kama Mtu wa kutegemewa

Kulingana na Kimmel (2014), jamii ambayo ina wanaume ambao wanashikilia na kuenzi itikadi za ubabedume na kujitambulisha kama wanaume kamili wamepiga hatua katika kujikomboa na kukomboa jamii yao. Jamii ya Waidakho inashikilia kuwa wanaume ni sharti wawe wa kutegemewa kama anavyoshikilia (Kimmel, Keshatajwa) kuwa ubabedume umeundiwa mtu binafsi kama mkusanyiko wa sheria ambazo hutoa maelezo ya mtu binafsi. Mwanaume wa aina hii hufanya kila juhudi kutafuta kazi ya

kufanya ili aikimu familia yake. Mwanamume anaonyesha sifa ya kutegemewa kupitia wimbo 8 ufuatao;

Wimbo 8 : **Nulangwaa**

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Nulangwaa* | Ukiitwa |
| *Eeeh* | Kubali |
| *Nulangwa Uvolenge ndi hanu* | Ukiitwa unaitikia unasema uko hapa |
| *Musatsa nalangwa, Eeeh* | Mwanaume ukiitwa itika |
| *Musatsa nalangwa avolenge ndihanu*. | Mwanamume akiitwa itika useme niko hapa. |

Kwa kurejelea wimbo 8, mwimbaji anasema, *musatsa nulangwa uvolenge ndihanu* yaani mwanamume ukiitwa aseme ako hapa, mwimbaji anasisitiza kuwa katika jamii ya Waidakho, mwanamume anafaa awe mtu wa kutegemewa. Mwanamume ambaye ako tayari kupigania jamii yake kutokana na maadui wake anamiliki sifa za uanaume. Mwanaume anafaa awe tayari kwa lolote lile. Katika familia, mwanaume ndiye kiongozi ambaye anafaa kuhakikisha usalama wa jamii yake.

Aidha, juhudi za mwanamume katika kuonyesha uwajibikaji unaelezwa katika wimbo 9 kutokana na jinsi mwimbaji anavyowatia nguvu katika harakati zao za kutafuta riziki. Licha ya wimbo 9 kuimbwa katika tafsiri ya Kiswahili, wimbo huu una maana katika sherehe za upiganishaji katika kuwatia moyo wanaume kama ifuatavyo katika wimbo 9.

Wimbo 9 : **Wanaweza**

Tafsiri
Wanaweza,
Wanaume
Wanawezaa
Hata kama itachukuwa muda
Wanaume tunaweza.
Hata kwa dhiki,
Tunaweza hata kama itachukuwa muda
Wanaume tunaweza.

Kwa mujibu wa wimbo 9, mwimbaji ameuimba wimbo huu katika lugha ya Kiswahili bila tafsiri ya Kiidakho katika sherehe za upiganishaji fahali. Lengo la ujumbe huu ulilenga kuwafikia wanaume wote wanaoishi katika kabila zingine nchini Kenya

kutokana na juhudi wanazozitekeleza katika kuimarisha ubabedume. Mwimbaji alilenga kuwatia wanaume nguvu kuwa licha ya changamoto wanazokumbana nazo katika hali ya kutegemewa, wataibuka washindi kutokana na juhudi zao.

Kulingana na mwimbaji katika wimbo 9 kuhusu tamaduni za waidakho, ni sharti mwanamume ajitolee kuzimbua riziki ili aweze kumlinda mke wake. Mwanamume ambaye hawajibiki basi mwanamke atalazimika kupata usaidizi kutoka kwa mwanamume mwingine. Hali hii itamsababishia mwanamume huyu aibu na kuonekana asiyemiliki sifa za uanaume. Mwanamke atamdharau na kutafuta mwanaume halisi. Katika hali hii mwanamke ana haki ya kuhama na kutafuta mume mwingine ambaye ana sifa za kuonyesha ubabe wa kuikimu familia yake.

### 4.2.8 Mwanamume kama mtu mkali mwenye msimamo dhabiti

Juhudi za kumtayarisha mwanamume katika jamii ya Waidakho zilianza pindi tu mtoto wa kiume alipopashwa tohari. Katika kipindi hiki mtoto wa kiume alifunzwa jinsi ya kuishi kama mwanamume na mambo ya kuepuka ili asije akawa mwanamume mwoga au asiyejua mahitaji yake ya kijamii. Mwanamume hakuruhusiwa kulia wakati wa kutahiri. Hii ni ishara ya mwanamume kamili. Kustahimili makali hayo ni ishara ya kumpokeza ujasiri na kuondoa uoga. Mwanamume anaonyesha msimamo wake na ukali kupitia wimbo 10 kama inavyojitokeza katika sherehe za upiganishaji fahali.

Wimbo 10 : **Mulina Wanje**

| **Kiidakho** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Mulina wanje murende wanje* | Rafiki wangu Jirani wangu |
| *Ooh eeh! ooh eeh !* | Ooh eeh ! ooh eeh! |
| *Mbele khureve ni watila khushindu shindu shiumundu* | Nilifaaa nikuulize kama umewahi shika kitu cha mtu |
| *Isisi ni wanje ivweru ni wowo* | Chumba cha kulala ni kwangu na sebuleni ni kwako |
| *Ooh eeh !ooh eeeh!* | Ooh eeh! Ooh eeh! |
| *Mundu mukhali mbele khureve ooh eeh* | Mwanamke nilifaa nikuulize ooh eeh |
| *Nu watila khushindu shiu mundu.* | Kama umewahi shika kitu cha mtu |

Kwa kurejelea wimbo 10, mwimbaji anamrejelea mwanamume kuwa na sifa ya ukali na msimamo dhabiti kutokana na maamuzi anayofanya katika familia yake na katika kukuza usiri wake. Kulingana na wimbo 10, mwimbaji anatamka kauli; *khutila khu shindu shiu mundu* yaani kuguza kwa kitu cha mtu ina maana kuwa mwanamke ni mvunja sheria. Aidha mwimbaji pia anatumia kauli; *isisi ni wanje ivweru ni wowo* yaani

chumba cha kulala ni maakazi maalum ya mwanamume na sebuleni ni kwa mwanamke ambapo ni mahali pa kuwakaribisha wageni.

Mwimbaji anarejelea kwa kusisitiza tamaduni za Waidakho kwa watoto kuwa, hawaruhusiwi kuingia kwenye chumba cha kulala cha babake. Sehemu hii huheshimiwa sana. Wanaume kupitia mwimbaji wanaelimishwa (*nutsia isisi kenyakhana ukhole shisatsa*) wakienda kwenye chumba cha kulala wanafaa watende kiuanaume. Katika chumba chake cha kulala, mwanaume ana uhuru wa kukaa uchi anapopumzika au kufanya mambo yake ya kisiri bila kujulikana ila tu mkewe ambaye ni rafiki yake na jirani yake.

Mwimbaji anamwonya Mwanamke dhidi ya kumleta mwanamume mwingine kwenye chumba chake cha kulala. Anamweleza kuwa akiwa na mgeni akae sebuleni. Mwanamke anafaa awe mtumwa kwa mwanamume, atende kulingana na matakwa ya mumewe. Mwanamke asipotenda haya hurudishwa kwao nyumbani apate mafunzo jinsi ya kumheshimu mumewe. Wengine hupata adhabu na mumewe ili wawe mfano mwema kwa watoto wanaokua. Mwimbaji katika wimbo 10 anadhihirisha nafasi ya mwanaume kuonekana mkali wa mwanamume inatokana na msimamo wa mwanamume huyo katika kuyatekeleza majukumu yake na katika kuongoza familia yake.

**4.3 Hitimisho**

Uchunguzi wa suala la ubabedume katika nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za upiganishaji fahali umebainisha kuwa sifa za ubabedume zinapatikana katika sherehe za upiganishaji fahali. Sifa hizi husaidia katika kuwasilisha maudhui yanayopatikana katika sherehe za upiganishaji fahali. Kutokana na uhakiki wa nyimbo hizi, usawiri wa mwanamume katika sherehe za upiganishaji fahali umedhihirika. Uchanganuzi wa sifa za mwanamume katika nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za upiganisaji fahali unatusaidia katika kuelewa mielekeo na matarajio ya Waidakho kuhusu nafasi ya mwanamume na mahitaji ya mwanamume katika jamii ya Waidakho. Mtazamo na mielekeo ya kitamaduni ya Waidakho kuhusu dhana ya ubabedume imebainika bayana. Sifa zinazojitokeza katika sherehe za upiganisaji fahali zinaweka wazi nafasi na wajibu wa mwanamume katika jamii ya Waidakho.

Utafiti huu ulichunguza namna ambavyo mwanamume alipitia mafunzo ya kijamii ili kuelewa iwapo matayarisho haya ya kuwa mwanaume yalichangia usawiri wa nafasi ya mwanamume katika jamii ya Waidakho. Kama alivyoeleza mmoja wa wasailiwa Luyuku, mwanamume wa Kiidakho alifunzwa kupitia hafla za tohara ambapo walifunzwa namna ya kuwa mwanamume kupitia kuiga vitendo vya baba zao na mashujaa mbalimbali katika jamii. Sherehe za upiganishaji fahali nazo zilitunga nyimbo mbalimbali ambazo ziliwakubusha majukumu yao.

# SURA YA TANO

# MAUDHUI YA UBABEDUME KATIKA NYIMBO ZINAZOIMBWA KATIKA SHEREHE ZA UPIGANISHAJI FAHALI

## 5.1 Utangulizi

Lengo kuu la sura hii ambayo inajibu swali la pili la utafiti huu ni kuibua, kuelezea na kujadili vipengele vya kimaudhui vinavyojitokeza katika nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za upiganishaji fahali ili kudhibiti suala la ubabedume. Katika sura hii, kuna uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo yaliyokusanywa uwanjani kwa kutumia uchunzaji-shiriki na utazamaji, kinasasauti, kamera za picha. Data iliyokusanywa iliibua maudhui ya ubabedume yanayobainika katika sherehe za upiganishaji fahali kama kiwakilishi kamili cha itikadi za jadi ya Waidakho kuhusu mwanamume.

## 5.2 Maudhui ya Ubabedume

Maudhui huwa ni jumla ya mawazo yote aliyonayo mwandishi wa kazi ya fasihi pamoja na mitazamo yake juu ya mawazo hayo. Maudhui kwa kawaida hujumuisha mawazo pamoja na dhamira mbalimbali yaliyomsukuma msanii hadi akatunga na kusanii kazi fulani ya kifasihi. Hata hivyo, maudhui hujengwa na vipengele kama vile dhamira, migogoro, falsafa, ujumbe na msimamo katika kazi hiyo ya mwandishi au mtunzi wa kazi ya kifasihi. Fasihi huwasilisha maudhui kama zilivyo tanzu zingine za kifasihi kupitia nyimbo kama njia ya kutekeleza majukumu mbalimbali katika jamii kwani ni rahisi sana kuteka makini ya hadhira (Senkoro, 1979).

Kulingana na Wamitila (2008) maudhui ni jumla ya masuala au mambo yanayoshughulikiwa katika kazi ya kifasihi kama vile nyimbo. Maudhui hujumuisha dhamira, itikadi, msimamo, maadili, mafunzo na falsafa. Ni dhahiri kusema kuwa msanii huwa na uhuru mkubwa wa kuteua lugha, mada na ujumbe anaoukusudia uwafikie hadhira yake. Msokile (1993:58) anasema kuwa maudhui ni jumla ya mambo yanayoelezewa ama kujitokeza katika kazi ya kifasihi. Maudhui ya kazi ya kifasihi hujumuisha dhamira, mtazamo ama msimamo, ujumbe, maadili na falsafa. Mawazo ya mhakiki huyu yameonyesha uhusiano sawia dhamira na ujumbe unaokusudiwa kuwasilishwa na mtunzi kwa njia ya kimaandishi. Hata hivyo, watunzi wengi katika jamii ya Waidakho walijikita sana kuelezea ujumbe unaolenga mila na itikadi za Waidakho katika kukuza ubabedume miongoni mwa watoto wa kiume. Haya

yalifanikiwa kupitia uteuzi wa lugha, dhamira, mtazamo na falsafa zinazokubalika na utamaduni wa Waidakho.

Mungania (1985) anasema kuwa mwandishi huandika yale ametayarisha kuwasilisha kwa njia ya ubunifu. Hapo ndipo mhakiki anapofasiria msomaji ili aone mambo kwa uwazi na kwa kupenya jicho la ndani kuliko alivyosoma awali. Kwa msingi huo tuna azimio la kuchanganua aina mbalimbali za maudhui na jinsi kipengele cha taswira kinavyotenda kazi ili maudhui ya mtunzi na yatakayotokana na utafiti wetu yaaangaziwe. Masuala yanayojitokeza katika nyimbo za upiganishaji fahali huwa ni matokeo ya tajriba za maisha, itikadi za jamii, mahusiano ya kijamii na mitindo ya maisha ya kila siku ya jamii ya Waidakho. Nyimbo hizi vilevile kutokana na maudhui yake huweza kuonyesha aina za mahusiano au hata matukio muhimu katika jamii ya Waidakho hasa ya kihistoria yanayopaswa kukumbukwa.

Nyimbo za upiganishaji fahali huwa na mikakati fiche inayotumika kuuliza, kuchanganua na kubadilisha mahusiano ya kijamii na mielekeo ya jamii ya Waidakho inayojikita na mila na desturi zao (Nyatuoro,2021). Mikakati hiyo inayaweka wazi mapambano ya kisiri na kwa hivyo kushawishi na kuleta maswala ya mawanda ya umma ambayo yamefichwa lakini yenye umuhimu katika kuonyesha upembezaji wa washiriki wa kijamii na makundi yanayokinzana. Yafuatayo ni maudhui yanayotawala katika nyimbo za upiganishaji fahali zinazolenga kutoa msimamo na mielekeo ya nafasi ya mwanamume katika kujenga suala la ubabedume katika jamii ya Waidakho.

### 5.2.1 Maudhui ya Ukatili

Maandalizi ya kumwandaa mtoto wa kiume huanza akiwa mchanga kwa kuhusishwa katika shughuli za kiume. Katika umri huu watoto wa kiume hupewa mafunzo ya jinsi ya kukabiliana na changamoto maishani kwa kuhusisha katika mitihani ya maisha kama kuwaua wanyama pori. Aidha, mtoto wa kiume hushauriwa dhidi ya kulia haswa anapokumbana na changamoto hizi na kuhusishwa na wanawake kwa kuwa ni wepesi wa hisia. Mwanamume ametawala na kumfanya mwanamke mtumwa na atende kulingana na matakwa yake. Wanawake wanaokaidi waume zao hupewa adhabu kama alivyo mtoto mdogo anapokosolewa akifanya makosa. Maudhui ya ukatili katika jamii yanaelezwa kupitia wimbo 11 kama ifuatavyo;

Wimbo 11: **Vasatsa Vali he**

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Vandu varevananga vasatsa vali he* | Watu wanauliza wanaume wako wapi |
| *Vasatsa yavo ×2* | Wanaume ndio hao ×2 |
| *Nutsia wavamenya vasatsa valulayo* | Ukienda kwa maboma zao wanaume ni wakali |
| *Vasatsa yavo ×2* | Wanaume ndio hao ×2 |
| *Ulihe lili vasatsa vasinjila* | kwenye vita wanaume wamesimama tisti |
| *Vasatsa yavo ×2* | Wanaume ndio hao ×2 |

Kulingana na wimbo 11, mwimbaji anaibua maudhui ya ubabedume kutokana na nafasi ya mwanamume katika utendakazi wa sekta muhimu katika jamii ya Waidakho. Mwimbaji hata hivyo anaonyesha jinsi mwanaume anachukua msimamo wa kuwa mkali ili kudhibitisha ubabe. Mwanaume katika wimbo huu anasawiriwa kuwa wa maana katika kutekeleza uongozi kwenye familia yake na ulinzi wa jamii dhidi ya maadui. Kulingana na tafifi za mtafiti ambaye aliishi miongoni mwa jamii ya Waidakho katika harakati za kukusanya data, aligundua kuwa mwanamume ameonyesha utawala dhidi ya mwanamke na kumgeuza mtumwa ambapo anafaa atende kulingana na matakwa yake. Wanawake wanaokaidi waume zao wanapata adhabu kama alivyo mtoto mdogo kama njia ya kumkosoa.

Mwimbaji pia anaeleza kuwa jamii inajivunia kuwepo kwa wanaume katili kwa kuwa wao huwa ngao ya jamii na kukinga jamii dhidi ya maadui. Mwimbaji anashauri zaidi kuwa mwanamume kamili katika jamii ya Waidakho anafaa aonyeshe ujasiri wake kwa kusimama tisti kama njia ya kuonyesha yu tayari kukabiliana na changamoto. Mwanamume katika jamii ya Waidakho anafaa kuonyesha sifa ya ubabe kwa kustahimili maumivu anapokumbana na adui ili aweze kuwa mshindi. Aidha, wanaume katika jamii ya Waidakho wanalinganishwa na fahali ambaye huandaliwa kushiriki mapambano ambapo licha ya majeraha kutoka kwa mpinzani anavumilia na kuibuka mshindi (Ouma, 2016).

### 5.2.2 Maudhui ya Utajiri

Utajiri katika jamii ya Waidakho hutokana na umiliki wa watoto wengi, mifugo na ardhi wala sio kiwango cha pesa. Mwanamume kuwa na watoto wengi ni utajiri kutokana na nafasi waliyo nayo katika kuzalisha mali nyingi. Watoto wa kiume husaidia katika kuwalisha mifugo na kufanya kazi za nyumbani. Wanaume huoa wake wengi ili wapate watoto wengi. Aidha, ubabe wa mwanaume utajitokeza kutokana na idadi kubwa ya

watoto. Utafiti huu hata hivyo umedhihirisha maudhui ya utajiri katika jamii ya Waidakho kutokana na wimbo wa 12 kama ifuatavyo.

Wimbo 12: **Mangondo muposta**

| **Kiluhya:** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Inzi musatsa ndarumila* | mimi mwanamume nilituma |
| *mangondo muposta* | pesa kwa posta |
| *Mama wanje na vakhali vanje* | mama yangu na wake wangu |
| *vakuli vana vanje khanyama* | Wanunulie watoto wangu nyama |
| *Khandi nindumila khandi mukamba papa wanje* | Tena nikatumia baba yangu |
| *akuli isuti khu anindili miruku chanje* | Anunue suti ili anilindie mifugo yangu. |

Mwimbaji katika Wimbo wa 12 anaonyesha nafasi ya mwanamume kama mwenye kumiliki mali haswa watoto wengi, mifugo na ardhi ni ishara tosha ya utajiri. Mwimbaji anamsawiri mwanamume kutokana na jinsi anavyojivunia watoto wake kwa kazi wanayomfanyia chini ya mwelekeo wa baba yake kwa kuhakikisha kuwa anatekeleza wajibu wake akiwa katika shughuli za kutafuta ajira. Mwimbaji anadhihirisha umuhimu wa mwanamume kuwa na mali kama njia moja ya kuweza kufanikisha majumu yake kama tunavyoona juhudi za mwanaume anayetajwa na mwimbaji katika kuhakikisha familia yake imepata chakula.

Mwanamume katika jamii ya Waidakho ni sharti aonyeshe ubabe wake kwa kuwa na watoto wengi kama ishara ya utajiri kwa kuwa watoto hawa husaidia kutunza mifugo na kufanya kazi za nyumbani. Mwimbaji anaibua suala la mwanamume kuoa wake wengi kama njia ya kuonyesha ubabe wake kutokana na uwezo alio nao kumudu mahitaji ya idadi kubwa ya watoto na wake zake. Kulingana na Papart (2016), mwanamke katika jamii ya Waidakho hakupaswa kumiliki mali ila walihusishwa katika shughuli za kumtumikia mwanamume kama kudumisha usafi, kupikia familia zao na shughuli za ulezi. Ubaguzi huu ulimpa mwanamume nafasi ya kumkandamiza mwanamke na kumweka katika hadhi ya chini.

### 5.2.3 Maudhui ya Ukware

Mwanamume katika jamii ya Waidakho hufurahia unyanyasaji wa bure wa ngono kama uthibitisho wao wa uanaume. Hata hivyo mwanaume kuzaa nje ya ndoa ni thibitisho la

kuonyesha mwanaume amekomaa. Suala la kuwa na idadi kubwa ya wanawake ulioshiriki nao ngono limeibua kuwepo kwa ubabe. Mwanamume katika hali hii ya kujitambulisha hana dosari yoyote kumpata mtoto nje ya ndoa. Wanaume waliodhaniwa kuwa wanyonge walitorokwa na wake zao na wengine walinyanganywa wake zao na wanaume waliokuwa jasiri na wenye uwezo. Mwanaume alipokea sifa sio haba kutokana na uwezo wake wa kushiriki ngono na idadi kubwa ya wanawake. Wimbo wa 13 unaeleza namna wanaume katika jamii ya Waidakho wanavyojihusisha katika shughuli za ukware ili waonekane wanaume zaidi wenye sifa za ubabe ikilinganishwa na wanaume wengine katika jamii.

Wimbo 13 : **Shikong'o Shianje**

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Kuka mbe shikongo shiange* | Babu nipe klabu yangu |
| *Mbee shikong'o shianje ×2* | Nipee klabu yangu ×2 |
| *Nzi khuserera isecheli* | Niende kuwatongoza wanawake Isecheli |
| *Ukhasera tawe ×2* | Usiwatongoze wanawake ×2 |
| *Ulasila khumurego* | Utaanguka mtegoni |
| *Nukhurikale na vina.* | Tutabaki na nani. |

Kwa mujibu wa Wimbo wa 13, mwimbaji anaibua suala la ukware kutokana na sababu kwamba mwanamume anatambuliwa kama mwanamume kamili kutokana na ujuzi na idadi ya wanawake ameshiriki nao ngono. Mwimbaji anaeleza kuwa mwanaume halisi alitambuliwa na idadi ya wanawake anashiriki nao ngono bila kubagua iwapo ni bibi ya mtu au la. Kwa mwanaume huyo jambo la maana ni kuwa na kinga. Dhana hii inakuza ukware miongoni mwa wanaume katika harakati za kutafuta ubabe.

Mwanamume katika wimbo wa 13, hana dosari yoyote kumpata mtoto nje ya ndoa. Wanaume ambao walidhaniwa kuwa wanyonge walitorokwa na wake zao na wengine walinyanganywa wake zao na wanaume waliokuwa jasiri na wenye uwezo kama anavyoeleza msailiwa 3 (keshatajwa). Kwa hivyo, ilibainika kuwa sifa za ubabe kwa mwanaume zilitokana na umaarufu wake wa kushiriki ngono nje ya ndoa kwa kuangazia idadi ya wanawake alioshirikiana nao.

Katika Wimbo wa 13, mwimbaji anamsawiri mwanamume kutokana na juhudi alizo nazo katika kujitambua kama mwanamume anapomwomba babake ruhusa na ujasiri wa kuwashurutisha wanawake wanaofanya kazi ya ukahaba sokoni i*secheli*. Aidha,

mwimbaji anamtambulisha baba yake mwanaume kama asiyefuata mila za Waidakho. Licha ya baba yake kupinga maamuzi yake mwanamume huyu anashikilia msimamo ya kudumisha ubabedume. Hii ni idhibati tosha kuwa mwanamume halisi katika jamii ya Waidakho alijulikana na kupewa sifa sio haba kutokana na uwezo wake wa kushiriki ngono na idadi kubwa ya wanawake.

Aidha, juhudi za mwanaume kuonekana mbabe kupitia ukware inajitokeza katika wimbo 14 kama ufuatavyo;

Wimbo 14**: Fwala Ikondomu**

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Nunyoli lingangule* | ukipata malaya |
| *Fwalaa* | Vaa |
| *Fwala ikondomu* | vaa kinga |
| *Khali nali mukhali wa mundu* | hata akiwa bibi ya mtu |
| *Fwalaa* | vaa |
| *Fwala ikondomu* | vaa kinga |
| *na nunyola khanyonyi khalai ivulitsa* | na ukipata msichana mzuri mpachike mimba |

katika Wimbo wa 14, mwimbaji anamweleza mwanamume kuwa asibague mwanamke awe kahaba au mke wa mtu bora atumie kinga. Mwimbaji akimshauri kinga ni njia moja ya kuwapa ujasiri wanaume kufanya tendo la ngono kiholela bila kuogopa magonjwa. Maelezo haya yaanashiria kwamba vitendo anavyovifanya mwanaume ili awe mwanamume kamili ni za ukware zisizokubalika kwani zinalenga kumkandamiza mwanamke. Aidha, maudhui ya ukware yanajitokeza katika Wimbo 15 kama njia ya kukuza na kuimarisha ubabedume kama ifuatavyo.

Wimbo 15 : **Mukhali Yandeva**

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Yandeva mukhali wanje yandevaa* | mke wangu aliniuliza |
| *Yandeva ukoni hena mudansi totoo* | aliniuliza nilikolala kwa dansi |
| *Yandeva ukoni hena mudansi mapaka mavweve* | aliniuliza nlilikolala kwa densi hadi asubuhi |

Kwa mujibu wa Wimbo 15, mwimbaji anaibua tabia aliyonayo mwanamume ya kutolala nyumbani bila idhini ya mkewe. Mwimbaji anamsawiri mwanamke kwa kuvumilia shida alizonazo dhidi ya mume wake. Tendo la kulala kwenye densi

linaashiria kuwepo kwa matendo ya ukware ambapo katika jamii ya Waidakho mahali palipo na densi pana makahaba na vitendo kama vile utumizi wa madawa za kulevya. Mwimbaji anaibua hisia alizo nazo mwanamke katika kukashifu mienendo ya mumewe ambayo ni kinyume na matarajio ya jamii ya Waidakho.

### 5.2.4 Maudhui ya Unyanyasaji

Edell (keshatajwa) anaeleza kuwa unyanyasaji wa kijinsia ni zao la ubabedume katika jamii ambapo wanaume huonekana bora na kuwa na nguvu ikilinganishwa na mwanamke. Wanaume hawa hutumia nafasi hii kuwanyanyasa wanawake kwa kuwanyima nafasi katika utekelezaji wa masuala muhimu yanayohusu jamii kama vile kushiriki maamuzi ya jamii na kutekeleza masuala muhimu katika jamii. Wanawake katika jamii nyingi za kiafrika wametengewa kazi za nyumbani kama vile kuwalea watoto na kuwapikia waume zao. Hata hivyo, suala la unyanyasaji linajitokeza katika jamii ya Waidakho kupitia nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za upiganishaji fahali kama inavyojitokeza katika Wimbo 16.

Wimbo 16 : **Murende wanje**

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Mulina wanje murende wanje* | Rafiki wangu Jirani wangu |
| *Ooh eeh! ooh eeh !* | Ooh eeh ! ooh eeh! |
| *Mbele khureve ni watila khushindu shindu shiumundu* | Nilifaaa nikuulize kama umewahi shika kitu cha mtu |
| *Isisi ni wanje ivweru ni wowo* | Chumba cha kulala ni kwangu na sebuleni ni kwako |
| *Ooh eeh !ooh eeeh!* | Ooh eeh! Ooh eeh! |
| *Mundu mukhali mbele khureve ooh eeh* | Mwanamke nilifaa nikuulize ooh eeh |
| *Nu watila khushindu shiu mundu.* | Kama umewahi shika kitu cha mtu |

Kwa kurejelea wimbo 16, mwimbaji anamrejelea mwanamume kwa kutompa nafasi sawa katika nyumba wanamoishi. Hili linatokea mwimbaji anapomsawiri mwanamume ambaye anaonyesha msimamo mkali kwa kumwonya mkewe kuwa sebule ndiko anakofaa kukaa na wanawe pamoja na wageni wanaomtembelea. Kauli hii inamnyima nafasi sawa mwanamke katika boma lake katika harakati za kumweshimu mwanamume. Kuwa na sifa ya ukali na msimamo dhabiti kutokana na maamuzi anayofanya katika familia yake na katika kukuza usiri wake. Kulingana na wimbo 16, mwimbaji anatamka kauli; *khutila khu shindu shiu mundu* yaani kuguza kwa kitu cha

mtu ina maana kuwa mwanamke ni mvunja sheria. Hii ni idhibati ya kutosha kuonyesha kuwa mwanamke ananyanyaswa na kila wakati anaonekana kuwa na dosari.

Kwa mujibu wa msailiwa 2, tamaduni za Waidakho haziwaruhusu watoto kuingia kwenye chumba cha kulala cha babake. Sawia na jinsi mwimbaji anavyoeleza msimamo wake kuhusu mkewe katika mahusiano yake chumbani, ni dhahiri kuwa mwanamume amemdunisha mkewe na kumweka kiwango kimoja na watoto ambao wanadhaniwa kuwa wavunja sheria.

### 5.2.5 Maudhui ya Ukakamavu

Kwa mujibu wa Masingu (keshatajwa), mwanamume kuonekana kuwa na uwezo na nguvu ni ishara ya ukakamavu. Maandalizi ya kuboresha nguvu na ukakamavu wa mwanamume huanza akiwa mtoto ambapo hupewa chakula kingi haswa ugali na uji akiwa mchanga ili anapokuwa awe na nguvu za kukabiliana na changamoto maishani na awe na uwezo wa kushiriki vita na kulinda jamii dhidi ya mahasidi. Kwa hivyo, ubabedume ulichangia kuelewa kwa mtoto wa kiume kuhusu namna anavyofaa kutenda ili kukubalika kama mwanaume katika jamii. Maudhui ya ukakamavu yanajitokeza kupitia Wimbo 17 kama ifuatavyo;

Wimbo 17: **Mama Yangaya**

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
| --- | --- |
| *Mama yangaya ×2* | mama alinikataza |
| *Mama yangaya khale* | mama alinikataza kitambo |
| *Mama yangaya khale* | mama alinikataza kitambo |
| *Mama yangaya khale makhuba* | mama alinikataza kitambo mambo |
| *Ka vakhali vavili* | ya kuoa wake wawili |
| *Nuhila vakhali vavili ukona manya shihuvi* | ukioa wake wawili utalala kama mwizi |
| *Mbukono.* | Kwa malazi |
| *Mama yangaya khale ×2* | mama alinikataza kitambo |
| *Yangaya khale makhuva ka vakhali vavili ×2* | alinikataza mambo ya kuoa wake wawili |
| *Nuhila vavili ukona ninzala munda* | ukioa wawili utalala na njaa |
| *Inzi nakaya mama natushitwa khuva ichirishi yi koroo* | mimi nimelelewa kuwa fahali mkuu |
| *ni nonda koko vasatsa vashianje valandola mutsiku wavo.* | nikifuata ushauri wako wanaume wenza wataniona kama adui wao |

Mwimbaji katika wimbo wa 17 anamsawiri mwanamume kuwa na uwezo na nguvu ya kuwaoa wake wawili licha ya ushauri anaopewa na mama yake. Mwimbaji anaonyesha nafasi ya mwanamume huyu katika kukaidi kufuata ushauri wa mama yake mzazi ili asije kuonekana adui wa wanaume wenzao. Hii ndio sababu anaonelea kutenda kulingana na mila za Waidakho na kushikilia msimamo wake. Mwimbaji pia anaonyesha kuwa maandalizi ya kuboresha nguvu na ukakamavu wa mwanamume huanza akiwa mtoto ambapo kulingana na utamaduni wa jamii ya Waidakho, wao hupewa chakula kingi haswa ugali na uji wakiwa wachanga ili wanapokua wawe na nguvu za kukabiliana na changamoto maishani na kushiriki vita vya jamii.

Aidha, mwimbaji anamrejelea mwanamume kamili katika jamii ya Idakho kama *ichirishi* kumaaanisha fahali kutokana na uwezo wake wa kuoa wake zaidi ya wawili kama vile mwimbaji anavyoimba. Katika wimbo huu mwanamume alipuuza ushauri wa mama yake kutokana na utamaduni kuwa ataonekana mnyonge, asiye na nguvu na asiye na uwezo. Mwanaume anayejulikana kama *Ichirishi* au fahali anachukuliwa kuwa mwanamume mwenye nguvu, mgumu na anayeoa wake wengi. Wanawake hawa walishirikiana huku wakijigamba kuwa *Navahila khu Ichirishi*, nimeolewa na fahali. Mtu anayejulikana kwa upendo kama fahali si tu kwamba anaogopwa bali pia anaheshimiwa.

Kulingana na msailiwa 4, wanasiasa wa Kiidakho wakiwania nafasi za uongozi hujitahidi kupata fahali au kitambulisho cha fahali yoyote ya kiume kama ishara yao ya kushirikishwa katika utamaduni wa Waidakho na kupata nafasi ya kuonekana kama wenye nguvu na uwezo. Mwanasiasa anayetambuliwa kama fahali hupewa heshima na kila mara hupewa fursa kuhutubia watu katika mkusanyiko wowote anaohudhuria kama ishara ya ukakamavu. Kulingana na Kabaji (2008), dhana ya ukakamavu inaibuka kutokana na mwanamume mgonjwa ambaye ana jukumu la kufanya mapenzi na mke wake hata kama ni mgonjwa ili kuthibitisha huo ugonjwa haujamfanya kiumbe dhaifu ila dhana ya ukakamavu imekuzwa.

### 5.2.6 Maudhui ya Ujasiri

Katika kujitahidi kufanya shughuli za kishujaa, mwanamume anafaa kuonyesha ujasiri licha ya kutofanikiwa au kukumbwa na changamoto. Matendo aliyotenda mwanamume

yalimpa sifa ya kuonekana kama tegemeo la jamii. Matendo haya yalikuzwa kutokana na tabia kubalifu jamii iliyomtarajia mtoto wa kiume kuyatenda. Mwanamume alishiriki vita na kuibuka mshindi, kuwaua wanyama wakubwa kama vile samba na kushiriki kazi ngumu za nyumbani kama vile kulima na kufuga mifugo. Haya yote yalikuzwa mapema kupitia mafunzo na kuiga baba yake au wanajamii shujaa katika jamii ya Waidakho alipokua. Jamii ya Waidakho inahimiza ujasiri kupitia wimbo 18

Wimbo 18 : **Vandu Varia**

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Ulwa ingwe ulwa isimba nihuma* | La kushangaza ukiskia sauti ya chui au simba |
| *Vandu vasatsa vechanyanga vandu varia* | Wanaume wanashangaa watu ni waoga |
| *Khali kuve vutukhu ama mbasu vandu varia* | Hata iwe usiku ama mchana watu ni waoga |
| *Musatsa nachingi shikong'o shie* | Mwanamume akibeba klabu yake |
| *Vandu varia* | Watu ni waoga |
| *Khali vasatsa valangwa mulihe* | Ata wanaume wakiitwa vita |
| *Vatsiku varia* | Maadui wanaogopa |

Kulingana na Wimbo 18, mwimbaji anaibua nafasi ya mwanamume kama mlinzi na wa kutegemewa katika hafla za usalama. Mwimbaji anatoa picha ya wanamume ambao wanawadharau wanaume wenzao na kuwasuta kutokana na uoga walio nao kwa simba na chui. Kulingana na Mutulu (2014), mwanamume akiwa mtoto hadi kuwa mtu mzima katika jamii ya Waidakho alitarajiwa awe jasiri ili atambuliwe kuwa mwanamume kamili. Kuthibitisha uume wake alipaswa kuwawinda wanyama hatari kama chui na simba. Pasipo tendo hili alitengwa na kuchukuliwa kama mwoga na kulinganishwa na mwanamke na hivyo kudharauliwa na kutoogopwa. Wanaume kama hao wanahesabiwa miongoni mwa watu waoga kama vile mwimbaji anavyotaja. Kulingana na msailiwa 3 (keshatajwa), ujasiri wa mwanamume ulitokana na mtihani aliopewa wa kumuua simba au chui msituni. Kwa hivyo maudhui ya ujasiri yanatokana na maamuzi aliyo nayo mwanamume katika kukabiliana na adui wake.

### 5.2.7 Maudhui ya Bidii na Kazi

Mudhui ya bidii na kazi yanaashiria ubabedume kama njia bora za mwanamume kutetea nafasi yake katika kutambuliwa kama mwanamume kamili. Mwanamume ambaye ameshikilia mila na desturi za ubabedume na kutambuliwa kama mwanamume amepiga hatua kubwa katika kujikomboa na kukomboa familia yake. Hatua za mwanamume wa

aina hii zimetokana na bidii anayofanya katika kutekeleza majukumu ya kishujaa na kuwajibika katika kuikimu familia yake. Mwanamume anaonyesha maudhui ya bidii na kama kama inavyojitokeza katika wimbo 19.

Wimbo 19 : **Wanaweza**

Tafsiri

Wanaume,
Wanaweza
Wanawezaa
Hata kama itachukuwa muda
Wanaume tunaweza.
Hata kwa dhiki,
Tunaweza ×2 hata kama itachukuwa muda
Wanaume tunaweza.

Mwimbaji katika wimbo wa 19, anaonyesha jinsi wanaume wanavyojigamba jinsi walivyo na uwezo wa kutenda. Kulingana na mwimbaji, mwanaume halisi anafaa kuwa mvumilivu na kutia bidii bila kushinikizwa na changamoto alizo nazo. Mwimbaji anadhihirisha picha ya wanaume kutokana na juhudi walizo nazo katika kupigana na janga la njaa na dhiki. Wanaume hawa wanajitolea na kufanya kazi kwa bidii ili wasije wakaonekana wanyonge katika kutekeleza majukumu yao.

Maudhui ya bidii na kazi katika wimbo huu yanaashiria ubabedume na njia bora za mwanamume kutetea nafasi yake katika kutambuliwa kama mwanamume kamili. Aidha, maudhui ya kazi yanajitokeza katika wimbo 19 ufuatao kuonyesha juhudi alizo nazo mwanaume katika kudumisha ubabedume na mwenye kuwajibika katika kuikimu familia yake na kuboresha hali yake ya mapato.

Kielelezo 20: **Mbele khu luchendo**

| **Asilia** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Mbele khu luchendo nzitsanga ×3* | niko safarini naja |
| *Hambi vosi khukhonyane luchendo* | mwanaume wote njooni tusaidiane |
| *Vashiele veru vakhusuvila* | wake zetu wanatutegemea |
| *Khuluchendo* | kwa safari |
| *Hambi vosi khukhonyane luchendo* | njooni wote tusaidiane safari. |

Mwimbaji katika wimbo 20 anaonyesha jitihada alizo nazo mwanamume katika kutafuta riziki ili atosheleze mahitaji ya familia yake. Mwimbaji anaonyesha furaha aliyo nayo mwanamume baada ya kufaulu kuzimbua riziki yake.

Aidha, mwimbaji anamsawiri mwanamume katika nafasi ya kuwashurutisha wanaume wenzake waungane pamoja katika kutafuta riziki. Mwanamume anajitahidi licha ya changamoto anazopitia katika kufanikisha mahitaji ya jamii, ana matumaini ya kuwa inawezekana. Mwanamume katika jamii ya Waidakho ni yule anatazamia mafanikio katika kuwajibika kulinda boma lake, kujenga boma lake na kuhakikisha familia yake imepata chakula cha kutosha.

Katika wimbo 20, maudhui ya uongozi inadhihirika kutokana na kauli kwamba katika mahitaji ya jamii mwanamume ni tegemeo. Wanaume katika jamii ya Waidakho walihakikisha kwamba jamii inalindwa kutokana na maadui. Sifa hii ya kuwa watu wa kutegemewa walipewa hadhi ya kuongoza jamii, kushiriki katika vikao vya kusuluhisha migogoro katika jamii na kutoa ushauri nasaha kwa jamii wakati jamii inakumbwa na mambo tata.

**5.3 Hitimisho**

Uchunguzi wa suala la ubabedume katika nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za upiganishaji fahali umebainisha kuwa maudhui ya ubabedume yanapatikana katika sherehe za upiganishaji fahali. Maudhui haya yamesaidia katika kudhihirisha na kuweka wazi nafasi ya mwanamume inayojitokeza katika sherehe za upiganishaji fahali. Kutokana na uhakiki wa nyimbo hizi, usawiri wa mwanamume katika sherehe za upiganishaji fahali umedhihirika.

Uchanganuzi wa madhui ya ubabedume katika nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za upiganisaji fahali unatusaidia katika kuelewa mielekeo na matarajio ya Waidakho kuhusu nafasi ya mwanamume na mahitaji ya mwanamume katika jamii ya Waidakho. Mtazamo na mielekeo ya kitamaduni ya Waidakho kuhusu dhana ya ubabedume imebainika bayana. Maudhui yanayojitokeza katika sherehe za upiganisaji fahali zinaweka wazi nafasi na wajibu wa mwanamume katika jamii ya Waidakho.

## SURA YA SITA

## ISHARA ZA KIUNA KATIKA SHEREHE ZA UPIGANISHAJI FAHALI KATIKA JAMII YA WAIDAKHO

### 6.1 Utangulizi

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza  ishara za kiuana katika sherehe za upiganishaji fahali ili kufichua vipengele vyake vya wazi na vya siri vinavyoelekeza kwenye matamanio ya kiume yaliyofichika, maadili na matarajio ya Waidakho kuhusu mtoto wa kiume. Mtafiti aliongozwa na nadharia ya semiotiki katika kufafanua miktadha ya uamilifu wa nyimbo na dhana zinazohusiana na sherehe za upiganishaji fahali. Utafiti huu unaonyesha mabadiliko katika mwelekeo na kujadili taswira na ishara za uanaume katika sherehe za upiganishaji fahali katika jamii ya  Waidakho Magharibi mwa Kenya. Utafiti huu zaidi unaelekeza uchunguzi katika ujenzi wa ishara za kiume ambazo zinafafanua viwango vya uanaume katika jamii ya Waidakho kama ifuatavyo;

### 6.2 Fahali

#### 6.2.1 Fahali kama Mwanamume Shujaa

Wanaume katika jamii ya Waidakho hujitambulisha na ng'ombe, ambayo hufafanua hisia zao za uume. Fahali ni kiasi kikubwa mfano wa mwanaume. Mwanaume anayejulikana kama *Ijirichi* au fahali anachukuliwa kuwa mwanamume mwenye nguvu, mgumu na anayevutia wanawake. Wanawake wengi hujigamba kuwa: *Ndavahira ku Ijirichi*, nimeolewa na fahali.



Picha 1: Picha ya fahali kwa jina Aguero

Picha ya 1 inaonyesha fahali maarufu kwa jina Aguero. Jina hili ni la mchezaji maarufu anayejulikana kote ulimwenguni kutokana na uwezo wake wa kucheza mpira wa kandanda. Kulingana na utamaduni wa jamii ya Waidakho,mtu anayemiliki sifa ya fahali Aguero huwa maarufu na hufanya vitendo vya kiajabu ili kukuza umaarufu wake.

Aidha, kulingana na msailiwa 1, baadhi ya wanasiasa Waidakho kama vile Bony Khalwale wakiwa kwenye bunge la kitaifa hujigamba mbele ya wenzake wakijidai kuwa *ninzi ichirishi yi ikolomani mwana mwidakho* yaani mimi ni fahali wa Ikolomani kutoka Idakho. Baada ya mtafiti kulinganisha sifa za wanasiasa hawa na fahali Aguero, mtafiti aliainisha ukweli kwamba wanasiasa hawa hujitolea bila uoga katika kutetea na kupigania maslahi ya wanaichi kutoka sehemu za Ikolomani kama njia ya kuboresha ubabedume dhidi ya viongozi wenzao.

Mtafiti alitangamana na wanajamii kuhusu fasiri ya jina fahali na wanamume Waidakho ambapo watafitiwa walitoa kauli '*fahali hufa na majani mdomoni.'* Fasili hii ilirejelea mwanamume mgonjwa katika jamii ya Waidakho akikaribia kifo. Kauli hii ilifafanuliwa na mmoja wa wasailiwa kuwa, mwanamume mgonjwa anafaa kufanya mapenzi na mke wake hata kama ni mgonjwa ili kuthibitisha huo ugonjwa haujamdhoofisha na kumfanya kiasi cha kuwa mwanamke. Majani mdomoni inarejelea mke aliyeoa ambaye anauwezo wa kuwazaa watoto na kuendeleza ukoo wa jamii yake. Ilibainika kuwa juhudi za kuthibitisha iwapo tendo hilo lilitekelezwa na mgonjwa, mkewe aliuzwa swali hili kwa njia fiche ili libaki kuwa fumbo kwa wanajamii wengine: '*je fahali aliuonja uji?*.' Uji katika muktadha huu ni neno la kiishara kurejelea kushiriki ngono. Mwanaume hafai kuonyesha udhaifu katika kushiriki mapenzi ila kujizatiti katika hali yake dhaifu kama njia ya kukuza na kuhimiza ubabedume katika wanajamii .

Kutokana na mahojiano kati ya mtafiti na wasailiwa katika jamii ya Waidakho, ilibainika kuwa, mapigano ya fahali hufanywa kwa sababu mbili: kusherehekea maisha ya shujaa na kwa burudani. Ingawa mkazo katika utafiti huu ni kipengele cha burudani, mapigano ya fahali wakati mwingine hupangwa katika sherehe inayojulikana kama *shilemba*, ambayo inaadhimisha maisha ya shujaa siku ya mazishi yake (Kabaji 2008). Hata hivyo, mtafiti mtafiti aligundua mwanamume kupewa sifa ya kuwa shujaa katika

jamii ya Waidakho anayestahili ibada ya *shilemba*, lazima mwanamume awe amepigana vita na kuua mwanamume mwenzake katika hali ya vita.

Kwa mujibu wa msailiwa 2 (keshatajwa), mwanaume katika muktadha wa Kiidakho ni mtu mzima aliyetahiriwa. Kumdhulumu mwanamke au mtoto ambaye hajatahiriwa si kuchukuliwa kama kitendo cha kishujaa. Wakati wa vita katika ardhi ya jadi ya Waidakho, hili lilikuwa tendo lisilo la kiume bali la uoga. Ilikuwa ni kitendo cha kijinga kilichohusishwa na wanaume wenye shida ya kiakili. Wakati wa *miviga ya shilemba*, mafahali hupigana kando ya kaburi na kueneza udongo kutoka kaburini kote kwenye kiwanja. Kimsingi, hii ni kuashiria kuwa roho ya shujaa inapambana na roho za watu aliowaua ili kuingia ulimwengu wa mababu (Mutulu, 2014). Ni nguvu hizi zinazomilikiwa na fahali ndizo wanaume wa Waidakho wanatamani kumiliki.

### 6.2.2 Fahali kama Ishara ya Utajiri

Kwa mujibu wa Travel (2020), uhusiano wa wanaume na fahali unaonekana katika harakati za kumlisha fahali na anavyotunzwa. Utafiti ulibainika kuwa wanaume wa Kiluhya wanamchukulia fahali kama rafiki yao na wao hutenga muda kuangalia fahali wao wakila. Hata katika nyakati za kisasa wakati ukubwa wa ardhi unapungua, ilibainika kuwa katika jamii ya Waidakho, nyumba nyingi zilizo na ardhi chini ya ekari moja zina angalau fahali aliyefungiwa nyumba. Waidakho wanaamini kuwa kumiliki fahali ni ishara ya utajiri . Ndoa ya Waidakho huhalilishwa kwa malipo ya ng'ombe kwa njia ya mahari. Wengi ambao mtafiti aliwahoji walikiri kuwa hawana vyeti vya ndoa na hawahitaji kwa sababu mali ya fahali ililipwa. Wanaidakho walijivunia kulipa idadi iliyoamuliwa na wazee kutoka upande wa mke kama ishara ya cheti cha ndoa kuliko maandishi kwenye kipande cha karatasi.

Kwa mujibu wa Kabaji (Keshatajwa), idadi ya ng'ombe kulipwa kama mahari huamiliwa mapema kabla ya mwanamume kuoa. Ng'ombe kumi na tatu waliandikiwa bikira lakini mwanamke aliye na mtoto nje ya ndoa hakudhaminiwa bali alihusishwa na idadi ndogo ya ngombe na fahali. Sharti hili la ubikira hata hivyo halitumiki kwa wanaume kwa kipimo sawa. Mwanaume mwenye mtoto nje ya ndoa alisifiwa vyema kuwa fahali 'aliyeanza mapema'. Kati ya yote mahari iliyolipwa ya mwisho ilikuwa

fahali. Fahali huyu aliashiria sala kwa mwanamke kuzalisha watoto wa kiume ambao wataendeleza mila na desturi za jamii .

### 6.3 Kifaa cha Isukuti

Kwa mujibu wa Ellis na McClinton (1990), anaeleza kuwa nadharia ya Semiotiki hujikita zaidi kwenye fasili ya ujumbe kuliko vile mchakato wa uwasilishaji wa ujumbe huo hufanyika. Aidha, vifaa vya isukuti vilitumika kama vifaa vilivyofinyangwa kuzua ujumbe ulio na ishara zilizobeba ujumbe kwa wanajamii Waidakho. Hata hivyo, Barthes (1994) alishikilia kuwa ishara hizi huchambuliwa kwa kuangazia misimbo ambapo uchambuzi wa vifaa vya utafiti vilichambuliwa kwa kuangazia msimbo wa ki-ishara katika kubaini maana mbalimbali baada ya kufumbua ishara katika vifaa vya isukuti vinavyotumika katika sherehe za upiganishaji fahali.

Mtafiti aligundua kuwa ngoma ya Isukuti ni kifaa cha kitamaduni katika jamii ya Waidakho katika kusherehekea sherehe mbalimbali ikiwemo sherehe za upiganishaji fahali. Inachukua umbo la ngoma ya kasi (isukuti mutiti), yenye nguvu (isukuti papa) na ya shauku (isukuti mama) inayoambatana na uimbaji. Kifaa hiki huwa na dhima kubwa sana katika kufanikisha sherehe ya upiganishaji kwa kuwaburudisha mashabiki na kumtia fahali nguvu anapoenda kwenye mashindano. Picha 2 ifuatayo inaonyesha miundo mbali mbali ya isukuti.



Picha 2: Ngoma za Isukuti

Kulingana na Ellis na McClintock (1990), ishara ambazo hujitokeza katika maisha ya binadamu huundwa na binadamu mwenyewe azitumie katika kurahisisha mawasiliano yake. Kifaa cha isukuti kinapata maana katika jamii ya Waidakho kulingana na msimbo

wa Ki-ishara kama anavyoeleza Bathes (1994) kwa kuzifumbua ishara hizo katika kutazama kifaa cha isukuti kama kinavyotumika katika sherehe ya upiganishaji fahali. Katika jamii ya Waidakho, isukuti hugawika katika aina tatu, *isukuti mutiti, isukuti mama na isukuti papa.*

*Isukuti papa* huwa kubwa kwa zote. Kifaa hiki kupigwa baada ya muda ili kunogesha ngoma hii. Ngoma hii husikika kwa umbali na nguvu zaidi. Ngoma hii inatafsiriwa kimuktadha katika jamii ya Waidakho kurejelea nafasi ya wanaume katika jamii. Wanaume katika jamii ya Waidakho hushirikishwa katika masuala tata ambayo huenda yamekuwa tatizo katika familia. Mara nyingi mwanamume hushirikishwa na majukumu yenye maana na tata yanayohusisha migogoro katika jamii ili kuhakikisha kuwa amani imedumishwa, familia imelindwa kutokana na maadui, kuhakikisha kuwa amekidhi mahitaji ya jamii na kuwa mshauri mwema katika masuala yanayoibuka katika jamii. Nafasi hizi zinampa sifa ya uanaume.

Mtafiti alishuhudia kuwa, *Isukuti mama* ni ya pili kwa ukubwa. Ngoma hii kulingana na miviga aliyoshuhudia mtafiti, alibaini kuwa ngoma hii hutoa sauti ya kuvutia. Ngoma hii hata hivyo mdundo wake haukubadilika licha ya kuimbwa kwa wimbo tofauti. Ili kuzua mvuto huu ngoma hii hupigwa kwa ustadi na kwa sauti ili kuwafanya mashabiki kuvutiwa zaidi. Hata hivyo, aina hii ya ngoma kulingana na fasili ya Waidakho baada ya kumsaili msaili 2 ambaye alieleza kuwa, ngoma hii inamwashiria mwanamke katika familia ambaye anafanya majukumu mengi kama vile kuandalia mumewe na watoto chakula, kutunza mifugo, kufanya usafi wa nyumba pamoja na kuwatunza watoto. Mwanamke katika jamii hii kulingana na fasili hii atajitahidi ili kujenga boma lake na kulifanya livutie kama ilivyo ngoma hii ya isukuti mama ambayo husababisha midundo ya kuwavutia wasikilizaji.

Sawia na *isukuti mama*, *isukuti mutiti* kulingana na msailiwa 3, ngoma hizi hupigwa kila mara bila kupumzishwa kwa nguvu zaidi ili zisikike kwa umbali. Kifaa hiki huashiria nafasi ya watoto katika familia ambao huwa wasaidizi wa mama na kumsaidia kutekeleza majukumu ya nyumbani. Watoto katika jamii wanapaswa kuwasaidia wazazi katika kutekeleza kazi za nyumbani kama kuwalisha mifugo, kuteka maji, kupika chakula na kusafisha boma. Hata hivyo, kazi za nyumbani zilitekelezwa

kulingana na jinsia ya mtoto. Watoto wa kiume walipata mafunzo ya kutekeleza kazi zinazohusiana na wanaume. Wanaume katika jamii ya Waidakho walifaa kuwaelekeza watoto na wake zao na kuwapa ushauri walipotenda kinyume. Hii ndiyo sababu *isukuti papa* ilipigwa mara moja moja baada ya kupigwa kwa *isukuti mama na mutiti.* Kwa hivyo, mwanamke ni mfanyakazi na mtumwa wa mwanamume ambapo anapata sifa ya uanaume na kuonekana bora zaidi kuliko mwanamke.

### 6.4 Mapambano ya Fahali

Mtafiti alishuhudia umati wa wanaume wengi wakimiminika kwenye ukumbi wa kupiganisha fahali wakicheza ngoma ya isukuti wakiwa wamebeba vilabu vyao. Baada ya kufikisha fahali wao kwenye ukumbi kila mwenye fahali alionekana akimsihi fahali wake 'afunguke' kama alivyosema mmoja wa wasailiwa katika ukumbi huo kumaanisha kukojoa. Fahali akionyesha ishara ya kukojoa huashiria kuwa yuko tayari kwa vita. Mara nyingi utawasikia mashabiki wakisema kuwa fahali wao amekubali changamoto. Waidakho pia huchukulia tukio hili likiwa la maana katika matukio mbalimbali haswa katika sherehe ya kulipa mahari. Kwa hivyo, katika miviga ya kulipa mahari, fahali anapopelekwa nyumbani kwa bibi arusi, ni sharti fahali akojoe ili sherehe ianze.

Kulingana na tafsiri ya Waidakho, kukojoa kwa fahali ni ishara kwamba bibi arusi atakuwa na uwezo wa kuzaa watoto wa kiume. Ni baada ya fahali kutekeleza tendo hili la kukojoa ndiposa mmiliki wake anaweza kuihimiza kusonga mbele na kupigana. Katika kipindi hicho cha mapambano , fahali hukoroma, wakizungusha vichwa vyao kutoka upande hadi upande na kuchimba kwato zao chini. Wakati huo, wamiliki wa mafahali bila kuchoka huendelea kuwasifu kwa kuwakumbusha ushindi uliopita.

### 6.5 Majina ya Fahali

Katika jamii ya Waidakho fahali ni kama wakala wa wanadamu. Wao ni zaidi ya binadamu kwa kupewa majina yanayoelezea sifa zao bora au angalau matarajio ya wamiliki wao. Kila fahali anayepigana katika jamii ya Waidakho ana jina lake. Majina yaliyotolewa yamedhamiriwa na sifa za fahali, matarajio ya mmiliki, hali ya kuzaliwa kwake au kwa heshima kwa fahali aliyeshinda vita vingi. Huu mtindo wa kuwapa fahali

majina pia hutumika katika kuwataja watoto miongoni mwa Waidakho. Baadhi ya majina mtafiti alikumbana nayo ni kama yafuatayo;

### 6.5.1 Spana

Kimsingi ni kifaa cha kufungulia nati. Kifaa hiki kina uwezo wa kufanya majukumu mengi. Katika jamii ya waidakho, fahali anayeitwa spana ni shujaa na mkakamavu. Fahali shujaa na mkakamavu ni yule hujitahidi na kupigana na mashindano zaidi ya mmoja. Mtafiti alishuhudia vita vya fahali kwa jina Spana ambaye alishiriki vita zaidi ya moja kwa siku moja. Fahali huyu licha ya majeraha alivumilia hali ngumu ya kudungwa na pembe za washindani wake ila aliepuka mshindi. Hata hivyo, kwa kuwa mila na desturi huongoza fikra na mielekeo ya wanajamii, wanajamii walihusisha sifa ya fahali Spana kama shujaa na mkakamavu kurejelea wanaume waliojitolea katika kutekeleza kazi ngumu na shughuli nyingi ili kuhakikisha maendeleo ya jamii yao ya Waidakho.

### 6.5.2 Osama

Kihistoria, Osama ni jina la shujaa aliyewahi kuwa gaidi na tishio katika ulimwengu. Osama alikuwa mtu mwenye nguvu aliyetishia na kuathiri nchi za Africa kimaendeleo. Utafiti ulibaini kuwa Jamii ya Waidakho imeiga matumizi ya jina hili na kuwarejelea fahali kutokana na uwezo wake wa kuwa na nguvu na kuwa katili kwa fahali wenzao. Kulingana na msailiwa 1, mwanamume aliyekuwa na nguvu na uwezo katika jamii ya Waidakho analinganishwa na jina hili kutokana na wajibu wake katika kutekeleza matendo ya kishujaa. Mtu aliyekuwa na maumbile ya ushujaa aliogopwa na kusifiwa katika matendo yake. Kama ilivyo kwenye desturi na mila za waluhya wanaume wenye sifa za kishujaa na waliorejelewa kwa jina Osama walipewa nafasi ya kuwa viongozi katika masuala ya kivita, maamuzi katika familia na jamii sawia na kutoa ushauri ulio nasaha.

### 6.5.3 Aguero

Katika sekta ya michezo ulimwenguni, Aguero ni jina la mchezaji sugu ambaye anajulikana kwa umaarufu wake wa kucheza mpira. Mchezaji huyu ana tajriba ya kucheza vizuri na kujulikana kwa kufunga mabao mengi katika mashindano ya ulimwenguni. Kutokana na umaarufu alio nao mchezaji huyu, jami ya Waidakho iliiga

jina hili kurejelea ushupavu wa fahali na umaarufu wake. Sifa ya ubabedume katika jamii ya Waidakho inatokana na umaarufu mwanaume alio nao dhidi ya wanaume wenzake na nafasi yake katika jamii katika kutekeleza suala la ubabedume. Kwa mujibu wa msailiwa 2 (keshatajwa), umaarufu wa mwanamume hudhihirika kutokana na vitendo vya kishujaa ambavyo amevifanya na vinavyompa nafasi bora kuliko wanaume wenzake. Tendo la kishujaa lilifafanuliwa kama uwezo wa kufanya matendo ya kishujaa ambavyo vilionekana vipya na vinavyojitokeza kwa njia ya miujiza katika jamii.

### 6.5.4 Tinga

Kifaa kinachoitwa tinga huwa na nguvu zaidi kutokana na uwezo wa kubeba vitu vizito. Kinara wa chama cha ODM hurejelewa tinga. Kumaanisha kuwa ana uwezo wa kutenda mambo makuu ya kishujaa bila uoga. Utafiti ulihusisha jina hili Tinga na fahali anayerejelewa kwa jina hili kuwa mwenye nguvu wa kupigana na fahali wakubwa wanaomshinda kimaumbile. Licha ya tofauti hizi za kimaumbile, mtafiti alishuhudia fahali huyu akiwa mshindi baada ya kustahimili mashindano kwa takriban dakika ishirini. Kwa Mujibu wa mila na desturi za Waidakho, mwanamume kamili alifaa ajihusishe katika shughuli ngumu kama vile kulima, kuwinda wanyama wakubwa na kulinda jamii dhidi ya hatari. Haya yote yalitekelezwa bila kulalamika kama anavyopigana Tinga mashindano mengi bila kufa moyo. Wanaume hawa ni sharti wakule kiapo katika matendo yao. Watoto wa kiume katika jamii ya Waidakho walipewa mafunzo ya jinsi ya kuwa jasiri. Kulingana na msailiwa 2, ujasiri wa mwanamume ulipimwa kutokana na uwezo wake wa kumuua simba kwenye msitu. Vijana walitarajiwa kujiandaa kuwa viongozi jasiri ambao wangelinda jamii kutokana na maadui.

### 6.5.5 Master Key

Master key ni ufunguo unaoweza ukatumika kufungulia kufuli nyingi tofauti. Kwa hivyo fahali kwa jina hili inarejelea fahali shujaa na mwenye majukumu mengi; kwa maana ya kupigana vita zaidi ya moja. Mtafiti alishuhudia fahali kwa jina Master key ambaye anaujuzi wa kuwashinda fahali wengine katika mashindano bila kutumia nguvu nyingi. Fahali kwa jina Master key huhusishwa katika mashindano mengi ili aridhike. Kulingana na nadharia ya ubabedume, wanaume ambao hufuata itikadi na utamaduni

wa ubabedume na kujitambulisha kama wanaume huonyesha ufanisi mkubwa wa kibinafsi. Kauli hii ina maana kuwa wanaume hawa hudhihirisha fikra na mawazo ya kiume na huonekana kama wenye bidii katika kutenda kazi zao kikamilifu. Mtafiti hata hivyo alibaini kuwa mwanamume hujishughulisha na kujenga boma lake, kutafuta riziki kuikimu familia yake, kuhusika katika maamuzi ya jamii na kulinda familia yake dhidi ya maadui.

**6.6 Maandalizi ya mapambano ya fahali**

Mapambano ya fahali ni muktadha wa uamilifu katika sherehe za upiganishaji fahali unaolenga kuelezea mahusiano ya mwanamume kutokana na desturi na imani ambao hutamalaki katika mfumo mzima wa jamii ya Waidakho. Kwa mujibu wa Jakinda (keshatajwa), mapambano ya fahali kulingana na jamii ya Waidakho ni shughuli ya wale walio na korodani, na inahusisha kujigamba kwa mwanamume katika jaribio la kumshinda na kumtiisha mpinzani wake. Pambano hili linahitaji maandalizi ya kina. Ingawa vita vienyewe vinaweza kuchukua muda mfupi kama dakika tano, muundo wa matukio hupangwa kwa kina kuelezea mtazamo wa kijinsia katika jamii ya Waidakho. Hali ya kimwili na kisaikolojia ya fahali ni ya nje ingawa imeidhinishwa kitamaduni.

Utafiti ulibainika kuwa fahali  aliyefugwa haswa kwa kupigana huishi maisha ya kutengwa na ng'ombe wengine katika boma katika maisha yake yote ya mapigano. Kutengwa huku kuna maana kwa mmiliki wa fahali kwa kushirikiana na fahali wake ili kuwa na makali dhidi ya mafahali wengine. Aidha, kwa mujibu wa msailiwa 2 (keshatajwa), kutengwa kwa fahali kunaepusha kuwepo na ushindani wa chakula na wanyama wasio na thamani. Hali hii ya kutengwa ilifasiliwa kuwa ni ishara kamili ya fasili ya mwanamume hasili Mwidakho. Mtafiti katika mahusiano yake na wanajamii katika jamii ya Waidakho aligundua kuwa mwanaume hajitahidi kupata chakula. Anakula peke yake wakati mke wake anakula pamoja na watoto. Hata hivyo, mtafiti alijikita zaidi kuchunguza ni kwa nini mwanaume ajitenge na familia yake wakati wanapokula chakula kwa kurejelea viashiria vya utamaduni wa waidakho ambapo aligundua kuwa fasili  hii inasadikisha  kumtazama  fahali kama aina ya mtu mbadala ambapo aking'ang'ania chakula hatakula chakula kingi ambacho kitampa nguvu na uwezo wa kufanya kazi ngumu za kishujaa katika jamii .

Msailiwa 3 (keshatajwa) aliibua fasili nyingine kuhusu fahali kama ishara kuwa katika jamii ya Waidakho, fahali aliyetengewa kupigana hafai kuhusishwa katika harakati za kusababisha ujauzito  kwa ng’ombe wa kike. Utafiti ulihusisha kutambua maana inayojitokeza kutokana na imani hii kwa kuchunguza uhusiano uliopo kati ya kutengwa kwa fahali katika kuwapa ujauzito ng’ombe wa kike ilifasiliwa kwa kutumia msimbo wa kiurejelezi katika kuchambua kiashiria hiki kwa kuangazia muktadha wa utamaduni wa waidakho. Mtafiti aliongozwa na mila na desturi za Wadakho kuwa fahali huepushwa kusababisha ujauzito kwa kuwa hali itampunguza uwezo na nguvu zake za kupigana. Ni imani iliyozoeleka miongoni mwa Waidakho kwamba mtu anapojitayarisha kwa aina yoyote ya mashindano, anapaswa kujiepusha na ngono.

Hata hivyo, hakuna kitu kinachoonyesha hali ya vurugu ya mchezo huu kama kitendo cha kunoa  pembe za fahali siku tatu kabla ya siku ya shindano kama anavyoeleza Kabaji (keshatajwa). Mmiliki anafanya zoezi hili anapozungumza na fahali katika lugha ya Kiidakho ya kejeli inayoendelea kwa muda mrefu.  Utafiti uligundua kuwa wamiliki wa fahali ni sharti wanoe pembe za fahali kuashiria wema wa mwanamume ulioongozwa na kutosheleza tamaa za ngono. Ilibainika kuwa kunolewa kwa pembe ni ishara ya kumtayarisha mwanamume katika uume wake sawia na jinsi fahali hufanyiwa maandalizi ya kujikinga na mbinu bora ya kushinda mapambano. Ishara ya  kunolewa pembe wanamume mwidakho  kupitia mila ya tohara ambayo ni ya maana kwa kumfanya mwanaume awe mwenye nguvu na hatari. Mchezo wa kupiganishaji fahali ni ishara  inayokusudiwa kuonyesha wanaume wawili ambao wanakumbwa na changamoto maishani na katika changamoto hizi za maishani ni sharti mwanamume mmoja aonyeshe uanaume wake dhidi ya mwingine.

**6.7 Ishara katika Nyimbo**

Kulingana Ellis na McClintock (1990), wafuasi wa nadharia ya semiotiki hujikita zaidi kwenye fasili ya ujumbe kuliko vile mchakato wa uwasilishaji wa ujumbe huu hufanyika. Hata hivyo, sifa mbalimbali za mhusika fulani zinawezaelezwa kwa kutumia viashiria mbalimbali ili kusimbua ujumbe unaokusudiwa. Jamii nyingi hutumia nyimbo kimafumbo katika kupitisha ujumbe kwa wanajamii. Aidha, sifa za mwanamume au mwanamke huelezwa kutokana na mazingira aliomo. Nyimbo hizi hupata maana

kutokana na muktadha aliomo mwimbaji na msikilizaji. Ishara hii imejitokeza katika Kielelezo 21 kama ifuatavyo;

Kielelezo 21

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Khanyonyi ni khalayi* | ndege ni mzuri |
| *Khamela mavaha×2* | amemea mabawa ×2 |
| *Khalitsanga viavene* | anakula za wenyewe |
| *Khanyonyi ni khalayi* | ndege ni mzuri |
| *Khuvayanga manyonyi manyishi ko!* | Ndege wengi wamefugwa |
| *Khu khulangwe vandu vasatsa* | ili tuitwe wanaume |

Kielelezo 22

*Nilikhunyola khu khanyonyi khanje nilikhusena ×2*
Nikikupata kwa ka ndege kangu nitakukanyaga ×2
*Nilikhunyola khu khanyonyi khanje nilikhusena watuvukha*
Nikikupata kwa ka ndege kangu nitakukanyaga ubondeke

Kulingana na Kielelezo cha 22, mwimbaji anarejelea *khanyonyi* kumaanisha kidege katika hali ya umoja kuonyesha hali ya kudunisha. Mwimbaji anamwaashiria mwanamke kama ndege. Ndege ni mnyama msafi anayejipenda na hupepea angani. Mwanamke anafananishwa kama kiumbe safi na mrembo ambaye huwa na misafara ya kila wakati. Kama anavyoeleza msailiwa 2 (keshatajwa) , *Soko ya Sejeri* katika eneo la Ikolomani, wanawake walichukuwa nafasi ya walitoka nyumbani kwao wakati wanaume wao walikuwa wameenda katika shughuli za kivita. Nafasi yao ilijikita katika kutekeleza majukumu waliyotenda wanaume wao ili kuikimu familia yao. Wengi walishindwa kustahimili hali ngumu ya maisha wakajiunga na ukahaba katika sehemu ya *Sejeri*. Kwa hivyo mwimbaji aliimba nyimbo kwenye miviga ya upiganishaji fahali kuwaonya wanaume waliogopa kushiriki vita kuhusiana na wake zao ila wajitahidi kuhusika katika shughuli za kukuza ubabedume miongoni mwao.

Mwimbaji anamsawiri mwanamume katika kielelezo 21 kama mwenye mapenzi katika kurembesha mke wake na kumtunza mke wake dhidi ya wanaume wengine. Katika kielelezo 21, mwimbaji anasema *khanyonyi ni khalayi khamela mavaha* kumaanisha ndege ni nzuri imemea mabawa. Mshororo huu unatafsiriwa katika jamii ya Waidakho kumaanisha kuwa mwanamume amefanya juhudi za kumtunza mke wake hadi amenenepa na kupendeza. Ila katika mshroro wa pili, mwimbaji anadhihirisha

ubabedume kwa kusema kuwa *Khuvayanga manyonyi manyishi khulangwe vandu vasatsa* yaani tunawafuga ndege wengi ili tuitwe wanaume kamili. Hii ni ishara kwamba mwanamume ni lazima aoe wake wengi ili aonekane mwanamke kamili. Mwanaume mwenye mke mmoja anasawiriwa kama mtu  mwoga na anayeogopa majukumu.

### 6.8 Klabu na pembe za Swara

#### 6.8.1 Klabu

Vifaa hivi hutumika katika sherehe za upiganishaji. Klabu huwa ni mti unaokatwa, huchongwa  na kisha  kukaushwa  kwa muda wa wiki mbili. Mti huu hufanyiwa kimila kwa kushirikisha madawa zinazotambuliwa katika jamii ya Waidakho. Kifaa hiki huwa cha maana kabla fahali kupelekwa kwenye ukumbi wa kupiganisha fahali. Kwa mujibu wa msailiwa 3 (keshatajwa),  Waidakho, fahali hupigwa na klabu kwenye uti wa mgongo kama njia moja ya kumpa ari ya kupigana na kumtakia mema katika mapambano.  Kwa mujibu wa picha 3, mashabiki katika sherehe za upiganishaji fahali hujivunia kifaa hiki kwa kukiinua juu wakati fahali hupigana kama ifuatavyo;



Picha 3: Klabu ambazo zimeinuliwa juu katika sherehe ya kupiganisha fahali

Kuinuliwa kwa kifaa hiki  kwa mujibu wa picha 3 wakati fahali wanapigana inaashiria mwanamume kamili ambaye ana nguvu za kiume za kustahimili ngono kwa muda mrefu. Mwanamume anafaa kumridhisha mke wake. Hii ndiyo sababu fahali kabla apelekwe kwenye mashindano ni lazima kifaa hiki kitumike kwa kumpiga fahali kwenye uti wa mgongo. Fahali huwa na ari ya kupigana kwa muda mrefu usiopungua dakika thelathini.

### 6.8.2 Pembe za swara

Pembe za swara ni kifaa ambacho kinapatikana baada ya mwanamume kuonyesha kuwa ana uwezo wa kuwinda. Sifa ya mwanamume kamili ni kuwa na uwezo wa kuwinda wanyama wakubwa walio hatari. Swara ni mnyama anayejulikana kwa uwezo wa kukimbia kwa muda mrefu. Kutokana na maumbile yake mnyama huyu huwa makini kujikinga dhidi ya maadui au mnyama wowote akimnyemelea kwa nia ya kumdhulu.



Picha 4: Picha hii inaonyesha kifaa kilichoundwa kutokana na pembe za swara ambacho hutumika kuwajulisha watu siku ya mapambano ya fahali.

#### 6.8.2.1 Mlio wa pembe za swara kuashiria siku ya mapambano

Kifaa hiki kiliundwa kutoka kwa mnyama huyu kutokana na sifa ya kuwa mkakamavu na mwepesi katika kutenda. Katika sherehe za upiganishaji fahali, pembe hizi za swara hupulizwa saa tisa asubuhi kuashiria kuwa ni siku ya kupiganisha fahali. Tendo hili huendelea hadi fahali wanapoanza mashindano. Katika fasili ya Waidakho inaashiria kuwa mwanamume kamili ikifika saa tisa uume wa mwanaume ni sharti usimame imara kuonyesha kuwa mwanamume huyo ako sawa na ana uwezo wa kumridhisha mke wake.

### 6.9 Hitimisho

Uchunguzi wa suala la uana katika sherehe hii umebainisha kuwa usawiri wa mwanamume kupitia nyimbo, dhana na vifaa unapatikana katika sherehe za upiganishaji fahali. Imebainika wazi kuwa masuala ya kijinsia katika jamii ya Waidakho yamejengwa katika suala la mahusiano ya mamlaka na utawala unaoamua nafasi ya wanawake. Utafiti huu umeonyesha mabadiliko katika mwelekeo na

kudhihirisha wazi taswira na ishara za uanaume katika sherehe za upiganishaji fahali katika jamii ya Waidakho Magharibi mwa Kenya. Ishara hizi husaidia katika kuwasilisha masuala fiche ya kitamaduni ya jamii ya Waidakho yanayopatikana katika sherehe za upiganishaji fahali kwa lengo la kuwaelimisha wanaume kuhusu itikadi za Waidakho. Kutokana na uhakiki wa ishara hizi, usawiri wa kijinsia katika sherehe za upiganishaji fahali umedhihirika. Uchanganuzi wa ishara za kiuana katika sherehe za upiganisaji fahali unatusaidia katika kuelewa mielekeo na matarajio ya Waidakho kuhusu nafasi ya mwanamke katika kumsawiri mwanamume na mahitaji ya mwanamume katika jamii ya Waidakho. Mtazamo na mielekeo ya kitamaduni ya Waidakho kuhusu dhana ya ubabedume imebainika bayana.

# SURA YA SABA

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

## 7.1 Muhtasari

Utafiti huu ulikuwa wa kuchunguza ubabedume katika sherehe za upiganishaji fahali katika jamii ya Waidakho. Dhima kuu ya kufanya utafiti huu ilikuwa kuchangia maandishi ya kitaaluma katika uwanja wa fasihi simulizi. Mtafiti alikusanya data ya utafiti huu nyanjani kutoka kwa kumbi za upiganishaji fahali ili kupata data ya kuchanganuliwa. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Ubabedume katika kuchambua mahusiano kati ya mwanamke na mwanamume na nadharia ya semiotiki ambapo ilimfaa mtafiti katikakuchambua miktadha za uamilifu katika sherehe za upiganishaji fahali katika jamii ya Waidakho.

Suala la ubabedume ni la kupigiwa mjadala kwa kuwa kila jamii huwa na mitazamo yake kulingana na utamaduni na itikadi zake kumhusu mwanamume. Utafiti huu uligundua kuwa sio kila mtoto wa kiume aliye wa jinsia ya kiume alipewa sifa ya uanaume. Mwanamume alipewa sifa ya uanaume kutokana na matendo aliyofanya. Mwanamume alishiriki vita na kuibuka mshindi, kuwaua wanyama wakubwa kamavile samba au chui na kushiriki kazi ngumu za nyumbani kama vile kulima na kufuga mifugo. Sifa hizi ziliweza kutambulika mapema kupitia kuiga baba yake au wanajamii shujaa katika jamii ya Waidakho wakati mtoto alipokuwa.

Kutokana na tafiti za mtafiti katika baadhi ya nyimbo na ishara mtafiti alikusanya, ilibainika kuwa mwanamume majukumu ya mwanamume yanaongozwa na mila na desturi za waidakho. Majukumu mengi yalitokana na uwezo na nguvu alizo nazo mwanamume katika kutenda mambo ya kishujaa. Ilibainika kutoka kwa wasailiwa kuwa watoto wa kiume waliiga matendo ya baba yao. Hata hivyo walitengewa chakula chao na baba yao kama walivyo fahali ili wawe na nguvu zaidi ya kupigana katika mashindano. Mwanamume ambaye alikulia chakula jikoni na wanawake aliiga sifa za wanawake sawia na fahali aliyekula na ngombe za kike. Fahali huyu alikuwa muoga na akikutana na fahali mwenzake katika mashindano hawezi stahimili mapigano.

Ubabedume hudhibitiwa na itikadi za kijamii ambazo huongoza mielekeo, fikra na mitazamo ambazo hufafanua majukumu sahihi ambyo mwanamume anastahili

kutimiza. Matendo aliyotenda mwanamume yalimpa sifa ya kuonekana kama tegemeo la jamii. Matendo haya yalikuzwa kutokana na tabia kubalifu jamii iliyomtarajia kwa mtoto wa kiume. Kwa mfano mtoto wa kiume hakupaswa kukaa jikoni chakula kikipikwa walifaa kukaa na baba yao wafunzwe mambo ya kishujaa na jinsi ya kuwa wanaume halisi. Pia mtoto wa kiume hakupaswa kuingia chumbani anapolala baba yake kwa vyovyote vile. Mwanamume asiyetenda vitendo hivyi alipewa adhabu kubwa ili awe mfano kwa wadogo wake.

Mtoto wa kiume ambaye ameshikilia mila na desturi za ubabedume na kutambuliwa kama mwanaume amepiga hatua kubwa katika kujikomboa na kukomboa jamii yake. Hatua za mwanamume wa aina hii zimetokana na bidii anayofanya katika kutekeleza majukumu ya kishujaa na kuwajibika katika kuikimu familia yake. Katika muktadha huu kulingana na jamii ya Waidakho, mtu aliyetambulika kama fahali alifanya kazi ngumu ambazo zikimshinda basi ni ishara kwamba hakuna mtu mwingine anaweza kuzitekeleza.

Katika kupambana kufanya shughuli za kishujaa, mwanamume alifaa kuonyesha ujasiri na hata asipofanikisha zoezi lake au akumbwe na changamoto, mwanamume hakufaa kuonyesha hisia. Hata hivyo, mambo haya yamepitwa na wakati kwa kuwa wanaume wa kisasa hawazingatii mila na desturi za jamii ya Waidakho. Hii ndiyo sababu wanaume wengi hawawezi tekeleza kazi za sulubu kama ilivyokuwa hapo awali kwa kuwa hawakupewa chakula kingi na cha kuwapa nguvu. Wengine waliambulia kwenye madawa za kulevya ambazo zimewafanya kuwa viumbe dhaifu ambao hawawezi wajibika katika kukimu familia zao. Jambo jingine ni kuwa, familia nyingi zimelelewa mjini na kusahau utamaduni wao kuhusu mtoto wa kiume. Hata wazazi wengine kwa sababu ya kazi wanazofanya, hawana muda wa kutosha wa kukaa na watoto wao kuwafunza tamaduni za jamii yao.

**7.2 Hitimisho**

Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo; 1) Sifa gani za mwanamume zinajitokeza katika nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za upiganishaji wa fahali katika jamii ya Waidakho? 2) Maudhui ya ubabedume hujitokeza vipi katika nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za upiganishaji wa fahali katika jamii ya Waidakho? 3)

Ishara- maana zipi za kiuana zinazojitokeza katika sherehe za upiganishaji fahali katika jamii ya Waidakho?

Uchanganuzi wa data umebainisha kuwa ubabedume unapatikana katika sherehe za upiganishaji fahali katika jamii ya Waidakho. Ubabedume huu husaidia katika kuelewa sifa za mwanamume kutokana na mila na desturi za Waidakho kumhusu mtoto wa kiume. Kutokana na utafiti huu wa ubabedume, mielekeo na matarajio ya mwanamume katika jamii ya Waidakho inaweza kujitokeza kwa uwazi. Uchanganuzi wa ubabedume katika sherehe za upiganishaji fahali miongoni mwa Waidakho umedhihirika kupitia taswira chanya hata iwapo ni hasi lengo ni kumtukuza mwanamume na kumdunisha mwanamke. Sifa za mwanamume zinazojitokeza katika sherehe hii zinaweka wazi nafasi ya mwanamume katika jamii ya Waidakho ambazo hutoa maudhui yake katika jamii.

Imebainika kuwa, sherehe za upiganishaji fahali zimeeleza mielekeo bora na mitazamo ambayo mtoto wa kiume anafaa kukumbana nazo katika maandalizi ya kuwa mwanamume wa kutegemewa katika jamii ya Waidakho. Hata hivyo, mtu yeyote yule anafaa kuwa mwenye fikra nzuri na kufanya maamuzi ya busara katika kukabiliana na changamoto anazokumbana nayo. Hii imejitokeza wazi katika mapambano ya fahali licha ya fahali wote kuwa na uwezo na nguvu, inabidi fahali mshindi kuibua njia za kushinda mapambano hayo. Kauli hii ina maana kwamba ufanisi wa mwanamume katika hali anayoipitia ngumu ili kutambulishwa kama mwanamume halisi anafaa awe mbunifu na mwenye nguvu. Hivyo katika kufanya utafiti wa masuala ya kiume, nadharia ya ubabedume ni faafu.

### 7.3 Mapendekezo ya Utafiti zaidi

Utafiti huu ulichunguza ubabedume katika sherehe za upiganishaji fahali katika jamii ya Waidakho magharibi mwa Kenya. Ili utafiti wowote uweze kuwa wa manufaa kwa jamii, ni lazima mtafiti aweze kutambua pengo ambalo anahitaji kuliziba na watafiti wa baadaye. Kutokana na muktadha huu, mtafiti anatoa mapendekezo yafuatayo kwa watafiti wa baadaye;

i. Utafiti ufanywe ili kuchunguza nafasi ya mwanamke katika jamii ya Waidakho na kumlinganisha na nafasi ya mwanamume.

ii. Utafiti unaweza kufanya kubainisha ubabedume katika tohara, ngano, au methali za Waidakho.
iii. Changamoto anazokumbana na mwanamke katika kukuza ubabedume na suluhu la kudumu litafutwe.

## MAREJELEO


Barthes, R. (1968). *Element of Semiology*. New York: Macmillan publishers.

Bayyo, F. (2020). *Usawiri wa jinsia ya kiume katika riwaya teule za Shafi Adam Shafi. Tasifu ya Uzamifu. Chuo kikuu cha Dodoma* (haijachapishwa).

Bearak, M. (2021). *A packed funeral, a rollicking bullfight and a message for Kenya's police: "Corona can't stop culture."* Washington Post; The Washington Post. https://www.washingtonpost.com/world/2021/06/13/kenya-bullfight-luhya-litali-funeral/. Accessed 10/02/2023.

Bell, E. & Bryman, A. (2007). The ethics of management research: an exploratory content analysis. *British journal of management*, *18*(1), 63-77.

Brandes, S. (2009). Torophiles and torophobes: The politics of bulls and bullfights in contemporary Spain. *Anthropological Quarterly*, 779-794.

Chepkwony, J., Simiyu, F. W., & Adero, M. (2020). Maudhui katika Nyimbo Teule Kwenye Kipindi cha Rauka. *Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili*, *2*(2), 32-43

Connell, R. (1995). *Masculinities*.Berkey: University of California Press.

Edell, D. (2015). *Urban teenage girls challenge and perpetuate cultural narratives through writing and performing theater. PHD Thesis*. New York University. (Unpublished).

Edwards, T. (2004). *Cultures of masculinity*. New York Routledge publishers.

Foley, L. (2014). *The Last Serious Thing: Modernist Responses to the Bullfight. PHD Thesis. Queen Mary University of London* (Unpublished).

Gay, R. (2000). *Educational Research Conference for Analysis and Application*. (Volume 4). New Jersey.

Hemingway, E. (1932). *Death in the Afternoon*. New York: Charles Scriber's Sons.

Jakinda, O. (2005). *Contingent valuation of livelihood functions and socio-cultural values of cattle in smallholder farms: a case study of Kakamega and Siaya Districts, Kenya. Doctoral dissertation, PHD Thesis. University of Nairobi*. (Upublished)

Kabaji, E. (2005). *The Construction of Gender through the Narrative Process of the African folktale: A case study of the Maragoli folktale. PhD Thesis. University of South Africa*. (Unpublished).

Kabaji, E. (2008). Masculinity and ritual violence: A study of bullfighting among the Kakamega Luyia, western Kenya. *Mila: A Journal of the Institute of African Studies*, *9*, 33-46.

Kenya. *Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili*, *1*(1), 35-41.

Khamala, G. (2009). *Gender Dimension of Ethnic Identies and Conflicts in Kenya: The case of Bukusu. Masters Thesis. Kenyatta University*. (Unpublished)

Kibigo, M. (2019). *Masculinity in the Isukha praise poetry during the ritual of shilembe and the Indegenous Sport of Mayo, the Semantic Perspective. Masters Thesis, Masinde Muliro University* (Unpublished).

Kimmel, M. (2014). After fifteen years: The impact of the sociology of masculinity on the masculinity of sociology 1. In *Men, Masculinities and Social Theory (RLE Social Theory)* (pp. 93-109). Routledge.

Kipury, (2002). *Oral Literature of Masaai*. Kampala: Ujuzi Educational Publishers DSM.

Kiruthu, F., Kapiyo, J. & Kimori, W. (2011). *The Evolving World: A History and Government Course. Form Three. Student's Book*. Oxford University Press.

Kobia, J. & Mung'ahu, R. (2017). Ubabedume katika Ushairi wa Kiswahili: Mfano wa Utenzi wa Fumo Liyongo. *Kioo cha Lugha, 11*(1) 40- 47

Kobia, J. (2008). *Taswira za Kiuana katika Nyimbo za tohara za wanaume miongoni mwa Waigembe. Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Kenyatta*. (Haijachapishwa).

Kothari, C.R. (2004). Research Methodology, Methods and Techniques, (2nd Edition) New Delhi: New Age International, (p) Limited Publisher.

Leach, M. (1994). The politics of Masculinity: An Overview of Contemporary Theory. In *Journal of Social Alternatives,* 12(4), 36-38.

Magambo, A., Simiyu, W., & Amukowa, N. (2019). Mchango wa tamasha za muziki katika ufundishaji wa uainishaji wa nyimbo katika shule za upili nchini

Malala, S. (2018). *Analysis of Representation of Women in Luhya Proverbs. Masters Thesis University of Nairobi* (Unpublished).

Masingu, K. (2013). *Influence of Cultural Activities on living Standards of Rural Dwellers of Ikolomani South Division of Kakamega South Sub-County, Kenya. Masters Thesis University of Nairobi* (Unpublished).

Matinde, R. (2005). *Uchanganuzi wa Ubabedume katika Majigambo ya Abakuria. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Egerton*. (Haijachapishwa).

Mbachi, F. & Likoko, S. (2013). Traditional male circumcision and its implications on the socio-economic and psychosocial life of the Bukusu Community in Kenya. *Research on humanities and social sciences, 3*(1), 218-224.

McCornick, J. (2000). *Bullfighting art, Technique and Spanish Society*. Piscataway, NJ: Transanction Publications.

Miruka, S. (2003). *Oral literature*. Nairobi: East Africa Publishers.

Mitchell, T. (1991). *Blood Sports: A social History of Spanish Bullfighting*. Philadelphia: University of Pennsylvania press.

Mohammed, Z. (2018). Taathira za Ubabedume kwa Mwanamme Mwenza wa Kizanzibari Kupitia Nyimbo za Taarab Asilia Tasnifu ya Uzamifu Chuo Kikuu cha State Zanzibari.

Mutulu, F. (2014). *The Fighting Bulls of Western Kenya*. https://afktravel.com/57076/ fighting-bulls-western-kenya. Accessed 16/01/2023.

Mutunga, W. (2009). Feminist Masculinity: Advocacy for Gender Equality and Equity. *Human Rights NGOS in East Africa. Political and Normative Tensions.* Kampala: Fountian Publishers.

Mwamzandi, I. (2001). Performance Carnival and the Deconstruction of Social Meaning: The case Study of Taarab among the Swahili. *Makala ya Kongamano la kimataifa Kiswahili 200: proceedings, 44.*

Mwayuuli. M. (2003). *The History of the Isukha and Idakho Clans. Among the Abaluyia of Western*. With an introduction by N. Nakabayashi. CUEA Publications.

Nyotuoro, A. (2021*). Bull fighting in Western Kenya*. (n.d.-b). Lughayangu. Retrieved January 19, 2023, from https://lughayangu.com/post/bull-fighting-in-western-Kenya.

Onyango, J. (2007). Masculinities in Kiswahili children's literature in Kenya. *In Nordic journal of Swajili Forum vol 14* (2007): 245-254.

Ouma, S. (2016). *Influence of Cultural Practices on Implementation of Development Projects in Shinyalu Sub- County Kakamega, Kenya. PhD Thesis, University of Nairobi.* (Unpublished).

Parpart, J. & Stichter, S. (Eds.). (2016). *Women, employment and the family in the international division of labour*. Macmilla press limited.

Rita, M. (2014). *The social construction of masculinity among the Chuka through circumcision, 1906-2000 Masters Thesis, Kenyatta University.* (Unpublished.)

Shiracko, N. (2016). A survey of ethnobotany of the Abawanga people in Kakamega county, Western province of Kenya. India.NISCAIR-CSIR Publishers.

Tamale, S. (2005). Eroticism, sensuality and “women's secrets” among the Luhya. *Feminist Africa*, (5), 9-36.

Travel, R. (2020) *Bull Fighting in Western Kenya*. Rickshawtravels.com. Retrieved January 19, 2023, from https://rickshawtravels.com/about/articledetails/Bull-Fighting-in-Western-Kenya/310.

Uchendu, E. (2007). Masculinity and Nigerian youths. *Nordic Journal of African Studies*, *16*(2).16(2): 279-297.

Waita, N. (2004). ‘Gender Conflicts and Oral Art Forms: An Analysis of the Patriach/ Matriach Conflict in inheritance and Resource Control among the Ndia and Gichugu.’ In *Contesting Social Death: Essay on Gender and Culture*. (Pp1-28). Nairobi: Kenya Oral Literature Association.

Walsh, M. (Ed.). (1997). *Women, men, & gender: Ongoing debates*. Yale University Press.

Wambunya, T. (2005). *Luyia proverbs from Kisa Marama Tsotso and Wanga*. London: Luyia Publishing Company.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Wheatsheaf.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi: Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

Wanjala, S. (2007). *Nyiso za Wabukusu; Maendeleo na Mabadiliko ya Lugha na Maudhui. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta*. (Haijachapishwa).

Waswa, B., Chai, F., & Buliba, A. (2022). Nafasi ya Muktadha katika Utendaji wa Mivigha ya Olubeko Miongoni mwa Abanyala wa Kakamega, Kenya. *Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili*, *5*(2), 29-39.

# VIAMBATISHO

**Kiambatisho 1: Nyimbo zilizokusanywa katika sherehe za upiganishaji katika jamii ya Waidakho**

Wimbo 1:

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Vandu varevananga vasatsa vali he* | Watu wanauliza wanaume wako wapi |
| *Vasatsa yavo ×2* | Wanaume ndio hao ×2 |
| *Nutsia wavamenya vasatsa valulayo* | Ukienda kwa maboma zao wanaume ni wakali |
| *Vasatsa yavo ×2* | Wanaume ndio hao ×2 |
| *Ulihe lili vasatsa vasinjila* | kwenye vita wanaume wamesimama tisti |
| *Vasatsa yavo ×2* | Wanaume ndio hao ×2 |

Wimbo 2:

| | |
|---|---|
| *Inzi musatsa ndarumila* | mimi mwanamume nilituma |
| *mangondo muposta* | pesa kwa posta |
| *Mama wanje na mukhali nu wanje* | mama yangu na mke wangu |
| *vakuli khanyama.* | Wanunue nyama |
| *Khandi nindumila khandi mukamba papa wanje* | tena nikatumia baba yangu keshoye |
| *akuli isuti.* | Anunue suti. |

Wimbo 3

| | |
|---|---|
| *Mama yangaya ×2* | mama alinikataza |
| *Mama yangaya khale* | mama alinikataza kitambo |
| *Mama yangaya khale makhuba* | mama alinikataza kitambo mambo |
| *Ka vakhali vavili* | ya kuoa wake wawili |
| *Nuhila vakhali vavili ukona manya shihuvi* | ukioa wake wawili utalala kama mwizi |
| *Mbukono.* | Kwa malazi |
| *Mama yangaya khale ×2* | mama alinikataza kitambo |
| *Yangaya khale makhuva ka vakhali vavili ×2* | alinikataza mambo ya kuoa wake wawili |
| *Nuhila vavili ukona ninzala munda* | ukioa wawili utalala na njaa |
| *Mama yangaya ×2* | mama alinikataza |
| *Mama yangaya khale* | mama alinikataza kitambo |
| *Mama yangaya khale makhuba* | mama alinikataza kitambo mambo |
| *Ka vakhali vavili* | ya kuoa wake wawili |
| *Nuhila vakhali vavili ukona manya shihuvi* | ukioa wake wawili utalala kama mwizi |
| *Mbukono.* | Kwa malazi |
| *Mama yangaya khale ×2* | mama alinikataza kitambo |
| *Yangaya khale makhuva ka vakhali vavili ×2* | alinikataza mambo ya kuoa wake wawili |
| *Nuhila vavili ukona ninzala munda* | ukioa wawili utalala na njaa |

Wimbo 4

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Khwenyanga khutsi khungo* | Tunataka twende nyumbani |
| *Hango hu khwalekha vulimu vyayumba* | nyumbani tulikotoka pamegeuka msitu |
| *Khwenyanga khulikorela Mombasa ×2* | unataka tupotelee Mombasa ×2 |
| *Mushiele wanje khutsi khungo* | mke wangu twende nyumbani |
| *Ooh mukhali wanje* | ooh mkwe wangu |
| *Khutsi khungo* | twende nyumbani. |

Wimbo 5

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Ulwa ingwe ulwa isimba nihuma* | ukiskia chui uskie samba ikiguruma |
| *Vandu vasatsa vechanyanga vandu varia* | wanaume wanashangaa watu ni waoga |
| *Khali kuve vutukhu ama mbasu vandu varia* | hata iwe usiku ama mchana watu ni waoga |
| *Musatsa nachingi shikong'o shie* | Mwanamume akibeba klabu yake |
| *Vandu varia* | watu ni waoga |
| *Khali vasatsa valangwa mulihe* | khali vasatsa valangwa mulihe |
| *Vatsiku varia* | maadui wanaogopa |

Wimbo 6

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Kuka mbe shikongo shiange* | Babu nipe klabu yangu |
| *Mbee shikong'o shianje ×2* | Nipee klabu yangu |
| *Nzi khuserera isecheli* | niende kuwatongoza wanawake Isecheli |
| *Ukhasera tawe ×2* | Usiwatongoze wanawake |
| *Ulasila khumurego* | utaanguka mtegoni |
| *Mukhaki wo Narikale na vina.* | Mke wako atabaki na nani |

Wimbo 7

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Nunyoli lingangule* | ukipata malaya |
| *Fwalaa* | Vaa |
| *Fwala ikondomu* | vaa kinga |
| *Khali nali mukhali wa mundu* | hata awe mke wa wenyewe |
| *Fwalaa* | Vaa |
| *Fwala ikondomu* | vaa kinga |

Wimbo 8

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Nulangwaa* | Ukiitwa |
| *Eeeh* | Kubali |
| *Nulangwa* | Ukiitwa |
| *Uvolenge ndi hanu* | unaitika unasema niko hapa |
| *Musatsa nalangwa,* | mwanamume akiitwa |
| *Eeeh* | Eeeh |
| *avolenge ndihanu.* | Aitike na aseme niko hapa |

Wimbo 9
Wanaweza,
Wanaume
Wanawezaa
Hata kama itachukuwa muda
Wanaume tunaweza.
Hata kwa dhiki,
Tunaweza hata kama itachukuwa muda
Wanaume tunaweza.

Wimbo 10

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Mulina wanje murende wanje* | Rafiki wangu jirani wangu |
| *Ooh eeh! ooh eeh !* | ooh eeh ooh eee |
| *Mbele khureve ni watila khushindu shindu shiumundu* | Nilifaa nikuulize kama umewahi shika kitu cha mtu. |
| *Isisi ni wanje ivweru ni wowo* | Chumba cha kulala ni change na sebuleni ni kwako |
| *Ooh eeh !ooh eeeh!* | Ooh eeh ooh eeeh |
| *Mundu mukhali mbele khureve ooh eeh* | mwanamke nilitaka kukuuliza ooh eeh |
| *Nu watila khushindu shiu mundu* | Kama ushawahi shika kwa kitu cha mtu |

Wimbo 11

| | |
|---|---|
| *Yandeva mukhali wanje yandevaa* | mke wangu aliniuliza |
| *Yandeva ukoni hena mudansi totoo* | aliniuliza nilikolala kwa dansi |
| *Yandeva ukoni hena mudansi mapaka mavweve* | aliniuliza nlilikolala kwa densi hadi asubuhi |

Wimbo 12

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Mbele khu luchendo nzitsanga ×3* | niko safarini naja |
| *Hambi vosi khukhonyane luchendo* | mwanaume wote njooni tusaidiane |
| *Vashiele veru vakhusuvila* | wake zetu wanatutegemea |
| *Khuluchendo* | kwa safari |
| *Hambi vosi khukhonyane luchendo* | njooni wote tusaidiane safari. |

Wimbo 12

| **Kiluhya** | **Tafsiri** |
|---|---|
| *Ulwa ingwe ulwa isimba nihuma* | La kushangaza ukiskia sauti ya chui au samba |
| *Vandu vasatsa vechanyanga vandu varia* | Wanaume wanashangaa watu ni waoga |
| *Khali kuve vutukhu ama mbasu vandu varia* | Hata iwe usiku ama mchana watu ni waoga |
| *Musatsa nachingi shikong'o shie* | Mwanamume akibeba klabu yake |
| *Vandu varia* | Watu ni waoga |
| *Khali vasatsa valangwa mulihe* | Ata wanaume wakiitwa vita |
| *Vatsiku varia* | Maadui wanaogopa |

**Kiambatisho 2: Picha ya Mtafiti katika sherehe za kupiganisha fahali**



## Kiambatisho 3: Ramani ya Eneo la Ikolomani



**Kiambatisho 4: Maswali ya Hojaji (dodoso) kwa Fanani na Wenyekiti wa Maandalizi ya Upiganishaji Fahali**

Mimi ni mwanafunzi wa Chuo kikuu cha Chuka katika Kaunti ya Tharaka Nithi. Ninafaya utafiti wa kiusomi kuhusu Ubabedume katika nyimbo za upiganishaji fahali katika jamii ya Waidakho. Hivyo, unaombwa kuijaza hojaji hii kwa uangalifu na uamilifu. Usiri utahifadhiwa na majibu utakayotoa yatatumiwa kwa madhumuni ya utafiti huu tu na si vinginevyo. Basi, unaombwa ushirikiano wa dhati katika kukamilisha kazi hii.

1. Maelezo ya binafsi

   Jinsia ……………………………………………

   Umri…………………………………………….

   Jina la kijiji………………………………......

2. Nyimbo zinazoimbwa wakati wa upiganishaji fahali huwa na dhamira gani kwa wanajamii wa Idakho?

   ……………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………

3. Je, mwanamume anapewa sifa zipi katika nyimbo hizo?

   ……………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………….

4. Mwanamke ana nafasi gani katika jamii ya waidakho katika kujitambulisha kama mwanaume kamili?

   ……………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
….

5. A) Je, miviga ya upiganishaji fahali una ishara zipi za kiuana katika jamii ya Waidakho?

Ndio……………… La…………………

b) Iwapo zipo taja ishara zozote za kiuana zinazojitokeza katika miviga ya upiganishaji wa fahali
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
………………………………………

c). Ishara ulizozitaja (5b) zina maana gani?
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………
…..

**Kiambatisho 5: Orodha ya Wasailiwa**

Msailiwa 1: Mwachi Evans mwenye umri wa miaka 55 kutoka Bushirika

Msailiwa 2: Kwatemba Nelson mwenye umri wa miaka 60 kutoka Malinya

Msailiwa 3: Brian Kakati mwenye umri wa miaka 50 kutoka Musoli

Msailiwa 4: Luyuku Francis mwenye umri wa miaka 52 kutoka Madivini

**Kiambatisho 6: Idhini kutoka kwenye Tume ya Maadili**

**CHUKA UNIVERSITY**

**Knowledge is Wealth *(Sapientia divitia est)* Akili ni Mali**

**CHUKA UNIVERSITY INSTITUTIONAL ETHICS REVIEW COMMITTEE**

Telephones: 020-2310512/18
Direct Line: 0772894438
Email: info@chuka.ac.ke,
P. O. Box 109-60400, Chuka
Website: www.chuka.ac.ke

**19th March, 2024**

**REF: CUIERC/ NACOSTI/505**
TO: **Austine Indulagi Asalache**

**RE: Ubabedume Katika Sherehe za Upiganishaji Fahali Katika Jamii ya Waidhakho Magharibi Mwa Kenya.**
This is to inform you that *Chuka University IERC* has reviewed and approved your above research proposal. Your application approval number is *NACOSTI/NBC/AC-0812.* The approval period is 19th March, 2024 – 19th March, 2025.

This approval is subject to compliance with the following requirements;

i. Only approved documents including (informed consents, study instruments, MTA) will be used
ii. All changes including (amendments, deviations, and violations) are submitted for review and approval by *Chuka University IERC*.
iii. Death and life threatening problems and serious adverse events or unexpected adverse events whether related or unrelated to the study must be reported to *Chuka University IERC* within 72 hours of notification
iv. Any changes, anticipated or otherwise that may increase the risks or affected safety or welfare of study participants and others or affect the integrity of the research must be reported to *Chuka University IERC* within 72 hours
v. Clearance for export of biological specimens must be obtained from relevant institutions.
vi. Submission of a request for renewal of approval at least 60 days prior to expiry of the approval period. Attach a comprehensive progress report to support the renewal.
vii. Submission of an executive summary report within 90 days upon completion of the study to *Chuka University IERC*.

Prior to commencing your study, you will be expected to obtain a research license from National Commission for Science, Technology and Innovation (NACOSTI) https://oris.nacosti.go.ke and also obtain other clearances needed.

Yours sincerely

**Dr. Benjamin Kanga**
**SECRETARY**

## Kiambatisho 7: Idhini kutoka NACOSTI

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 290505

Date of Issue: 25/April/2024

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Mr.. AUSTINE INDULAGI ASALACHE of Chuka University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Kakamega on the topic: UBABEDUME KATIKA SHEREHE ZA UPIGANISHAJI FAHALI KATIKA JAMII YA WAIDAKHO MAGHARIBI MWA KENYA for the period ending : 25/April/2025.**

License No: NACOSTI/P/24/34985

**290505**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**